

# *MAKAO YA BAADAYE YA*

## *BWANA ARUSI WA MBINGUNI*

### *NA BIBI-ARUSI WA DUNIANI*

 Na tuendelee kusimama muda kidogo, tunapoinamisha mioyo yetu sasa mbele za Mungu.

<sup>2</sup> Baba yetu wa Mbinguni, kweli tunashukuru sana kwa majaliwa ya kuwapo hapa leo, tumekusanyika pamoja katika Jina la Bwana Yesu. Tunaomba utusamehe dhambi zetu, na kwa kuwa tuko hapa kuielekeza mioyo yetu kwenye mambo ya Milele na Uzima ulio ng'ambo ya huu upatikanao na mauti. Sasa tunaomba ya kwamba utatupa maagizo Yako, ya jinsi ambavyo itupasavyo kugeuka, mambo gani yatupasayo kufanya katika siku za usoni, na hata katika wakati huu sasa, kupapata mahali pale ambapo tunaninii... tumeahidiwa.

<sup>3</sup> Kuna wengi walio wagonjwa na wenyewe haja nchini, nao hawajaikamilisha safari yao. Naye adui yetu mkubwa, si adui yetu tu, bali adui Yako, amekuja kuwashambulia na ku—na kuyakomesha maisha yao, na kuwapeleka ka—kaburini kabla ya wakati wao. Nasi tunawaombea, leo, ya kwamba Wewe na rehemza Yako na neema, Bwana, utaziongezea siku zao zifike kwenye wakati uliokusudiwa.

<sup>4</sup> Jukwaani, ama mimbarani, hapa kuna leso na vifurushi. Na huko nje kwenye kumbi na kuzunguka mahali hapa, ni hao walio kwenye vitanda vidogo, machela, wagonjwa na wanaoteseka, wakisimama kati ya wasikilizaji wakiwa hawana nguvu za kutosha kusimama.

<sup>5</sup> Ee Mungu Milele, Mbarikiwa, naomba uyasikie maombi yetu asubuhi ya leo, kwa Damu ya Bwana Yesu; usiangalie ouvu wetu, bali tukijua ya kwamba Yeye alisimama badala yetu, na Yeye Ndiye anayetuwalishaa kwa maombi haya. Naomba kila mmoja na kila mtu aponywe kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana.

<sup>6</sup> Bariki leso hizi. Zitakapowekwa juu ya wagonjwa, naomba waponywe.

<sup>7</sup> Na sasa, Baba, huku tukisubiri ile ibada kuu ya kuponya, tunayoamini itafuata, tupasulie njia ya Uzima, Bwana, tupate kujua kwa Neno Lako yale yatupasayo kufanya. Kwa maana tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>8</sup> Kwa kawaida, haya yanahesabiwa mojawapo ya majaliwa yangu makuu sana, ni kuwa katika nyumba ya Mungu

na kuzungumza na watu Wake. Na sasa najua watu wamesongamana sana, nami nina somo refu sana. Kwa hiyo mimi nina...mimi ni—ninatumaini kwamba mtaenea, vizuri iwezekanavyo, mpaka tutakapomaliza Ujumbe.

<sup>9</sup> Sasa, kuna joto, lakini tunashukuru kwa ajili ya vibaridishi. Lakini, kundi kubwa namna hii, hakuna mtambo wa kubaridisha hewa ungalizeza kulishughulikia, mnaona, kwa sababu mwili wako mwenyewe ni mtambo, kama nyazi joto tisini na nane, na daima unatoa joto, na huku mmesongamana. Lakini mimi na—natumaini kwamba Mungu atawafanya mkae starehe kama Yeye awezavyo.

<sup>10</sup> Na wakati tumeingia, tunapofanya mikutano kama huu, ni—nisingewafanya mje hapa, kwa vyo vyote, kama sikufikiria ilikuwa kwa ajili ya kuwasaidia, kama sikufikiria ya kwamba ilikuwa ikiwasaidia, na ya kwamba mngefaidika, kuja. Na tena, nikijua pia ya kwamba hatuna muda mrefu mno zaidi wa kufanya hivi, ya kwamba tuna—tunafikia kwenye mama—masaa yenye ya mwisho kabisa, na mimi—na mimi nataka kutumia kila dakika, niwezayo, kwa ajili ya Ufalme Wake. Na sasa ninatumaini ya kwamba Bwana Mungu atatubariki tunapokutanika.

<sup>11</sup> Na nataka kuwapongeza, ya kwamba, jana nilikuwa nikitembelea mahali mbalimbali, huko nje nikiwaona baadhi ya wagonjwa na wanoteseka, kwenye hoteli, nami nikakutana na baadhi ya mameneja juma hili, kwenye baadhi ya mikahawa. Kwa mfano, nilikuwa kule kwenye Ranch House juma hili, karibu na hapa, na meneja alinipa mkono tulipoanza kutoka. Naye akasema, aliniita, “Ndugu Branham.” Sijui alinijuaje. Ndipo akasema... .

Nikasema, “Wewe ndiwe meneja?”

<sup>12</sup> Akasema, “Mimi ndiye mwenye mali.” Kwa hiyo basi akasema, “Naam, watu wako huja hapa kula, kutoka kule chini.” Kasema, “Wao... .”

Nami nikasema, “Vema, nadhani wanajazana kwa wingi sana mahali hapa.”

<sup>13</sup> Akasema, “Bwana, hilo ndilo kundi moja la watu wazuri sana niliopata kuona.” Akasema, “Kwa kweli ni wazuri sana.”

<sup>14</sup> Nilienda kwenye hoteli moja jana, kumwona bibi mdogo niliyetaka kuzungumza naye, baba yake na mama yake walikuwepo, nami ilinibidi kumwendea meneja nipate kujua ho—hote... .chumba walichomweka.

<sup>15</sup> Akasema, “Na wewe ni Ndugu Branham?” Huko ni kule kwenye Oaks.

Ndipo nikasema, “Naam, bwana.”

<sup>16</sup> Akasema, “Ninataka kukupa mkono.” Akasema... . Akanitambulisha kwa mkewe; mtu na mkewe wazuri sana.

Wakasema, "Kila mtu kwenye hoteli hii anahudhiria ibada zako. Tumeiweka kwa ajili yao." Kisha akasema, "Wateja wetu wengine wote tuliwakatalia."

Nami nikasema, "Vema, ninakushukuru kwa ajili ya jambo hilo."

<sup>17</sup> Yeye kasema, "Ndugu Branham, kundi moja la watu wazuri sana niliopata kuona, ni watu wanaokuja hapa, wanaohudhuria mikutano yako."

<sup>18</sup> Jana usiku nilimtembelea rafiki yangu, Bw. Becker hapa chini, na sikuzote nilipenda sambusa zake. Yeye ni ninii sana... Yeye, nilimjua nilipokuwa mvulana; nimemjua maishani mwangu mwote. Kulikuweko na mtu na mkewe walioketi pale kutoka kwenye—kwenye mahali pale pa zamani, kule kwenye Hoteli ya Riverside kule chini. Kwa hiyo wao... Bw. Becker akasema, "Billy?"

<sup>19</sup> Nikasema, "Ni kitu gani, Homer?" Tunajuana vizuri sana.

Akasema, "Ninawalisha watu wako wote juu kule."

<sup>20</sup> Yapata watu mia mbili, ama kitu kama hicho, kila Jumapili, hula kwenye Blue Boar. Na kila niendako, ninasikia matamshi ya jinsi mlivyo watu wazuri.

<sup>21</sup> Jamaa huyu akasema, "Kule chini kwenye—kwenye Riverview kule chini," kasema, "mahali pale pote pamechukuliwa na watu wanaohudhuria huu mkutano." Kasema, "Kuna mamia ambao hawataweza kuingia."

<sup>22</sup> Kwa hiyo, kuwa hivyo, kwangu mimi ninyi ndio chumvi ya dunia. Ni—ninashukuru sana kujuja ya kwamba nina majaliwa ya kuwahubiria watu ambao hata wenyе dhambi na watu... Sisemi watu hawa ni wenyе dhambi, lakini ninamaanisha watu ambao, biashara na kadhalika, wanaoweza kusema ya kwamba ninyi ni watu wazuri, nao wanawapenda katika biashara zao, kwenye sehemu zao. Mwajua, huko ni kukolea chumvi. Ninapenda jambo hilo, mwenendo wenu, jinsi mnavyojali mambo.

<sup>23</sup> Daima nimesema, "Kama mtu akiingia na hana, hana pesa za kujilipia chakula, nipigieni simu tu." Mnaona? Nikasema, "Tutashughulikia jambo hilo." Na nimesema, "Wapeni chakula sikuzote, kama wana pesa au hawana." Mnaona, cho chote kiwezakanacho.

<sup>24</sup> Ninajisikia ninyi ni watoto wangu. Ninyi—ninyi ndio nyota ambazo mimi... Kama nitapata kuwa na moja nitakapofika kule, ninyi mtakuwa ndio lulu hiyo, sehemu inayong'aa sana, kwenye—kwenye taji ya huduma yangu. Itakapotiwa taji, ninyi ndio mtakaokuwa lulu hiyo.

<sup>25</sup> Nami nimekuwa nikiwaambia, katika nyakati zilizopita, huhusu zile Muhuri Saba, zile Nyakati za Kanisa, na yale mambo ambayo—ambayo yamekuwa yakinende.

<sup>26</sup> Na sasa, asubuhi ya leo, nina somo muhimu sana. Kwangu mimi, ni lenye baraka sana. Ninatumaini litawagusa jinsi iyo hiyo. Na laiti tu ningalilileta katika uvuvuio ule ule niliolipokelea, lingekuwa jambo zuri sana, lakini hilo litakuwa ni juu ya Mungu kufanya jambo hilo.

<sup>27</sup> Nimekuwa nikiwaambia juu ya ni *wapi* na ni *nini* kinatukia, nasi tunaona mambo haya yote yakitendeka.

<sup>28</sup> Sasa ninazungumza, asubuhi ya leo, juu ya: *Makao Ya Baadaye ya Bwana Arusi Wa Mbinguni Na Bibi-Arusi wa Duniani*, mahali watakapoishi. Na, kwa kuwa, ninatumaini ya kwamba kwa neema ya Mungu sisi sote ni sehemu ya uchumi mkuu wa Mungu.

<sup>29</sup> Na sasa na—natumaini ya kwamba mtanivumilia, chukueni Biblia zenu, penseli zenu, ama cho chote mfanyakacho kusoma pamoja nami, maana nitarejea kwenye Maandiko mengi. Nikijaribu kumaliza kwa wakati mzuri tupate kuwaombea wagonmjwa; nami niliahidi jambo hilo. Mmekuwa mkiomba kwa kitambo kidogo kilichopita, vyumbani na kila mahali, kwa ajili ya wale amba karibu hawajiwezi na hawana matumaini.

<sup>30</sup> Na, Bwana akipenda, labda nitakuwa na ibada nyingine tarehe kumi na sita, labda tu maombi kwa wagonjwa.

<sup>31</sup> Naanza likizo yangu sasa. Tangu Januari iliyopita, nimekuwa nikisafiri, na nitarudi hapa. Nitakuwa hapa. Naipeleka jamaa yangu Tucson asubuhi, kisha nitarudi kutumia wakati hapa Kentucky, pamoja na baadhi ya rafiki zangu, kuwindia, na kuwindia kindi, kwa majuma kadha, ama labda siku saba ama nane, siku kumi, zo zote zile, isipokuwa Bwana aniongoze mahali pengine. Sijui kamwe, ni mahali gani hasa mtu utakakokuwa; hatujui jambo hilo kamwe, kwa maana hilo limo mikononi mwa Mungu, Mungu peke yake.

<sup>32</sup> Sasa kwa ajili ya somo hili muhimu sana, sisi—sisi... Ninakisia, kama nigechukua muda wangu juu ya jambo hili, kwa vile huna budi kuingiza mambo mengi, ingechukua majuma mengi. Lakini nimeandika Maandiko machache, muhtasari mdogo, kugusia tu mambo yake yaliyo muhimu, kufikia mahali ambapo itawaacha msome kwa bidii.

<sup>33</sup> Halafu hivi karibuni, labda, Bwana akipenda, kwenye Octoba, sijui ni lini, bali wakati wo wote Yeye atakaporuhusu, ningetaka kuchukua si—siku chache, za mfululizo tu wa mikutano, kweye sura ya 12 ya Ufunuo, kuiunganisha na hii hapa. Loo! ninaamini lingekuwa jambo lenye utukufu sana. Lingekuwa lenye utukufu tu. Lingekuwa jambo la utukufu kuona jinsi Yeye alivyofanya.

<sup>34</sup> Halafu, sisi tukija pamoja sasa, nilisema jambo usiku, nilisema, "Mwajua, wakati mimi..." Asubuhi, kama ilivyo kila asubuhi, nafikiria, "Nitakaposhuka kuja hapa, nitamsalimu kila mmoja wa rafiki zangu aliyeko." Sasa nitafanyaje jambo hilo?

<sup>35</sup> Pamoja nami hapa, nina rafiki yangu mpenzi, Daktari Lee Vayle anayeketi hapa nyuma, mkewe mzuri sana na binti yake. Na Ndugu Roy Borders, na, rafiki, Ndugu Ruddell, Ndugu Beeler, na Ndugu Palmer, na Ndugu Jackson. Na, loo, jamani! nanii—nanii... Hao ndugu wapenzi kutoka sehemu zote mbalimbali! Ndugu Anthony Milano, na, loo! kila mahali unapoangalia, unamwona ndugu mwingle fulani! Kutoka kule Arkansas, siwezi kukumbuka majina yao; Ndugu John, Ndugu Earl Martin, na Ndugu Blair. Na, loo! kuna tu... ninyi... Kweli haina mwisho, mnaona. Nina furaha sana kuwa na kundi kama hilo limenizunguka ninapofundisha Neno la Mungu, watu ambaio ninafikiri ni watu mashujaa, watu halisi wa Mungu.

<sup>36</sup> Ninashukuru kwa ajili ya maskani hii ndogo. Ninashukuru kwa ajili ya milango yake mitano iliyo wazi kwa watu wote. Kila mlango... Tuna mashemasi wanne hapa, watu walijazwa na Roho; wadhamini wanee, watu walijazwa na Roho. Yaani wawili kwenye kila mlango. Na ina milango miwili upande wa mbele, kwa ajili ya mapasta wawili, wachungaji.

<sup>37</sup> Tuna furaha kuwa nanyi; tunamshukuru Mungu kwa jambo hili. Na Yeye awabariki daima.

<sup>38</sup> Sasa tunataka kusimama kidogo tu, tunaposoma kutoka kwenye Petro wa Pili sura ya 3, na pia kutoka Kitabu cha Ufunuo 21.

<sup>39</sup> Tunaposimama, Ee Bwana, ijaze mioyo yetu na furaha kwa sababu ya kusomwa kwa Neno Lako, tukijua ya kwamba Yesu amesema, ya kwamba, "Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatashindwa." Kujua tena ya kwamba Yeye alisema, "Maandiko yote hayana budi kutimizwa." Na tunaposoma mambo haya, na tuwe na ufahamu kutoka Kwako, saa ambayo tunaishi. Tunaomba katika Jina la Yesu, Mwandishi wa Kitabu hiki. Amina.

<sup>40</sup> Petro wa Pili 3.

*Wapenzi waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi;  
katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa kule  
kuwakumbusha,*

*Mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa  
zamani na manabii watakatifu, na zile amri za Bwana  
na Mwokozi zilizoletwa na mitume wenu.*

*Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku  
za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye  
kudhihaki, wafuataao tamaa zao wenyewe,*

*Na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?...  
(Kama hilo halipatani na huyu mwanamke kafiri!)...  
na tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa  
hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa.*

*Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji, kwa Neno la Mungu;*

*Kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.*

*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.*

*Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.*

*Sasa, Bwana hakawii kutimiza ahadi yake, kama watu wengine wanavyokudhani kukawia; bali huvumilia kwetu maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*

*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi usiku; katika siku hiyo mbingu na nchi, kwa mshindo mkuu... zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vyatya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*

*Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imetupasa sisi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa,*

*Mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kule kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vyatya asili vitateketea na kuyeyuka?*

*Lakini, kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.*

*Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili msionekane... ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa na bila aibu.*

*Nanyi mkiuhesabu uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na... yetu mpenzi Paulo amewaandikia kwa hekima aliyopewa;*

*Vile vile... nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, hupotoa, kama—kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjivu wao wenywewe.*

*Basi, wapenzi, mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa... na kosa la hao wahalifu, mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.*

*Lakini, kueni katika neema, . . . katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele. Amina.*

<sup>41</sup> Sasa katika—katika Ufunuo wa Kristo, kwenye sura ya 21, ninasoma Maneno haya.

*Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.*

*Nami Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*

*Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na mwanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, na kuwa Mungu wao.*

*Naye Mungu atafuta kila chozi katika macho yao; wala mauti haitakuwapo tena; wala kuomboleza, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*

*Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia, Andika: kwa kuwa maneno hayo ni amini na kweli.*

*Akaniambia, Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi za maji ya uzima bure.*

*Yeye ashindaye atayarithi mambo yote, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu.*

Na tuombe tena.

<sup>42</sup> Bwana Yesu, kwa ahadi kama hiyo na usemi mkali kama huo ambao Yesu Mwenyewe pamoja na yule mtume ametutolea kuhusu ile saa tunayokaribia, tupe, Ee Bwana, yahusuyo mwelekeo Wako, tupate kujua jinsi ya kukaribia jambo hili kwa njia inayofaa. Kwa sababu, linakuja, tunajua. Maandiko hayana budi kutimizwa, na basi yatatimizwa. Na sasa, Bwana, tunaomba rehema Yako tena juu yetu sote, tunapojifunza Neno Lako. Uwe pamoja nasi na utufunulie Hilo, Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

<sup>43</sup> Sasa, sijui kama kungeweza kuwa na njia ambayo labda, labda wanaweza kuzima taa nytingine za ukumbi, na kuziacha tu za hapa jukwaani, jambo ambalo labda lingekuwa ni afadhali, na kupunguza umeme kidogo. Karibu tuunguze mtambo wa kurekebisha nguvu za umeme, usiku wa juzi. Na kama mlinzi

atatufanya jambo hilo, tungefurahia kuzimwa kwa taa za chini, taa za ukumbi wenyewe zizimwe. Ndipo nafikiri mtakuwa na nafasi kubwa ya kuona, ya kuandika.

<sup>44</sup> Sasa, somo langu tena, kulitangaza, kwamba tunaelekeea kwenye so—somo la: *Makao Ya Baadaye Ya Bwana Arusi Wa Mbinguni Na Bibi-Arusi Wa Duniani*.

<sup>45</sup> Sasa kwa vile kumekuwa na ninii... Itanilazimu tu kufanya jambo hili. Kuna joto sana kupita kiasi hapa, mnaona. Naam, bwana. Tunapo ninii... Najua mke wangu hataki nifanye hivyo; lakini, hivyo, kutoa koti langu. Kuna joto sana kupita kiasi hapa. Mnaona, ninyi huko mnapata hewa, na imezuiwa tu kwenye kizimba kidogo hapa, mnaona. Sasa, katika siku za—za usoni, ama...

<sup>46</sup> Katika siku zilizopita, hasa, tumejifunza *Zile Muhuri Saba, Zile Kanisa Saba*. Ndugu Vayle na hao wengine wanashughulikia hayo sasa, kwa uaminifu, kuyaweka katika namna ya kitabu.

<sup>47</sup> Na tukiona vitu hivi vyote vya siri ambavyo tumeona vikitimia, ndipo ninafikiri, baada ya kufahamu jambo hilo, katika saa tunayoishi, na mahali pale; hakuna mtu angalitaka kuketi akiwa na akili timamu kweli na kuchunguza yale yaliyokwisha kunenwa, na yale yanayoahidiwa kutokea, na yale yaliyokwisha kutokea, ila yule angeweza kusema ya kwamba mambo hayo yametimia. Mnaona? Yale hasa Mungu aliyosema angefanya, amefanya hivyo juu ya alama kabisa. Mnaona?

<sup>48</sup> Sasa, nafikiri katika jambo hili, ya kwamba, bila kujuu ni wakati gani Bwana Yesu aweza aje, nilifikiria lingekuwa jambo zuri, ilionekana inampendeza Roho Mtakatifu ya kwamba tungezungumzia kuhusu jambo hili, basi; na labda tulirudie tena, mara mbili au tatu, kwa sababu sitakuwa kabisa na wakati wa kutosha kuyatoa haya yote.

<sup>49</sup> Kama vile ambavyo unagusa so—somo ambalo huenda likawa linamkwaza kidogo mtu fulani, huwezi kulifafanua kabisa kulifanya dhahiri, kisha unarudi tena kuchukua somo linalofuata.

<sup>50</sup> Na halafu baadaye, katika...kama Bwana akipenda, tunafikia kwenye ya 12, muhuri, ama si... Samahani. Sura ya 12 ya Ufunuo, ambayo iko katikati ya kule Kuja kwa Bwana na ule mwisho wa zile Baragumu, na kadhalika. Tutajiribu kurudisha hilo, kuonyesha Shetani ni nani, na yale aliyofanya, alitoka wapi, na kusudi lake ni nini, na jinsi ambavyo uzuri wake mkuu aliopewa ulivyosababisha kuanguka kwake. Uongo wake ulisababisha kule kuanguka; uzuri.

<sup>51</sup> Halafu, jinsi isivyowezekana kwa mtu ye yote anayetaka kuangalia jambo hilo kwa usahihi, huo “uzao” wa nyoka. Ningesai kwa ajili ya jambo hilo, kwa mtu ye yote, mnaona, ambaye angetaka kuangalia jambo hilo, kwa—kwa ufahamu wa

kawaida kabisa. Mtoto anaweza kuona jambo hilo. Mnaona? Sasa, nasi tutafikia jambo hilo baadaye.

<sup>52</sup> Sasa, tunafahamu hapa ya kwamba Maandiko haya mawili... Sababu ya mimi kusoma Petro wa Pili sura ya 3, na kuilinganisha na Ufunuo 21, zote mbili hapa zinazungumzia somo lile lile, lakini Yohana kamwe—kamwe hakuliandika kama Petro alivyoliandika. Mnaona? Tunafahamu ya kwamba Makao haya makuu ya Bibi-Arusi yatakuwa hapa duniani.

<sup>53</sup> Na sasa kama ukisoma, kama tu sura ya 21, sura ya 21 ya Ufunuo, mtume hapa alisema, ama nabii alisema, ya kwamba, “Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya.” Inasikika kana kwamba kunakuja maangamizi.

<sup>54</sup> Sasa, jinsi ninavyopata Jumbe zangu ni kwa maombi. Nitakuwa nimeketi katika maombi ndipo ninafunuliwa jambo fulani. Ndipo ninalingojea dakika chache na kuona kama ni kweli, halafu nalisikia likija karibu. Na basi wakati mwagine ninaendelea kungoja mpaka ono linatokea. Lakini linapoanza kuja, nami nimeridhika linatoka kwa Mungu, ndipo huenda kwenye Maandiko. Mnaona, yaani, yanapaswa kuwa ndiyo thibitisho la kila jambo la kiroho linalotendwa, maana Biblia ndiyo ufunuo mkamilifu kwa Yesu Kristo; mnaona, Ndiyo Mwili Wake.

<sup>55</sup> Na sasa, katika jambo hilo, labda ninapata mahali katika Maandiko ambapo hapasikiki tu sawa, nami nitashangaa. Ninarudi tena kwenye maombi. Linakuja tena. Ndipo ni—ndipo ninaanza ku—kuyachunguza Maandiko yangu.

<sup>56</sup> Sasa, Biblia yetu imeandikwa katika Kiingereza, na maneno ya Kiingereza hubadilika, kila wakati. Kwa mfano, kama vile Yohana 14, ilivyosema, “Katika nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi,” makao katika nyumba. Vema, basi, wewe, utakavyofanya na jambo hilo basi, ni kulifuatilia mpaka kwenye—kwenye la asili uone vile James ilivyomaanisha, ama urudi kwenye ya Waebrania, ama kwenye ya Kiyunani, kutoka kwenye ile fasiri ya kwanza. Na pale inasema, “Katika ufalme wa Baba Yangu kuna majumba mengi ya kifalme.” Vema, basi, unarudi kwenye wakati ambapo wale wafasiri walimfasiria Mfalme James, *ufalme* uliitwa, katika Kiingereza, “nyumba,” naye mfalme alikuwa ndiyo baba juu ya raia wake. Hiyo ndiyo sababu walifasiri, “Nyumbani mwa Baba Yangu kuna makao mengi.” Mnaona? Na basi unachukua maneno hayo nawe inakubidi kuyachunguza.

<sup>57</sup> Halafu, mnaona, kutokana na uvuvio huo... Mimbara hii asubuhi ya leo, ninasema, hakuna hata wakati mmoja ambapo haijakuwa moja kwa moja, Maandiko. Hivyo ndivyo *Uzao Wa Nyoka* na mambo haya mengine yote yanavyokuja. Mnaona? Kwa...

<sup>58</sup> Nay o ni, kweli, kama mtu fulani angesoma tu na kusema, “Nyumbani mwa Baba Yangu kuna makao mengi,” kama hukusimama ukachunguza, ukaomba, utachanganyikiwa kabisa. Mnaona? Lakini endelea tu kuomba. Mungu daima fulifanya sawa iwapo linatoka kwa Mungu.

<sup>59</sup> Sasa, Yohana anaeleza badilisho na ninii... jinsi linavyotukia... Yeye halielezei, hasa, lakini Petro analielezea. Yohana alisema tu, “Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya; mbingu za kwanza na nchi ya kwanza imekwisha kupita. Hapana bahari tena. Nami Yohana nikaona Mji ule mtakatifu ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama Bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.” Lakini, tunageuka nyuma kwa Petro wa Pili sasa tuone, Petro anaeleza jinsi tendo hili lenye hatua mbalimbali litakavyotukia. Sasa, kama ungechunguza yale ambayo Yohana alisema, inasikika kama, “Kwa kuwa mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita,” zimetoweshwa kabisa. Mnaona, halafu, hilo linasikika la kustaa jabisha sana. Kwa hiyo hilo ndilo lililonigusa mimi, nami nikaanza kutafuta neno, “kupita.” Na, sasa, lakini ni dhahiri kwamba haya yote mawili, ya mtume na ya nabii, yalikuwa yanazungumzia jambo lile lile.

<sup>60</sup> Na sasa, pia, katika Kitabu cha Isaya, sasa, ikiwa mnataka kuandika Maandiko haya, katika Isaya 65:17. Isaya, akinena juu ya ule Utawala wa Miaka Elfu, miaka hiyo elfu moja ya kupumzika kwa—kwa ajili ya watu wa Mungu. Isaya alinena habari zake, naye alisema, “Mimi... Kulikuweko na... Mambo yote ya kale yamekwisha pita,” na jinsi watakavyojenga nyumba, na kukaa ndani yake. Kama tungalikuwa na wakati... Labda tuchukue tu wakati na—na kusoma haya kwa dakika moja tu, Isaya 65, na hebu tusome tu kwa dakika chache hapa. Na jambo lenyewe liko hapa, naam, kwa ajili yetu. Sasa, kuanzia, Isaya 65:17.

*Na, tazama, mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya...*

<sup>61</sup> Sasa, Isaya, nabii, alikuwa mmoja wa manabii walioandika Biblia nzima katika unabii wake. Yeye anaanza na uumbaji; katikati ya Kitabu chake, kweye sura ya 40 hivi, anatokeea Yohana Mbatizaji, Agano Jipy; naye anaishia hapa, katika Kitabu chake, katika Ufunuo, katika Utawala wa Miaka Elfu. Kuna vitabu sitini na sita katika Biblia, na kuna sura sitini na sita katika Isaya. Yeye aliandika maelezo kamili.

<sup>62</sup> Sasa, tunaona, hapa sasa yeye anachukua sura ya 65, sura moja zaidi, naye anazungumza juu ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Hebu angalia jambo hilo, jinsi lilivyo nzuri.

*...tazama, mimi naumba mbingu mpya na... nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni. (Hilo ni “yatapita.”)*

*Lakini fu—furahini, mkashangilie daima, . . . hata kwa ajili ya hivi ambayo nimekwishaumba; maana, tazama, naumba Yerusalem uwe wa shangwe, na watu wake wawe furaha.*

*Nami nitaufurahia Yerusalem, nitawaonea shangwe watu wangu; sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, kwa kuwa . . . wala sauti ya kuomboleza.*

*Hatakuwapo tena mtoto wa siku chache, na . . . wala mzee ambaye hajatimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa maiaka mia atalaaniwa. Ndipo ninii. . . .*

*Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na watakula matunda yake.*

*Nao hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; (hiyo ni kusema, shamba lako, mwanao analirithi, ama baadhi ya warithi wako) . . . hawatapanda, akala mtu mwingine kule;) wao wanapanda mimea yao wenyewe na kubaki humo; wana Uzima wa Milele) . . . maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu, na ninii zangu nydingi . . . na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nydingi.*

*Hawatajitaabisha kwa kazi bure, wala hawatazaa kwa taabu; kwa sababu wao ni wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na watoto wao pamoja nao.*

<sup>63</sup> Sasa angalia, hapa ndipo nitakapofikia, baada ya kitambo kidogo.

*Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, Mimi nitasikia.*

*Mbwa-Mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja, na simba atakula majani kama ng'ombe; . . . mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka. Hawatadhuru ama kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema BWANA.*

<sup>64</sup> Ni ahadi ya namna gani, ya manabii hawa na wakuu wenye hekima nydingi, waalimu wa Biblia, huko nyuma kabisa katika zamani za kale, kuona Siku hii yenyе utukufu ikija!

<sup>65</sup> Kwa vifungu hivi, mtu anaweza kufikiria, ama kuongozwa, hasa, kuamini ya kwamba sayari yote, ya dunia hii, itaangamizwa, "Nafanya Mbingu Mpya na Dunia Mpya," mnaona, kwamba mbingu zitatoweka na nchi itatoweka, ziangamizwe kabisa. Lakini tukisoma kwa makini, na pamoja na msaada wa Roho Mtakatifu, tunawenza kuona Ukweli wa jambo hili; na hilo ndilo tunaloendea.

<sup>66</sup> Ni anga tu inayoizunguka, na dhambi iliyo juu ya dunia, ambayo itaangamizwa. Mnaona? Sasa, tunatambua ya kwamba *mbingu* zinamaanisha “anga za juu.” Mnaona?

<sup>67</sup> Kunatendeka nini? Wakati huo, ndipo michongoma hii, na magonjwa, na mauti, na siasa, na mwanamume mwenye dhambi, na mwanamke mwenye dhambi, na pepo wachafu, vyote vitaondolewa na kuangamizwa. Mnaona? Haina budi kutendeka namna hiyo, kwa maana twaenda kuisha papa hapa. Tutathibitisha jambo hilo kwa Biblia. Papa hapa ndipo tutakapoishi. Sasa angalia, michongoma, virusi, maradhi yote na kadhalika, vyote vitaondolewa kabisa. Yote haya, kuwepo kwake duniani sasa, taratibu za kujitengenezea, siasa, dhambi, kila namna ya pepo wachafu ambao wameuchafua ulimwengu, na *mbingu* zote juu yetu ndani hapa, zimejaa pepo wachafu. Sasa tutaingia kwenye kilindi na kwenda kirefu, katika hili, mnaona.

<sup>68</sup> Yote haya yapo katika *mbingu*, ama anga, na dunia iliyopo sasa. Dunia hii inashikilia vitu hivyo, lakini haikufanywa kwa kusudi hilo. Dhambi ndiyo ilisababisha iwe namna hiyo. Mnaona? Ilifanywa na Mungu, Muumba. Lakini yote . . .

<sup>69</sup> Na miili yetu yote, tunayoishi ndani yake sasa, iliwekwa katika dunia hapo Mungu alipoiumba, kwa maana wewe umetokana na mavumbi ya dunia. Yote iliwekwa nje hapa. Wakati Mungu Mwenyewe alipoiumba, wewe ulikuwa katika mawazo Yake. Na ndani Yake, yule Mkuu wa Milele, mlikuwemo na wazo, ambalo ni sifa Yake.

<sup>70</sup> Na sasa dhambi ilisababisha haya yote kutukia. Nayé Mungu, katika kizazi hiki, anakusanya zana Zake.

<sup>71</sup> Shetani yungalipo. Hiyo ndiyo sababu mambo haya yote hutukia. Yeye yungali hapa, na majeshi yake yote maovu yangali hapa. Angalia, hiyo ndiyo sababu dunia sasa ni chafu sana. Hiyo ndiyo sababu ya kuendelea kwa takataka na mambo ya kipuuzi; umwagikaji wa damu, vita, siasa, dhambi, uzinzi, kila namna ya uchafu unaendelea, ni kwa sababu kwamba Shetani ndiye mtawala wa dunia hii na anga hili.

Unasema, “Ati ang- . . . ?” Naam, bwana!

<sup>72</sup> *Mbingu* na dunia pia zimejaa pepo ambao wanaweza kutushtaki mbele za Mungu. Yesu Yupo kutuombea. Mnaona? Huku washtaki wakiendelea kutuelekezea kidole, “wao walifanya *hivi*, walifanya *hivi*, walifanya *hivi*,” bali ile Damu ingali inafunika. Yeye alikuja kumkomboa yule Mteule aliyetangulia kumwona. Hiyo ndiyo sababu ni chafu sana leo.

<sup>73</sup> Hapa, yule mtume, katika Petro wa Pili hapa, sura ya 2, na aya ya 5 na . . . na aya ya 5 na ya 6. Naam, nimeipata. Yeye anataja hatua tatu za dunia. Mnaona, yeye—yeye anachukua hatua zake tatu. Angalia jinsi anavyozileta.

<sup>74</sup> “Dunia ya kale iliyofanyizwa kutoka katika maji,” sasa, hiyo ilikuwa ni dunia iliyotangulia siku za gharika.

<sup>75</sup> Sasa, ile iliyopo sasa, dunia ya sasa tunayoishi sasa, inayoitwa “dunia.”

<sup>76</sup> “Dunia ile ya kale iliyofanyizwa kutoka katika maji,” Mwanzo 1:1. Sasa na “dunia” iliyopo sasa. Na halafu, tena, ananena juu ya nyingine, “dunia ijayo,” Nchi Mpya. Dunia tatu; hatua tatu za dunia.

<sup>77</sup> Basi angalia jinsi Mungu anavyoufanya dhahiri kwetu mpango Wake wa ukombozi. Loo! hili liliifurahisha nafsi yangu kweli nilipoliona, jinsi Yeye anavyofanya dhahiri kwetu hapa mpango Wake wa ukombozi. Sasa linganisha kile tunachokiona kwa macho yetu wenywewe. Kile Mungu alichofanya kuukomboa ulimwengu Wake, Yeye amefanya mpango ule ule kuwakomboa watu Wake, kwa kuwa Mungu asiyebadilika habadiliki hata katika mipango Yake wala kitu cho chote kile. Jambo lenye utukufu sana!

<sup>78</sup> Jinsi Yeye alivyotuongoza sisi Kwake, kwenye maskani ndani yetu, kwa hatua tatu za neema; kama tu alivyoiongoza dunia katika hatua tatu, aje duniani. Kama vile Mungu atavyokujua ulimwenguni baada ya huo kupitia katika hatua tatu mbalimbali za utakaso, hivyo ndivyo hasa Yeye anavyotujia katika hatua tatu za neema. Nilifundisha jambo hilo hapo mwanzo; sijabadilisha kamwe, tangu wakati huo. Ni Neno la Mungu.

<sup>79</sup> Huna budi kuweka tatu zako pamoja, saba zako, kumi na mbili zako. Nambari za Biblia hazina budi kufuatana kikamilifu la sivyo utavuruga picha yako kabisa. Kama huwezi kufahamu jambo hilo, endelea tu kuomba. Angalia, litaingia moja kwa moja, kweli kabisa. Mungu hukamilishwa katika tatu. Mnaona?

<sup>80</sup> Angalia, “dunia ile ya kale,” iliyotangulia ile gharika; “dunia” iliyopo sasa; na Ile ijayo.

<sup>81</sup> Sasa, hatua ya kwanza ambapo Yeye anatuleta... Mnaona, mpango Wake wa ukombozi ni sawa kabisa kwa kila kitu. Yeye hutumia taratibu ile ile. Yeye kamwe habadiliki. Alisema, katika Malaki 3, “Mimi ni Mungu, wala sibadiliki.” Jinsi Yeye anavyolifanya jambo hilo, basi, kama Yeye alimwokoa mtu wa kwanza aliyepata kumwokoa, kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia, Yeye hana budi kumwokoa huyo mwingine; na kila mtu anayemwokoa hana budi kuwa vivyo hivyo.

<sup>82</sup> Kama Yeye alimponya mtu katika wakati wo wote katika safari ya maisha; hata iwe ni katika siku za Yesu, mitume, manabii, wakati wo wote ule; wakati hali zile zile zinapotimizwa, Yeye hana budi kufanya jambo hilo tena. Hiyo ni kweli. Yeye habadiliki. Mwanadamu hubadilika, majira hubadilika, nyakati hubadilika, vipindi hubadilika, bali Mungu

hudumu yeye yule. Yeye ni mkamilifu. Ni tumaini la jinsi gani hilo linapaswa kuwapa watu walio wagonjwa.

<sup>83</sup> Kama Yeye alipata kumponya mtu, Yeye hana budi kufanya jambo hilo tena wakati masharti yayo hayo yanapotimizwa. Yeye akiwahi, akiwa aliwahi kumwokoa mtu, Yeye hana budi kufanya hivyo juu ya misingi ile ile aliyofanya jambo hilo mara ya kwanza. Kama alipata kumjaza mtu kwa Roho Mtakatifu, Yeye hana budi kufanya jambo hilo juu ya msingi ule ule aliofanya jambo hilo mara ya kwanza. Kama alipata kumfufua mtu katika wafu, Yeye hana budi kufanya jambo hilo mara ya pili, na kila wakati mwingine, juu ya kanuni ile ile.

<sup>84</sup> Yeye habadiliki. Loo! jinsi hilo linavyonipa tumaini! Ni kitu gani? Si katika nadharia ya kujitengenezea, jambo ambalo kundi la watu lilikutanika; bali Neno Lake lisilobadilika.

Unasema, “Hilo ni kweli?

<sup>85</sup> Yeye alisema, “Na neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe kweli.” “Kwa maana mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” “Maandiko yote yana pumzi ya Mungu, kwa hiyo ni mazuri na yanafaa kwa mafundisho.” Pia kumbukeni, ya kwamba, “Maandiko yote yatatimizwa,” kila sehemu yake.

<sup>86</sup> Angalia jinsi Mungu anavyolifanya jambo hilo dhahiri kwetu. Na kama hilo halikuwa thi-thibitisho kuu, ninii zuri... baraka kuu, za pendo kutoka kwa Mungu! Ninapoonaa jambo hili, na kuona kwamba tangu nilipokuwa mvulana, mara ya kwanza kabisa Kristo alipopata kunishughulikia, daima nilidumu kufundisha hatua hizo tatu za neema. Angalia kama jambo hilo si kweli sasa.

<sup>87</sup> Sasa, hatua ya kwanza ni “kumtubia Mungu.” Halafu kinachofuata jambo hilo, ni ubatizo wa maji, “ubatizo wa maji,” “Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo.” Mnaona, ubatizo wa maji unafuata, ukionyesha ya kwamba toba ilikuwa ya kweli. Ama, “kuondoa” dhambi zetu za zamani, huko hakuna uhusiano wo wote na dhambi za usoni. Kunaondoa tu. “Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo.” Kwa ajili gani? “Ondoleo.” Kuondolewa kwa dhambi ya zamani hakuna uhusiano wo wote na za usoni. Ni kwamba tu, dhambi zako zimekatiliwa mbali, yale uliyotenda.

<sup>88</sup> Huwezi kutubu kwa ajili ya yale aliyofanya Adamu. Wewe kamwe hukuyatenda; Adamu ndiye aliyeyatenda. Wewe husamehewa tu kwa yale uliyotenda. Ile tabia ya kale ingali pale.

<sup>89</sup> Hebu nichukue ubao huu kwa dakika moja tu. [Ndugu Branham anaelezee kwenye ubao—Mh.] Sasa, huu hapa moyo wa mwanadamu. Sasa, mimi si... Mimi niko mbali sana na kuwa mwanasanaa. HUU *hapa* moyo wa mwanadamu; na huu *hapa* moyo wa mwanadamu. Sasa, huu *hapa* una nyoka ndani yake,

hiyo ni dhambi, na hapa ana uhai wake. Huu *hapa* una hua ndani yake, ambaye ni Roho Mtakatifu, hapa ye ye ana Uzima. Vema, huyu *hapa*, ana kijicho, chuki, wivu; hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, ni jamaa huyu *hapa*. Vema, huyu *hapa* ana upendo, na furaha, na uvumilivu; na Hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, *hapa* chini.

<sup>90</sup> Sasa, unapoulizwa, ama unaposamehewa dhambi zako, umefanya hivi tu, umeondoa *hiyo*. Bali kitu kilichokufanya ufanya jambo hilo kingali mle. Hicho ni lile shina la kale la uovu; lingali pale. Angalia, ndipo unatubu na kubatizwa katika Jin la Yesu Kristo, ambapo anakusamehe dhambi zako. Angalia.

<sup>91</sup> Halafu, pili, unakuja utakaso, jambo ambalo hutayarisha nia yetu kwa ajili ya utakatifu, kuwazia mema. Kuondolewa mbali... *utakaso* ni neno la Kiyunani lenye maana mbili, ambalo linamaanisha “kilichosafishwa, na kuwekwa kando kwa ajili ya utumishi.”

<sup>92</sup> Halafu, baadaye, unakuja ubatizo wa Moto na Roho Mtakatifu, kusudi Mungu apate kuishi ndani yetu. Nao Moto wa Mungu unaisafisha mioyo yetu na dhambi, na kumweka Roho Mtakatifu ndani. Ndipo tunaishi Maisha yale yale *Huyo* aliyioishi, kwa maana Huyo yumo ndani yetu.

<sup>93</sup> Angalia, katika uzazi wa kawaida, wakati mwanamke anapomzaa mtoto mchanga. Maisha ya kawaida ni mfano wa maisha ya kiroho. Wakati mwanamke anapomzaa mtoto mchanga, mambo ya kawaida, jambo la kwanza linalotukia ni kuvunja chupa, halafu damu, ndipo roho (uhai). Unamnyakua huyo jamaa mdogo na kumpiga [Ndugu Branham anapiga kofi mara moja—Mh], na huyoo, anapiga makelele. Maji, damu, roho.

<sup>94</sup> Na sasa wakati mtoto mchanga anapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, ye ye huja kwa njia iyo hiyo: maji, Damu, Roho.

<sup>95</sup> Sasa angalia, utakaso, ile hatua ya tatu... hatua yake ya pili, husafisha nia; inaweza moyo, nia ya moyo, katika utaratibu wa utakatifu.

<sup>96</sup> Mtu anaweza kutubu dhambi na angali anafikiria juu ya... Vema, labda ye ye ni m—mzinifu, kila mwanamke anayeonekana mzinifu anayempata, lingalipo. Labda ye ye ni mlevi; kila anaposikia harufu ya pombe, ingali mle. Mnaona?

<sup>97</sup> Bali wakati anapotakaswa, jambo hilo hutakasa tamaa hiyo ikatoka ndani yake. Mnaona? Huondolea mbali ile hamu yake. Yeye angali anaweza kujaribiwa, bali Yeye huondolea mbali ile hamu yake. Hata hivyo, ye ye si sahihi bado.

<sup>98</sup> Halafu, anabatizwa kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Amesafishwa, akaunguzwa, akasafishwa; kisha akawekwa katika huduma ya Mungu.

Utakaso huwatenga tu kwa ajili ya utumishi.

<sup>99</sup> Basi tazameni jinsi jambo hilo huja hasa, jumbe zikija. Martin Luther, kuhesabiwa haki; John Wesley, utakaso; pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Zile jumbe, hiyo ndio sababu hapawezi kuwepo na nyakati zingine zake, mnaona. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Hatua tatu. Ubatizo husafisha moyo kwa Roho Mtakatifu.

<sup>100</sup> Jinsi lilivyo la kushangaza sasa, Yeye anapopitisha mahali tutakapoishi, katika utatatibu uo huo.

<sup>101</sup> Sasa, Yeye ameliita Kanisa kupitia kuhesabiwa haki, akiliita kupitia kwenye kutakaswa, kisha akalijaza na Roho Mtakatifu na Moto. Naye akalipitisha katika hatua fulani, ili kwamba Yeye Mwenyewe, Roho Mtakatifu Mweneyewe, Mwana wa Mungu, angweza kuishi katika moyo wa mwanadamu. Sasa, halina budi kupitia humo kabla Yeye hajaweza kuja ndani Yake.

<sup>102</sup> Angalia, Yeye aliufanya ulimwengu, ambamo Bibi-arusi ataishi, vile vile, mpango Wake ule ule wa—wa wokovu.

<sup>103</sup> Angalia ule ulimwengu uliotangulia ile gharika. Yeye, baada ya huo kutubu, kwa njia ya Bibi-arusi wa siku hiyo. Nuhu, Yeye aliupa ubatizo wa maji, akaufunika kwa maji. Halafu, kuhesabiwa haki, akionyesha ya kwamba Yeye yuko njiani kuuita ulimwengu huu ulioanguka, kutoka Edeni, urudie kule kurejezwa kwake upya tena.

<sup>104</sup> Ndipo Kristo akaja akamwaga Damu Yake juu yake, akausafisha na kuudai. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Mnaona, huo ndio ulimwengu tunamoishi ndani yake sasa.

<sup>105</sup> Unaona jinsi Shetani, hapa katika Maandiko, alivyojaribu kumfanya Yeye auharibu mpango wa Mungu apate kuupokea, aliumpa Yeye alipompeleka juu ya mlima, na kujaribu kuumpa Yeye bila ya kununuliwa kwa Damu?

<sup>106</sup> Hivi uliona jinsi Ibrahimu, wakati hao walipojaribu kumpa lile shamba, ye ye alilinunua kwa shekeli kadha za fedha, mbele ya watu, kama ishara, kama shahidi? “Na ijulikane leo ya kwamba nilipanunua mahali hapa pa kuzikia.” Mnaona, kupanunua! Naye Shetani alijaribu ku—kumpa Yeye ufalme amba ni mali yake sasa. Alijaribu kumpa Yeye kama zawadi, bali Yeye asingeupokea. Maana ni, mnaona, basi Shetani bado angaliweza kuudai. Lakini, ilibidi ununuliwe. Amina. Yeye alikuwa Neno katika utimilifu wake. Wao wasingeweza kumdanganya Yeye katika jambo hilo.

Halafu, sasa huo utapata ubatizo wa Moto.

<sup>107</sup> Mnaona, sasa huo umekwisha... Nini kilichotukia? Kristo alikuja akiliita Kanisa kwenye toba, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo; kulitakasa Kanisa; na pamoja na Moto wa Mungu ukishuka na kuchoma takataka zote, kisha anakuja na kuishi katika moyo wa binadamu.

<sup>108</sup> Sasa, dunia, itakavyokombolewa kwa ajili ya mту huyu aliyekombolewa, Yeye anatumia njia Yake ile ile. Yeye aliubatiza katika maji, baada ya siku zilizotangulia ile gharika. Akamwaga Damu Yake juu yake, kuitakasa na kuidai. Ni Yake.

Shetani alijaribu kusema, "Nitakupa hiyo Wewe."

<sup>109</sup> Yeye akasema, "La, bwana, Nitainunua." Na iwe ushahidi. Yeye aliiinuliwa, kama ishara, ya kwamba aliiinunua. Yeye aliiinunua.

<sup>110</sup> Bali sasa haina budi kupitia ubatizo wa Moto, Moto mtakatifu kutoka kwa Mungu, ambo unaisafisha dunia na mbingu zinazoizunguka. Ndipo, imenunuliwa kusudi waliokombolewa wapate kuishi juu yake, kuishi humo katika amani. Angalia, ubatizo wa Moto ni wa kuisafisha na dhambi, na magonjwa, na virusi, na wenye dhambi, na ibilisi na kundi lake lote. Yeye lazima atupwe, kwenye Ziwa la Moto. Moto Mtakatiu kutoka kwa Mungu, unashuka kutoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, na kuiunguza, angalia, kuifanya tayari kwa Mungu kuishi ndani yake. Kwa kuwa, Mungu, katika Ulimwengu Mpya ujao, ataishi duniani. Maana, mnasema, "Mungu, Yeye anaishi katika moyo wa mwanadamu." Lakini, Yeye na Bibi-arusi wanakuwa Mmoja, nao wanaenda Nyumbani kwao katika Ulimwengu Mpya. Na mpango ule ule wa ukombozi unatumwiwa kukombooa, pia, ulimwengu na watu wanaoishi ndani yake.

<sup>111</sup> Mnaona, moyo hauna budi kusafishwa namna hiyo. Kabla Mungu hajaweza kushuka katika utu wa Roho Mtakatifu, ambao ni Kristo akishuka na kukaa katika moyo wa mwanadamu, hauna budi kutubiwa kwanza. Hauna budi kubatizwa katika maji, katika Jina Lake, kuonyesha ni mali ya nani.

Halafu hauna budi kusafishwa kwa Damu ya Yesu.

<sup>112</sup> Halafu ule Moto mtakatifu pamoja na Roho Mtakatifu, kutoka kwa Mungu unashuka chini na kuunguza tamaa zote za dhambi, tabia yote ya ulimwengu. "Na, kwa hiyo, yeye anayetenda dhambi maksudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli..." Halafu, tena Biblia ilisema, "haiwezekani..." "Kwa maana, m—mtu aliyezaliwa na Mungu hawezi kutenda dhambi; hatendi dhambi." Hakuna njia kwake kufanya dhambi. Anawezaje kuwa mwenye dhambi, na aliye kombolewa, wakati ule ule? Ninawezaje kuwa katika duka la rehani, na nje ya duka la rehani, wakati ule ule? Mnaona? Loo! Yeye alitukomboa kwa Damu Yake; kwa Roho Wake Yeye alitusafisha; kisha anakuja kuishi ndani yetu, Kanisa. Si madhehebu, sasa; Kanisa!

<sup>113</sup> Angalia kwa makini sasa tunapochukua jambo hili, mahali tutakapo—tutakapoishi. Sasa, sasa, ile—ile toba ya siku zilizotangulia ile gharika, basi, zilisababisha ubatizo wa maji. Ndipo Kristo akaja na kumwaga Damu Yake juu yake, kuisafisha na kuidai. Ndipo yanakuja, baadaye, maangamizi ya dunia ilivyopo sasa.

<sup>114</sup> Dhambi zote zilizoko kwenye mbingu juu, “ye ye ni mtawala wa nguvu za hewani,” ye ye huzuia (kukinga) baraka kutoka kwa Mungu. Humo hutoka ndani radi za umeme na kuipiga dunia, na kila kitu, kutoka mbinguni, mvua nyingi za barafu, na tufani, tufa- . . . dhoruba na kila kitu, “vinatoka juu,” ambavyo ni Shetani, “mtawala wa nguvu za hewani.”

<sup>115</sup> Angalia, angalia jinsi Shetani alivyojaribu kuichukua, kama nilivyosema dakika chache zilizopita, kwa kuimpa Yesu bila kuinunua. Ndipo, Shetani angali ana madai juu yake, kwa sababu imetiwa alama, mnaona. Lakini Yesu anainunua kwa Damu Yake iliyomwagika na kuirudisha kwa mwenyewe halisi. Mnaona? Hivyo ndivyo alivyojutununa, kwa Damu Yake, Jinsi aliyolinunua Kanisa.

<sup>116</sup> Na sasa ubatizo wake wa Moto unaisafisha na vijidudu vyote vya maradhi, magojwa yote, maradhi yote, hata vitu vyote vya kiroho; ambapo kwetu sisi, pia, inafanyika namna ile ile; kuifanya tayari kwa Mungu kuishi ndani yake, katika wakati huu mkuu unaokuja, Nchi Mpya. Mnaona, Yeye huikomboa kwa njia ile ile anayowakomboa watu Wake. Yeye huifanya vile vile hasa, mpango Wake wa ukombozi. Kwa kuwa, Yeye ni Mungu asiyebadilika, daima ye ye yule katika mipango Yake.

<sup>117</sup> Jinsi nimewaambia, hapo awali, na kuwalishwa jambo hilo, na kwa nyakati zote, ya kwamba Mungu hawezi kubadilika; hulijulisha, kila njia, kwa njia ile ile.

<sup>118</sup> Yeye alitutangazia, ujumbe Wake wa kwanza, katika ulimwengu uliotangulia siku za ile gharika, kwa nabii Nuhu.

<sup>119</sup> Nilikuwa nikizungumza na ndugu mpenzi ambaye yupo anaketi pamoja nami sasa. Jana, ye ye alisema, “Ulisema jambo moja, Ndugu Branham, ambalo daima limenishtusha.”

Nikasema, “Ni jambo gani, ndugu?”

<sup>120</sup> Naye akasema, “Ulisema hivi,” na ni kweli, ““Wachache, jinsi kundi dogo litaokolewa katika siku za kule Kuja.” Nasi tukazungumza jinsi Yesu alivyojema, ‘Mlango ni mwembamba na njia imesonga, na ni wachache watakaoiona.’ Sasa angalia, Biblia ilisema, ‘Kama iliyokuwa katika siku za Nuhu ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kule Kuja.”

Nikasema, “Ndugu, wewe una ninii tu . . .”

Akasema, “Kumbuka, pana watu wanane tu pale.”

Nikasema, “Una nusu ya picha tu.”

<sup>121</sup> Hata hivyo, Nuhu alikuwa mfano wa waliosalia waliovushwa, si lile kundi lililobadilishwa. Henoko, mtu mmoja, alienda katika Unyakuo kabla ya gharika kuja, ikionyesha ya kwamba Kanisa haliingii kwenye ile dhiki wala kitu cho chote karibu nalo. Henoko alibadilishwa, mtu mmoja. Loo! kanisa huenda likawa watu wengi; bali Bibi-arusi atakuwa kundi

dogo sana litakalofanyiza yule Bibi-arusi. Sasa, huenda kanisa likawa watu wengi sana; lakini, Bibi-arusi, mnaona, linganisha wanane na mmoja. Pungufu mara nane, kuliko kanisa, ndio watakaokuwa Bibi-arusi.

<sup>122</sup> “Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi,” hao wanaojua vema zaidi, kufanya jambo hilo, nao wanaenda na kulifanya hata hivyo? Hao wanaofuata kanuni za madhehebu badala ya Neno, wao wataonekana wapi, ingawa wanaitwa Wakristo, wakilichukua Jina la Kristo?

<sup>123</sup> Sasa, kikamilifu, Nuhu alikuwa mfano wa wale watakovushwa. Kumbukeni, wakati Nuhu alipotoka, Hamu alikuwa pamoja naye. Dhambi ilikuwa ingaliko mle. Dhambi ilivuka moja kwa moja, kupitia safinani. Kutokuamini, mashaka yalivuka katika safina, yakabebwa juu ya hukumu. Lakini Henoko alienda juu zaidi ya ile safina, alienda katika Uwepo wa Mungu. Lakini Nuhu alivuka kisha akatoka, na kulikuwa bado kuna dhambi; mfano wa ule Utawala wa Miaka Elfu, wa hali ya ulimwengu.

<sup>124</sup> Ule Utawala wa Miaka Elfu sio mwisho wake. Kungali kutakuwako na wakati baada ya Utawala wa Miaka Elfu. Utawala wa Miaka Elfu ni kipindi cha wakati; lakini, si ile Nchi Mpya. La, hasha. Angalia, katika jambo hilo, tutalifikia baada ya kitambo kidogo.

<sup>125</sup> Mnaona, dunia, iliyokombolewa, inamrudia mwenyewe wa asili tena. Ilichukua... Yeye aliichukua kutoka kwa Shetani. Alivuta, akaitoa nchi kutoka kwa Shetani, kama vile tu alivyokutoa wewe kutoka kwa Shetani, kama vile Yeye alivyomtoa maskini yule mwanamke kisimani kutoka kwa Shetani. Hapo amesimama kuhani, akidhania yeye alikuwa pamoja na Mungu, naye hakuwa na kitu. Mnaona?

<sup>126</sup> Ningetaka kuwachorea jambo hilo kwa muda kidogo tu. Sasa, tunataka kulifanya hili dhahiri sana, kwa hiyo sasa angalieni kwa makini sasa fundisho hili. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao, kwa ajili ya aya chache zifuatazo.—Mh.]

<sup>127</sup> Sasa, hii hapa, huyu *hapa* ni Mungu. Mungu, ambaye ni wa Milele, bila... Hakuna mtu ila Yeye. Lakini, katika Mungu, Yeye alikuwa na sifa. Sasa, hii *hapa* inawakilisha Neno, Neno la Mungu, lilitofanyika mwili likakaa kwetu katika utu wa Yesu.

<sup>128</sup> Sasa huyu *hapa*, jamaa huyu hapa, tutamfanya namna *hii*. Sasa, *huyu* anaitwa mwanamke kisimani. *Huyu* ni kuhani, Farisayo. Na mahali unapoona *huu*, ubao wazi, inamaanisha neema na wokovu.

<sup>129</sup> Sasa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Zile hatua tatu. Ilikuwa ni sifa kwanza, iliyoukuwa ndani ya Mungu, ambapo alijiwazia

Mwenyewe kuwa mwanadamu; na hilo likamshusha Yeye chini apate kuwa Yesu; na sasa, kama utawahi kuwa mahali Pale, ulikuwa pamoja Naye wakati huo. Kwa kuwa, kuna namna moja tu ya Uzima wa Milele, huo ni Mungu; nawe ilikubidi kuwa sehemu ya Mungu hapo mwanzo, si kile tu ulichochagua hapa chini. Yeye alikuchagua. “Wote alionipa Baba Yangu wataniija Mimi.”

<sup>130</sup> Sasa mwangalie kuhani huyu hapa. Tunaona sehemu yake ya chini, *hana*, maisha yake ya nyuma, nyuma huku nyuma yake, kuchaguliwa kwake tangu zamani nyuma hapa, ni mwenye dhambi.

Hapa ni kuzimu, *hana* chini.

<sup>131</sup> Sasa, sehemu hii ndogo *hana* ndani, inayoonekana kama ubao, hiyo inawakilisha usafi wake. Yeye alikuwa kuhani. Alikuwa mtu mwenye heshima. Hiyo iliakilisha *hii*. Yeye alikuwa, pia, ilimbidi awe mtu mzuri, la sivyo asingeweza kuwa kuhani. Lakini unaona jinsi alivyopata jambo hilo, ilikuwa kisomo cha akili.

<sup>132</sup> Sasa, maskini mwanamke huyu, maisha yake ya kwanza, *hana* juu, yeye alikuwa ni malaya, alikuwa ametiwa unajisi kabisa. Lakini huko chini kabisa ndani yake, *hana*, kulikuweko na kufahamu kudogo tu. “Ninajua atakapokuja Masihi...” Mnaona? Mnaona, hiyo ilikuweko.

<sup>133</sup> Angalia, Yesu alipokuja na kulidhihirisha Neno, kwa sababu Neno liliyatambua mawazo yaliyokuwemo moyoni; kama Waebrania 4 isemavyo Hilo litafanya, 4:12, ya kwamba Yeye angefanya jambo hilo. “Neno lilitambua mawazo ya moyo,” Naye alikuja kama Mwana wa Adamu, yule Nabii. Nini kilitukia? Kuhani huyu, akiwa tu na kisomo cha akili, alisema, “Ni pepo,” kwa maana hivyo ndivyo madhehebu yake yalivyoliita. Ilifanya nini? Hakuwa na uwakilisho, kwa hiyo lilimtia giza.

<sup>134</sup> Lakini maskini mwanamke huyu hakuwa na kitu cha kuonyesha; yeye alikuwa mchafu na kinyaa alivyoweza kuwa. Lakini, angalia, kule chini kabisa ndani yeke, yeye ana uwakilisho, unaona. Na, basi, alikuwa akitazamia hili lifanyike mwili.

Na wakati aliposema, “Nenda kamwite mumeo uje naye hapa.”

Alisema, “Bwana, sina ye yote.”

<sup>135</sup> Kasema, “Umesema kweli, maana una watano, na yule uliye naye sasa si wako. Umekuwa na watano. Hiyo inakufanya uwe na sita.”

<sup>136</sup> Yeye akasema, “Bwana!” (Si, “Wewe ni,” si, “Beelizebuli.”) “Naona ya kuwa U Nabii. Sasa, tunajua Masihi, aitwaye Kristo, atakuja. Naye atakapokuja, Yeye atafanya jambo hili.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

<sup>137</sup> Hakuna tashwishi tena. Haikukubidi kueleza jambo hilo. Aliliona. Akaliamini. Huyoo akaondoka! Kwa nini? Lilimfanyia nini? Lilimkombo.

<sup>138</sup> Sasa angalia, Yeye alikuja kuwa Mkombozi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] *Kukomboa* kuna maana gani? “Kurudisha.” Kwa nini yeye hakumpata kuhani? Yeye hakuwako kule juu. Mnaona? Mnaona, yeye hakuwa na uwakilishi.

<sup>139</sup> Yeye alikuja kukomboa kile kilichokuwa kimeanguka. Katika kule kuanguka, *hili* lilichafuliwa, kwa upande wa msichana yule; lakini Mungu alikuwa naye katika mawazo Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Nayе alikuja kumsafisha. Mnaona? Kwa hiyo Mungu... Yeye mwanamke alikuwa na Uzima wa Milele. Mnaona?

<sup>140</sup> Ambapo, yule kuhani, lilifanya nini kwake? Lilimrudisha moja kwa moja mpaka kweneye kikomo cha safari yake. Hakuwa na kitu, kwanza, ila kisomo cha akili.

<sup>141</sup> Sasa sikiliza, ewe rafiki, kama kitu pekee ulicho nacho ni kisomo cha akili tu, hebu pata kitu tofauti na hicho. Wala hutaweza kamwe kulipata Hilo isipokuwa una uwakilisho. Hiyo ndiyo sababu ninaamini mmetoka mashariki na magharibi, kaskazini na kusini; Neno, liishilo, likidhihirishwa.

<sup>142</sup> Angalia sasa, jinsi anavyoifanya Njia Yake ijulikane kwa manabii Wake, hapo mwanzo. Yeye hajaibadilisha wakati wo wote.

<sup>143</sup> [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]... wokovu. Yeye alimhesabia haki mtu; akamtakasa; akatuma na Roho Mtakatifu na Moto, na kuiteketeza dhambi ndani yake, kisha akaishi ndani yake, Yeye Mwenyewe.

<sup>144</sup> Yeye huifanya dunia, ambayo Yeye ataitumia katika mpango wa ukombozi, namna ile ile. Ilitubu na kubatizwa majini, katika... na Nuhu. Yesu alikuja akaitakasa, kwa kuinyunyizia Damu Yake, na kuidai. Na katika ile Nchi Mpya ijayo, itapata ubatizo wa Moto mtakatifu, kuisafisha na kila pepo, kila kirusi, kila ugonjwa, kila kitu kilichomo, na kuifanya mpya. “Niliona Mbingu Mpya na Nchi Mpya.”

<sup>145</sup> Unakuwa mtu mpya. Amina! Si yule wa kale tu aliyetiwa viraka, kwa kujiunga na kanisa ama kujaribu kugeuza ukurasa mpya, bali wewe ni kitu kipyaa kabisa. Mungu humchukua mtu yule wa kale na kumteketeza kabisa, kwa Roho Mtakatifu na Moto, kisha Yeye Mwenyewe anakuja, anatuma uwakilisho wako. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watanijia Mimi.” Mwaliona? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Mpango ule ule; njia ile ile.

<sup>146</sup> Shetani alikuwa . . . ataondolewa duniani, kama tu vile hasa Shetani alivyoondolewa kwako. Shetani hawezi kusumbua; ama, anaweza kukujaribu, bali hawezi kumpata Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Kwa maana, Mungu, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, alitangulia kumwona, na akamtuma Yesu kumkomboa, nayo ile Damu inanena kwa niaba yake. Anawezaje kufanya dhambi wakati, hata, haiwezi kuonekana na Mungu? Yeye hata haninii . . . Kitu pekee anachosikia ni sauti yako. Yeye huona uwakilisho wako. Amina! Hijo ni kweli. Mnaona?

<sup>147</sup> Kwa njia ile ile, kwa maana dunia ni moja ya sifa Zake kama tu vile wewe ulivyo moja ya sifa Zake. Dunia inakuwa moja ya sifa Zake, kwa sababu ilikuwa ni mawazo ya Mungu, hapo mwanzo. Kuwa na dunia, kuwa kwenye Kiti cha Enzi, kuwa Mfalme, kuwa Mkombozi, kuwa Mponya, hizo ndizo sifa Zake.

<sup>148</sup> Kama tu sifa zako. Siwezi kusema “m—m—mhimili” isipokuwa ninafikiria juu ya mhimili. Siwezi kusema “mtu” isipokuwa ninafikiria juu ya mtu. Na ninapofikiria juu ya mtu, halafu niseme “mtu,” kule kuwazia ndiko sifa yangu na kule kutamka ndiko neno. Mnaona?

<sup>149</sup> Kama vile Isaya, angewezae kusema, ya kwamba, “Bikira atachukua mimba”? Wazo ni nini?

<sup>150</sup> Sasa, wengine wenu mnashangaa jinsi hizo, huo utambuzi, unavyokuja. Nitawaambieni. Mnaona, ni neno ninalosema. Wala si kuwazia kwangu, kwa maana mimi sijui. Sijui juu ya kuwazia kwa jambo hilo. Ninawezaje kukwambia wewe ni nani na unatoka wapi, na huku sikuju wewe? Ninawezaje kukwambia uliyotenda miaka kumi iliyopita, na huku sijakuona maishani mwangu? Ninawezaje kukwambia mahali utakapofanya na yale utakayofanya miaka kumi tangu sasa? Ninajuaje mambo ya usoni? Lakini ni wazo la Mtu mwiningine.

<sup>151</sup> “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo. Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo.” Mnaona, ndipo si mawazo yenu. Ni mawazo Yake, kupitia kwenu. Nanyi hamneni maneno yenu wenyewe; mnanena Maneno Yake.

<sup>152</sup> Hivyo ndivyo ambayo, mara nyingi ndugu wanachanganyikiwa, katika kufasiri lugha, na kadhalika. Mnaona, wao wanasema mambo ambayo si kweli, hawatambui ya kwamba huyo ni Shetani. Mnasema, “Katika bustani ya Mungu?” Ngojeni tu mpaka tutakapomaliza, mwone kama sivyo, au la. Magugu na ngano vinakua kwenye shamba lile lile. Vyote vinaishi kwa jua lile lile na mvua ile ile. Mnaona?

<sup>153</sup> “Lakini kama kuna mmoja kati yenu aliye nabii, Mimi Bwana nitasema naye. Na iwapo analosema linatukia, basi huyo ni Mimi, mnaona, maana yeye hatamki yake. Yeye anatamka mawazo Yangu, sifa Zangu za mambo ambayo hayana budi kuja, nami nitatumia mdomo wake kuyatamka kwake. Na baada ya

ye ye kuyasema, hayana budi kutimia. Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatashindwa kamwe.”

<sup>154</sup> Isaya alisema, “Bikira atachukua mimba.” Hiyo imekwisha. Yeye atachukua mimba. Yale aliyosema Mungu, Yeye huyatenda.

<sup>155</sup> Loo, kufanya yajulikane, kwa manabii Wake, madhihirisho Yake yote, kwa maana ni sifa za mawazo Yake yaliyotamkwa.

<sup>156</sup> Sasa, hilo lilikuwa hapa, katika maskini mwanamke *huyu*. Yeye alikuwa mmoja wa sifa Zake. Mnaona?

<sup>157</sup> Na pale alikuweko yule kasisi, akiiwakilisha ile Nuru. Yeye alijifunza hayo katika Biblia. Alikuwa ameelimishwa kwamba Mungu alikuwa Mungu. Alikuwa amejifunza kwamba utakatifu ulikuwa ni sawa. Alikuwa amejifunza kwamba kulikuweko na torati ya Mungu. Alikuwa amejifunza hayo kwa sababu ilikuwa ya mawazo ya kiakili. Naye alikuwa amezaliwa katika ukoo mzuri; alikuwa Mlawi. Lakini alilija tu kwa mawazo ya kiakili. Basi wakati ile Nuru ya wakati huo . . . Mnaona, yeye alijifunza jambo hilo kwa yale yaliyokuwa yametukia, si yale yaliyokuwa yanatukia wakati huo; yale yaliyokuwa *yametukia!* Basi wakati alipopata yale yaliyokuwa yakinukia wakati huo, madhehebu yake hayakusema kitu juu Yake, kwa hiyo yeye hakuwa na uwakilisho Wake.

<sup>158</sup> Lakini hapa alikuwako Mkombozi duniani wakati huo, kukomboa sifa hizo za Mungu, naye akapokea hilo. Yeye hakutilia swali jambo hilo. Alisema, “Masihi atakapokuja, Yeye atafanya jambo hili,” na hilo lilitosha. Naye akaona likifanywa, kwa hiyo . . . Yeye alisema, “Mimi ndimi Mashihii,” kwa hiyo hilo likatosha. Hakuna swali tena. Alienda tu, akimwambia kila mtu, “Njoni, mtazame Mtu niliywona.”

<sup>159</sup> Hatua hizi hutufanya sisi kuwa wasafi, hekalu kwa ajili ya ya makao Yake: kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto. Hizo hufanya utakaso wa hekalu (letu) hili.

<sup>160</sup> Kwa hiyo, kama vile umbo la dunia ya kale halikuangamizwa, kwa maji wakati iliposafishwa; umbo lile la sayari, umbo la kale, ninii . . . uchafu wote, vitu vyote ambavyo Mungu aliweka duniani, havikuangamizwa wakati ulimwengu wa kwanza ulipoangamizwa. Na Biblia ilisema, “uliangamizwa,” bali umbo lenyewe halikuangamizwa. Iliangamiza tu dhambi na wenye dhambi waliokuwa juu yake. Umbo lilibakia.

<sup>161</sup> Lakini, mnaona, kama vile kuhesabiwa haki, kama vile ninyi Wabatisti na Wamethodisti mnavyotaka kuliwazia jambo hilo, kuhesabiwa haki tu, kuamini na kubatizwa, huko hakutoshi. Utatangatanga uyarudie moja kwa moja mambo ya ulimwengu, na kukata nywele zako na kuvala kaptura, na cho chote kile. Mnaona, hakuna kilichotukia bado. Uliangalia tu nyuma ukaona ulikoseea.

<sup>162</sup> Kuhesabiwa haki kuliufanyia nini ulimwengu? Hakukuufanyia kitu; ulianza moja kwa moja tena, ukiwa na dhambi nyingi tu kama ulivyopata kuwa nazo. Hivyo ndivyo mtu anavyofanya, na huo ndio umbali tu anaoenda.

<sup>163</sup> Hivyo ndivyo yule mwinjilisti mashuhuri, Billy Graham, anavyopaswa kuona. Alisema, “Ninaenda na kuwapata waongofu elfu thelathini, ninarudi mwaka mmoja baadaye na hakuna hata thelathini.” Huo ndio umbali tu walioenda. Mnaona? Na, hakika, wao wanatubu. Ninaamini wao hutubu; wengi sana wao, ama baadhi yao, angalau. Lakini hilo silo linalohitajika. Jambo hilo linathibitika hapa.

<sup>164</sup> Sasa, kwa hiyo umbo la dunia ya kale halikuangamizwa kwa maji. Ulimwengu ule ulioshwa tu. Huo ulipata ubatizo wake. Ulibatizwa.

<sup>165</sup> Kwa hiyo umbo litabakia, ingawa itaunguzwa kwa Moto. Huo hauiangamizi dunia, mnaona, huangamiza tu dhambi iliyomo.

<sup>166</sup> Angalia hapa, baadhi yenu enyi wanafunzi wa Biblia, na zaidi sana Daktari Dale anayeniangalia. Angalia katika Petro, katika sura ya 2 ya Petro hapa, sura ya 3, hasa, yeye anatumia neno “ulimwengu,” kama Neno la Kiyunani *kosmos*, ambalo maana yake ni, “utaratibu wa ulimwengu.” “Dunia itatoweka, viumbe vya asili vitateketea na kuyeyushwa kwa joto kali mno.” Mnaona? Haimaanishi ya kwamba dunia, sayari, itapita. Lakini ulimwengu, *kosmos*, siasa, wenze dhambi, taratibu, dhambi, magonjwa, virusi, kila kitu kilicho kibaya, kitapita. Kila kitu ambacho wakati mmoja . . .

<sup>167</sup> Mungu siku moja alizitetemesha mbingu, lakini kwakati huu Yeye alisema Yeye ataitetemesha nchi, mbingu na nchi . . . “Yeye aliitetemesha nchi,” hasa, “na kisha wakati huu Yeye atazitetemesha mbingu.” Mnaona? “Kwa kuwa tunapokea Ufalme usioweza kutetemeshwa.” Ni Ufalme wa Milele. Angalia jinsi anavyoliendea jambo hilo.

<sup>168</sup> Angalia hapa, Petro alisema, “Na itayeyushwa kwa joto kali mno, na kazi zilizomo ndani yake zitateketea,” si sayari. “Kazi zilizomo ndani yake,” kazi za mwanadamu, wanasiasa wao wote na kazi zao, na madhehebu yao yote na kazi zao za kujitengenezea, vyote vitaangamizwa pamoja nayo itakapoteketea.

<sup>169</sup> “Na—na mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu.” Ulichunguza hapa? “Mbingu zitapita kwa mshindo mkuu.” Sikilizeni! Dunia nzima itawaka moto, na hewa zilizomo duniani zitashika moto na kuilipua. Hiyo ni kweli kabisa. Nena . . . Biblia ilisema hapa, Petro alisema, “Na mbingu zitapita, pamoja na dunia, kwa mshindo mkuu.” Mlipuko wa namna hiyo utaisukasuka, loo, jamani! maana hauna budi kuangamiza kila ugonjwa, kila mchongoma, kila mwiba. Kila kitu kinachopaswa

kuteketezwa, ule Moto utakiteketeza. Na, kumbukeni, si kwa jumla moto wa kawaida tu, ni Moto mtakatifu pia, mnaona, utakaomwondolea mbali Shetani na wote walio wake, pepo wote, "Mbingu na nchi pia," amina, "zitapita," zikiua vijidudu vyote, wadudu wote, uhai wote wa kawaida ulio juu yake na unaozunguka, hata H20 (maji) yatalipuka. Wazia jambo hilo. Nena kuhusu mshindo!

<sup>170</sup> Unafikiri mshindo ule mdogo nje huku Tucson ulikuwa kitu, wakati Yeye alipozifungua zile Muhuri Sita, ulioitikisa nchi karibu na hapo, na kusababisha maneno. Ngojea mpaka dunia hii itakapopokea ubatizo wake!

<sup>171</sup> Unaajua, mtu anapoupoapea ubatizo wa Moto, kuna makelele mengi sana hapo. Wao wanafikiri hiyo ni aibu, kuwasikia watu wakipiga makelele na kupaza sauti namna hiyo. Ngojeni tu mpaka dunia hii itakapopata ubatizo wake!

<sup>172</sup> Naam, itaeleza...itayalipua, H20, maji, kwa kuwa Biblia ilisema hapa katika Ufunuo 21, "wala hapana bahari tena," italipuliwa. Jambo hili litabadilisha uso wote wa dunia nzima. Itapasuka na kuvunjika vipande-vipande. Sehemu yote ya nje, uso wa dunia, na kuingia futi mamia kadha ndani yake, itafunuliwa tu kabisa. Anga, hewa zilizomo duniani sasa, mahali ambapo wanapata makombora haya yasiyowenza kupenya ndani yake, eneo kubwa sana kule juu, huko juu kabisa kwenye namna fulani ya eneo ambako kuna kila namna ya hewa, wao wanasesma; na hizo zitalipuka. Hasira takatifu ya Mungu itakuja juu yake, mnaona, na itaisafisha, itaubadilisha uso wote.

<sup>173</sup> Sasa, wengi wenu ninyi mnaotaka kuandika neno hili, neno la Kiyunami, "kupita." Linatokana na neno... Ilinibidi kulichunguza. Nikafikiria, "dunia hii itapitaje, na hata hivyo tutaishi humo?" Lakini kama utaangalia, baadhi yenu ninyi watu mnaotaka kuliandika, nitawaendelezea harufi zake. Nisingeweza kulitamka, p-a-r-e-r-e-c-h-o-m-i-a. Sijui jinsi ya kulitamka.

<sup>174</sup> Sasa, kwa njia hiyo, kama nilivyosema, ninapopata... Uvuvio wa kitu fulani ukinigusa, basi mimi hurudi kulichunguza neno hilo. Sasa, hapa, siwezi kuendeleza herufi za hilo neno, ama siwezi—siwezi kulitamka. Lakini, katika jambo hilo, Bwana angali ananipa njia. Ninaondoka ninaenda na kuangalia maana ya neno hilo, kisha ninalipata. Mnaona? Ndipo nimelipata, tena. Mnaona?

<sup>175</sup> Mbingu na nchi *zitapita*, sasa, neno hili maana yake ni, "kupita kutoka hali moja kuingia nyngine." Halimaanishi "kuangamizwa," kama vile neno la Kiingereza lingemaanisha, *kupita*, ni kuangamizwa. Lakini neno hili la Kiebrania, ama Kiyunani hapa, halimaanishi *kupita*; linamaanisha, "kupita kutoka kwenye kitu kimoja kuingia kingine." Angalia, lakini, "kupita kutoka kwenye hali moja," inasema, "kuingia nyngine."

<sup>176</sup> Sasa angalia, Paulo alilitumia, kama ukitaka kulisoma sasa. Liandike, unaweza kulisoma baadaye. Katika Tito 3:5, Paulo anatumia neno lili hili, linamaanisha kuzaliwa upya kwa mtu, ya kwamba mtu ametoka kutoka mwenye dhambi akawa mtakatifu, hajaangamizwa kabisa. Mtu anapobadilishwa, ye ye haangamizwi, bali ye ye ni mtu aliyebadilika. Ye ye amebadilishwa kutoka alivyokuwa akawa alivyo, si kuangamizwa.

<sup>177</sup> Yesu alitumia Neno lile lile katika Mathayo 19:28; sasa, si 28:19. Sasa, 19:28, Yeye aliwaambia, “Mtaketi pamoja Nami katika Ufalme wa Baba Yangu, mmezaliwa upya,” mnaona, “mmebadilishwa,” mtakapobadilishwa. Alitumia neno lile lile.

<sup>178</sup> Tena alitumia neno lile lile aliposema, kwa yule mwana-punda, akasema, “Mfungueni mwana-punda mkamwache aende zake.”

<sup>179</sup> Alisema jambo lile lile katika kufufuliwa kwa Lazaro, “Mfungueni! Mbadilisheni! Amekuwa amfungwa; mwache aende zake!”

<sup>180</sup> Inamaanisha nini? Dunia itafunguliwa kutoka katika mikono ya Shetani. Itafunguliwa. Itafunguliwa kutoka kwenye siasa, itafunguliwa kutoka kwenye taratibu za madhehebu ya dini; ikatumie kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, utakaoanzishwa hapa duniani. Lakini mradi tu imo mikononi mwa Shetani, siasa... Shetani ndiye mtawala wa dunia hii, anaimiliki; ilikuwa ni mali yeke, lakini sasa Kristo ameikomboa.

<sup>181</sup> Wakati mmoja nilikuwa mali yake, lakini si sasa. Wakati mmoja, mwanamke yule mdogo alikuwa mali yake, lakini si sasa. Mnaona, Yeye alikuja kuifungua. Yeye alifungua mikono ya dhambi, ya Shetani, kwenye uhai wangu, kwenye uhai wako, na sasa sisi si wake.

<sup>182</sup> Hivi mara nyingi mmenisikia nikisema, katika maombi, “ondoa mikono yako kwenye mali ya Mungu”? Mnaona? Amina! Uwe na imani kudai yaliyo yako. Hizo ni haki zako. “Ondoa mikono yako kwa mwanamke huyo!” “Ondoa mikono yako kwa mwanamume huyo!” Mnaona, imani itafanya jambo hilo. Loo, jamani! Si kuiangamiza, lakini, ni tu, “Ondoa mikono yako kwake,” kuifungua, kuiachilia, kuitoa. Inabadilika.

<sup>183</sup> Dunia itabrudilika. Siasa zitabrudilika. Dini zitabrudilika. Madhehebu yatapita. Siasa zitapita. Ufalme wa Mungu utadumishwa.

<sup>184</sup> Tunasoma katika Yohana, tunasoma Yohana katika Ufunuo 6:14, mnaona, “ikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa.” Biblia ilisema ninii... ya kwamba itaninii... Yohana alisema, “Niliona mbingu na nchi zikiondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa. Yohana, Ufunuo 6:14.

<sup>185</sup> Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita," ama, kwa maneno mengine, "Mbingu na nchi zitabadilishwa." Mnaona, alitumia neo lile lile pale pale tena.

<sup>186</sup> La, si kuangamizwa. Kwa kuwa, baadaye, katika Ufunuo 21:2 hadi 24, aliona Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, ukikaa juu ya dunia hii. Haimaanishi itaangamizwa. Zile taratibu zitabadilishwa.

<sup>187</sup> Daneili aliona jambo lile lile. Mwamba uliochongwa bila kazi ya mikono uliipiga dunia; na hiyo sanamu yote ya hizo taratibu ikavunjiliwa mbali ikawa kama makapi ya viwanja vyta kupepetea wakati wa hari, na upopo ukavipeperusha. Nao ule Mwamba, Wenyewe, ukakua ukawa Mlima mkubwa ulioijaza nchi. Angalia Mlima huo sasa, katika muda kidogo. Mlima huo uliifunika nchi.

<sup>188</sup> Pia, tunaona hapa, hapa, pia, katika Ufunuo pale, ilisema, "Wafalme wa Nchi Mpya wataleta heshima zao na utukufu wao ndani yake." Dunia, mnakaa . . . Yerusalemu Mpya inakaa juu ya dunia hii. Mnaona, ilibadilika tu.

<sup>189</sup> Wewe ni mtu yule yule, katika kimo, uliyekuwa wakati Mungu alipokuita, mwanamke yule yule. Lakini, unaona, jambo ni kwamba, ilikuwa ni kuzaliwa upya. Maisha ya zamani yalipita. Tamaa ya zamani imepita. Wakati, ulipenda kunywa pombe, na kulaani, na kugombana, na kuzozana, na kuzurura, na uzinzi, kitu hicho kilikufa tu. Unaona? Lakini sasa wewe umezoea . . . Wakati huo wewe ulikuwa chombo cha Shetani; sasa umekombolewa.

<sup>190</sup> Na hivyo ndivyo dunia itakavyokuwa, jinsi ile ile, inakombolewa, Mbingu Mpya na Nchi Mpya.

<sup>191</sup> Ni kama wewe tu, "Wewe ni kiumbe kipyta." Nalo neno la Kiyunani pale, mtu ye yote anajua, lilisema, "Wewe ni kiumbe kipyta." Amina! Kiumbe kipyta katika hekalu lile lile la kale. Haleluya. Angalia jambo linalotukia hapa sasa. Tukufu! Vema.

<sup>192</sup> Sasa tunaona ya kwamba dunia hii itashikilia wafalme wa nchi.

<sup>193</sup> Na, tena, katika Mathayo 5:5, Yesu alisema, Wenyewe upole watairithi nchi." Si kuninihii tu, kuwa na dunia nyingine. Itakuwa ni dunia ile ile. Ninajaribu ku—kuwfakishia mpango wa ukombozi, kabla, kama sitawafikishia kitu kingine, mnaona. Ubatizo wa Moto, juu yake, ni wa kuisafisha tu na kuifanya mahali panapofaa kwa watu Wake wapole kuishi mle. Mnaona? Loo!

<sup>194</sup> Kama vile alivyotufanya sisi, uumbaji Wake, kuishi mle. Kabla ya Yeye kuweza kuja ndani yake, ilimbidi kutupa ubatizo wa Moto; ndipo Roho Mtakatifu akaingia na kuishi, ubatizo wa Moto. Halafu, unapopata ubatizo huo wa Moto, ndipo Roho Mtakatifu anaweza kuingia. Kitu gani? Anapoingia, Yeye

anachoma kila kitu kilicho kinyume cha Neno, kabisa ndani yako. Mnaona? Hataamini kitu kingine ila Neno, kwa maana Yeye ni Neno. Mnaona? Mnaona?

<sup>195</sup> Sasa, hilo ndilo tulilokuwa tunazungumzia hivi majuzi, thibitisho la Roho Mtakatifu. Mnaona? Thibitisho la Roho Mtakatifu ni wakati unapoweza kulipokea Neno; si taratibu fulani, bali kupata kuelewa vizuri. Unajua je ya kwamba Neno ni wazi, unalifahamu Hilo? Liangalie likijithibitisha Lenyewe.

<sup>196</sup> “Vema,” mnasema, “Ninaona *hili* likifanya kitu hiki, na *kile*.” Loo! naam, magugu yanaishi kwa njia ile ile. Mnaona?

<sup>197</sup> Bali haina budi kuwa ni Neno lote. Kuwa Bibi-arusi, huna budi kuwa sehemu Yake. Yeye ni Neno. Mnaona? Na ni sehemu gani ya Yeye? Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii wakati Yeye amwitapo Bibi-arusi Wake. Iweni sehemu ya hilo. Mnalipata? Sasa, msi-msiachilie hilo sasa. Angalieni.

Naye anapafanya mahali panapofaa pa kuishi Milele.

<sup>198</sup> Angalia, huu bado haujatajwa kuninii... Huu Utawala wa Miaka Elfu, ile miaka elfu moja, si Nchi Mpya. Mnaona, Utawala wa Miaka Elfu ni enzi tofauti. Huo ndio tutakaoingia, Utawala wa Miaka Elfu, bali huo si Nchi Mpya na Mbingu Mpya. La, la. Hapo ni mahali tu pa kupumzikia, mnaona, muda wa kupumzika, si Mbingu Mpya na Nchi Mpya hata kidogo; kwa kuwa, mnaona, katika ule Utwala wa Miaka Elfu tuna vitu ambavyo visingeingia katika Hizo. Ni mfano wa ile siku ya saba ya kale, kutoka Edeni; siku ya saba, baada ya Yeye kuufanya ulimwengu. Ile siku ya saba, Yeye alipumzika katika Edeni, na ule Utawala wa Miaka Elfu.

<sup>199</sup> Mnaona, dunia sasa ina umri wa karibu miaka elfu sita. Mnaona? Na kila maiaka elfu mbili umepata ma—maangamizi. Mnaona?

<sup>200</sup> Miaka elfu mbili ya kwanza, gharika ilikuja, Nayé akaubatiza (kwa kitu gani?) maji.

<sup>201</sup> Miaka elfu mbili iliyofuata, Yesu alikuja kuutakasa na kuudai, akadondosha Damu Yake juu yake, akauita Wake. Vema.

<sup>202</sup> “Nitakuja tena,” a-ha, sasa kama Mfalme pamoja na Malkia Wake, na miaka elfu mbili ya pili (Yeye anafanya nini?) Yeye anakuja na kutoa muda Wake wa mapumziko.

<sup>203</sup> Kisha anauteketeza, na kuudai kuwa ni Wake; Yeye anawarudisha walio Wake na kuwaweka humo.

<sup>204</sup> Basi angalia, si ulimwengu mkamilifu, Utawala huu wa Miaka Elfu, ni mfano wa siku ya saba. Halafu kunakuja ile Hukumu ya Kiti cha Enzi. Mnaona, tungali tuna hukumu. Tungali tuko katika wakati, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu. Ni siku moja, miaka elfu moja. Ni kipindi cha wakati. Siyo, msichanganye jambo hilo na Nchi Mpya, sasa, maana siyo.

<sup>205</sup> Huenda mkaniambia jambo hili. Sasa nahisi huenda mtu fulani akaniambia jambo hili, ya kwamba, "Sasa, Ndugu Branham, utafanya nini sasa? Umeishiwa na saba zako kamilifu. Unaelekea wapi, utafanya nini sasa? Sasa, wewe ni mwana-majira." Ambapo, ndivyo nilivyo. Ninaamini ya kwamba ndivyo Mungu alivyo, pia. Tazama, angalia. "Umeishiwa na mifano yako ya majira. Kwa kuwa, kama utaweka kitu fulani baada ya siku hiyo ya saba, utaipataje? Unaelekea wapi sasa?"

<sup>206</sup> Vema, nitawaelekeza mwangalie kitu fulani, mnaona. Mnaona? La, sijaninii, sijaishiwa na majira, bado. Nina Andiko lingine hapa. Na, kumbukeni, yote hayana budi kutimizwa, kila sehemu Yake. Mnaona?

<sup>207</sup> Sasa unasema, "Ndugu Branham, unajaribu kuweka kitu fulani kule mbali sana baada ya siku hiyo ya saba, sabato hiyo ya siku ya saba."

<sup>208</sup> Kama vile Mungu alivyoifanya nchi na kufanya kazi siku sita, kisha akapumzika kwenye siku ya saba, ilikuwa tu ni mfano wa wakati, wakati. Lakini ndiyo kwanza niseme tu hapa, tunakuwa wa Milele.

<sup>209</sup> "Kwa hiyo mfano wako uko wapi sasa? Ulisema wewe ni mwana-mifano. Kwa hiyo, wewe, wewe umeishiwa na mifano sasa." La, sijaishiwa. Hebu tuone tu kama tumeishiwa.

<sup>210</sup> Hebu turejee kwenye Mambo ya Walawi, nyuma kwenye sura ya 23 ya Mambo ya Walawi. Sasa nawatakeni mwone katika Mambo ya Walawi, mahali tulipokuwa Jumapili iliyopita, ama ninii iliyopita... Hili ndilo linalomipa hilo wazo, papa hapa. Sura ya 23 ya Mambo ya Walawi, na aya ya 26.

<sup>211</sup> Sasa kumbukeni, kuna siku saba za sikukuu. Sikukuu ya baragumu, sikukuu ya—ya vibanda, sikukuu ya kutikiswa kwa miganda, ninii... Zote hizi, kuna siku saba kuu za sikukuu, hizo zilikuwa tu ni mfano wa Nyakati Saba za Kanisa. Nanyi mnakumbuka kulikuwa na sabato ngapi kati ya moja na nyininge? Mnaona, sabato saba kati ya Pentekoste na zile baragumu, ambazo zilikuwa Nyakati Saba za Kanisa. Na kulikuwako na siku saba za sikukuu, ambazo zinawakilisha zile Nyakati Saba za Kanisa. Endelea kuhesabu namba zako.

<sup>212</sup> Mnasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, umeishiwa. Una saba yako."

<sup>213</sup> Vema, hebu tuchukue ile sikukuu ya mwisho, ambayo ni sikukuu ya vibanda. Sasa angalieni hapa katika aya ya 36.

*Ninyi mtamsongezea BWANA sadaka kwa moto siku saba; siku nane—siku ya nane kutakuwa na kusanyiko takatifu (kuna wakati mwингine mtakatifu unaokuja) ...kusanyiko takatifu kwenu; nanyi mtamsongezea BWANA sadaka kwa moto; na ni*

*mkutano wa makini huu; msifanye kazi yo yote ya utumishi.*

<sup>214</sup> Sasa tuna “siku ya nane.” Sasa, kuna siku saba tu, lakini hapa tunazungumza juu ya “siku ya nane,” kusanyiko takatifu, kusanyiko. Angalia, “Msifanye kazi siku hiyo.” Ile siku ya nane, ni (nini?) kurudi kwenye siku ya kwanza. Mbona, inanena juu ya Umilele, inapozunguka bila mahali pa kusimama. Amina. Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>215</sup> Angalia, ilikuwa pia ni katika siku hii ya nane. Siku ya mwisho, ya sikukuu ya vibanda, angalia baada ya hiyo, baada ya sikukuu ya mwisho, baada ya Wakatia wa mwisho wa Kanisa, baada ya siku saba nzima za mwisho juu ya nchi, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, ndipo Kusanyiko hili Takatifu linakuja.

<sup>216</sup> Kumbuka, hii ni sikukuu ya vibanda, *vibanda*, “mahali pa kukusanyikia.” Amina! Ambapo, “Katika Utawala wa Miaka Elfu,” Biblia ilisema, “watajenga nyumba; na kukaa ndani yake.”

<sup>217</sup> Lakini katika ile Nchi Mpya, Yeye tayari ameenda akaandaa mahali. Pameisha jengwa. Sisi hatuna uhusiano wo wote na kujengwa kwake. Amina. Milele! Loo! mimi nalipenda tu Neno hilo! Jamani! Kusanyiko Takatifu, siku ya nane. Ambapo, kuna siku saba tu. Halafu kwenye siku ya nane, ambapo inarudi kwenye siku ya kwanza tena, inarudi moja kwa moja kwenye siku ya kwanza, siku ya nane ni Kusanyiko Takati- . . . Takatifu.

<sup>218</sup> Angalia, siku saba, zinahusiana tu na ule uumbaji wa kale, wakati wa dunia. Siku saba, huo ni ule Utawala wa Miaka Elfu, siku ya raha. Kama vile Mungu alivyofanya kazi siku sita, akastarehe ya saba; Kanisa linafanya kazi siku sita, na kustarehe kwenye ya saba, lakini ungali uko katika kipindi cha wakati. Sineni juu ya Milele.

<sup>219</sup> Lakini, mnaona, hakuna kitu kama siku ya nane; unarudi kwenye siku ya kwanza tena, unaona, siku ya kwanza.

<sup>220</sup> Sabato inanena juu ya torati ya kale, ambayo ilikuwa ya kupita. Kule kuadhimisha sabato, ambayo “ilipita,” au, nimesema, “ilibadilika ikawa nyngine.” Haikupita; ilibadilika tu kutoka ile torati ya zamani, ya kuadhimisha siku fulani ya juma.

<sup>221</sup> Isaya, sura ya 19, ilisema, ninaamini 28:19, ilisema, “Amri lazima iwe juu ya amri; huku kidogo, na huku kidogo.” “Lishikeni lililo jema.” “La, bali kwa watu wageni, na kwa lugha nyngine nitasema na watu hawa. Na huku ndiko kuburudika.” Mnaona?

<sup>222</sup> Unaingia katika Uzima, si kuadhimisha siku fulani au kivuli. Paulo alisema, pale katika Waebrania sura ya 4. “Mnashika siku na vivuli, na vitu kama hivyo; nachelea ujuzi wenu.” Mnaona, sisi hatuingii katika siku fulani na taratibu. “Mmepita kutoka

mautini kuingia Uzima wa Milele,” si siku na majira. Mmepita mautini mkaingia katika Umilele. Hilo ndilo kusanyiko taka-... kusanyiko, kusanyiko, hasa.

<sup>223</sup> *Siku saba*, angalia, ambazo “hupita,” au, nilivyosema, “zinabadilika zikawa nytingine.” Siku nane zinahusiana na uumbaji mpya, mnaona, si ule uumbaji wa kale. Siku nane ni uumbaji mpya.

<sup>224</sup> Kwa kuwa, ilikuwa katika siku ya nane ambapo Bwana wetu alifufuka katika wafu. Hilo hapo kusanyiko lako lingine, utakatifu; si kufikiria sabato, hata kidogo, ama sikukuu za vibanda, sikukuu ya *hii*, na sikukuu ya pentekoste. Yesu alifufuka katika wafu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, katika siku ya nane. Baada ya zile sabato saba, ama siku saba, Nyakati Saba za Kanisa, Yesu alifufuka katika wafu. Siku ya nane, ambayo ni kusanyiko takatifu, mnaona, ambayo ni siku ya kwanza.

<sup>225</sup> Mnaona, mmeninii, mmekwisha pita katika wakati, mkaingia katika Umilele tena; si kuadhimisha siku, na kuadhimisha sabato; na miandamo ya mwezi, na vitu kama hivyo. “Lakini *umepita*,” umebadilisha hali yako; si kukuangamiza. Utukufu! “Bali kupita kutoka mautini kuingia katika Uzima wa Milele.” Loo! mambo ambayo Biblia inatufundisha! Mnaona, kupita kutoka moja kuingia nytingine.

<sup>226</sup> Sawa, “kupita,” ile sabato ya kale imepita. Yesu alifufuka katika siku ya nane. Hiyo ilikuwa siku tukufu, takatifu. Wala haikuwa siku fulani; maana siku, wakati, ulikuwa tayari umekwisha. Ulipita ukaingia katika Umilele. Mnaona, iligeuka moja kwa moja ikarudi kwenye siku ya kwanza tena. Mnaona?

<sup>227</sup> Umilele ni kama du-duara. Huwezi kupata kona kwake. Huwezi kupata mahali pa kusimama katika duara kamilifu. Unaendelea na kuendelea. Sijali unaenda umbali gani, ungali unaenda. Unaweza kuanza kuzunguka namna *hii*; uende kuditia kwenye sakafu, kuditia duniani, uende nje ya dunia, ungali unae-... [Mahali patupu katika kanda—Mh.]

<sup>228</sup> Vitu vyote vilivyoumbwa hapa chini, vilivyopotoshwa, si kuumbwa, na Shetani, vitaanguka wakati ile kengele kuu ya dhahabu itakapolia na Baragumu ikilia.

<sup>229</sup> Na kule nyuma hapo mwanzo, ambapo ile nguzo ya kushikiza ilifanywa kule Edeni, wakati mwanadamu alipokuja duniani na akaanguka, mwana-kondoo mdogo alimwaga Damu Yake. Kalvari iliinua msalaba, ulioshikiza Agano la Kale; kwao hao waliohesabiwa haki, walioutazamia Huo. Na katika wakati huu mpya, kwenye kule Kuja kwa Bwana, kwenye Nchi Mpya, ile kamba ya wokovu (ile Damu, zile Nguvu za ukombozi ambazo ninanena habari zake, na katika utaratibu uo huo imemkomboa mwanadamu na nchi pia) itafufuka katika Umilele tena. Na

lile Ziwa la Moto litateketeza kila kitu kisichomcha Mungu na kisichochaguliwa tangu zamani Kwake. Mnaona jambo hilo?

<sup>230</sup> Angalia, ile siku ya nane, Yesu alifufuka tupate kuhesabiwa haki. Yule Mfalme wa Milele, mwenye Ufalme wa Milele wa kubatiziwa nao, kupata Uzima wa Milele. Si siku saba; haikuwa na uhusiano na siku yo yote. Inanena juu ya nyine, Milele, inayokuja; ikizungumzia juu ya wakati wa Milele, Ulimwengu ninaonena habari zake.

<sup>231</sup> Pia, angalia, baada ya siku hamsini, ama sabato saba kutoka hapo, tena kunakuja siku nyine takatifu. Nini kilitukia? Roho Mtakatifu alishuka kwenye Siku ya Pentekoste, kwenye siku ya saba . . . Ama, siku ya nane, hasa, siku ya nane, akashuka kwenye siku ya nane. Ilikuwa sabato saba baadaye, kikamilifu kabisa baada ya kufufuka Kwake, mnaona; kwa hiyo ingekuwa mara saba ya hizo tena, kuileta tena kwenye siku ya kwanza ya juma tena, kikamilifu kabisa. Mnaona?

<sup>232</sup> Hilo hapo kusanyiko lako takatifu, halina uhusiano wo wote na vitu vya kuonekana. Imepita hivyo. Ni kuingiea katika Ufalme wa Mungu, na Uzima wa Milele, pamoja na waliochaguliwa tangu zamani ambao kamwe hawakuanza. Haikuanza katika siku yo yote. Wewe hukuokoka kwenye siku yo yote. Daima ulikuwa umeokolewa. Amina. Yesu alikuja tu kuwakomboa hao; bali uliokolewa, tangu mwanzo, kwa maana ulikuwa na Uzima wa Milele, kwanza.

<sup>233</sup> Samaki wa mtoni hawezi kamwe kuwa samaki sindano ama kiluwiluwi. Huenda akawa katika maji yale yale pamoja naye, lakini alikuwa, tangu mwanzo, samaki wa mtoni. Jarife lilimshika tu, mnaona, bali alikuwa hivyo tangu mwanzo. Kuna hiyo ninii . . .

<sup>234</sup> Sasa, hatujaishiwa na muda wa nyakati. Sivyo? Tuko kabisa kwenye Maandiko. Siku hamsini baadaye, akaja.

<sup>235</sup> Mnaona, nane haiwezi kuhesabiwa pamoja na juma. Mnaona, haiwezi kuhesabiwa, siku nane katika juma moja. Huwezi kufanya jambo hilo, unaona, kwa sababu kuna siku saba tu katika juma moja. Zihesabu namna yo yote utakavyo. Jumapili ndiyo siku ya kwanza ya juma. Unaona, unahesabu saba, ndipo huna budi kurudi na kuanza tena. Unahesabu saba, unarudi na kuhesabu tena. Mnaona?

<sup>236</sup> Nasi tulishi katika mifano hii yote hapa ndani, lakini, unapofikia ya nane, unaingia katika Umilele. Wewe huji kwa torati, wala kawaida za dini, na taratibu. Unakuja kwa kuchaguliwa tangu zamani. Amina! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.] Kuna kusanyiko takatifu halisi na la kweli! Mnaona? Nasi tunamalizia wakati wa saba wa kanissa, wakati wa kanissa, wakati wa Pentekoste. Mnaona jambo hilo? Tunaingia kwenye hilo kusanyiko takatifu. Tunaingia kwenye Umilele huo wa halisi, wa kweli, ambamo Kanisa limeitwa; si

kwenye vituo fulani, madhehebu fulani, bali kwenye Umilele pamoja na Mfalme wao wa Milele. Mnaona? Hatuna hayo hata kidogo, hakuna kitu kama siku, na kadhalika, na nyakati. Umepita ukaingia katika Umilele, ulikotoka. Ulikuwa Kule, kwanzza. Mnaona?

<sup>237</sup> Kama una Uzima wa Milele, kuna wa aina moja tu, huo ni Mungu, nawe ni sifa iliyodhihirishwa. Unaona? Kama wewe... Kama sivyo ulivyo, hutakuweko, hata hivyo. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Mnaona? Ambapo, "yanapita," mambo haya yote ya kale; bali Mambo haya hayapiti, kwa hiyo yananena juu ya Umilele. Roho Mtakatifu ni wa Milele. Halafu, wewe uko katika Umilele, mahali ulipokuwa wakati wote, lakini umetambua tu hivi punde jambo lililotukia.

<sup>238</sup> Unaona, wewe ulifanywa kwa ajili ya kusudi la Milele, kwa maana ulikuwa dhi-dhihirisho la sifa iliyokuwa ndani ya Mungu, ambaye alikuwazia na akakutamka; Naye akaifanya dunia apate kukutwaa toka kwake, na kukufanya mwanadamu. Ndipo dhambi ikaja ikapotosha njia Yake. Ulikuja, hata hivyo, bali ulikuwa umepotea pamoja na ulimwengu. Kwa hiyo Yeye akaja na kukukomboa, sifa iliyotamkwa, kisha anaikomboa dunia hii kwa njia ile ile. Halafu, kusudi Lake linaendelea. Mnaona? Loo! Haleluya! Loo! jambo hilo linanisaidia sana, kuwazia tu juu ya mambo yajayo!

<sup>239</sup> Sasa, katika Waefeso 1:10, inaitwa...Sasa, kama unaandika, Waefeso 1:10, inaitwa, si muda wa wakati, si siku ya saba. Inaitwa, "Utimilifu wa wakati." Na "wakati utimiilifu wa wakati" umetimia, hapo ndipo wakati utakapokwuwa umekwisha kutimizwa. Wakati hakuna wakati tena, basi unaingia katika Umilele, baada ya wakati wa saba wa kanisa kuisha, na umekwisha; wakati wa Luther umekwisha, wakati wa Methodisti umekwisha, wakati wa Pentekoste umekwisha. Na sasa unaingia katika (nini?) Umilele; hakuna saba tena, hakuna tatu tena, hakuna nyingine tena. Wao wako katika Umilele, ambako hakuna wakati kama namba, na nyakati, na kadhalika. Amina! Loo, jamani! Mnaona jambo hilo sasa?

<sup>240</sup> Ama, baada ya wakati kutimizwa, dhambi zote zimekwisha, ziemondolewa, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, kwenye ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. (Mfano, kwa Roho Mtakatifu.) Baaada ya ulimwengu kushika moto na kubatizwa, ubatizo wake wa Moto mtakatifu kutoka Mbininguni; dhambi zote zimekwisha, virusi vyote vimekwisha, pepo wote wamekwisha, kuigi-, majaribu yote yamekwisha, uovu wote umekwisha. (Mfano sasa.) Basi Mungu anafanya nini? Yeye anaweza kuketi juu ya nchi, mnaona, kwa maana dhambi zote zimekwisha.

<sup>241</sup> Hilo ndilo jambo lile lile analofanya Yeye anapokupa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto. Yeye anaweza kuja na

kuishi pamoja nawe, nasi tunaweza kuketi katika Ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, kwa sababu tayari tuko ndani Yake. Si kwamba "tutakuwa." Sasa tunaketi katika Kristo Yesu. Tunaingaje ndani Yake? Kwa ubatizo mmoja wa Roho Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Kristo," ambapo, tumo sasa. Si "tutakuwa" ndani ya Kristo; tuko ndani! Yeye ndiye yule Mfalme mkuu wa kiroho juu ya Roho aliye ndani yetu, kwa sababu tulikuwa ndani Yake hapo mwanzo.

<sup>242</sup> Mnaona, Mungu, hapo mwanzo, wakati alipofikiria juu yako na kufikiria juu ya wengine namna hiyo, akajifikiria Mwenyewe kwamba anaweza kugusika. Hayo yalikuwa ni mawazo Yake. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye aliyaoyesha mawazo Yake kwa Neno. Yeye alisema, "Iwe." "Na iwe," ikawa. "Iwe," ikawa.

<sup>243</sup> Halafu, baada ya kitambo kidogo, Yeye aliendelea kusema "na iwe," mpaka watu wakasema, siku moja, "Usiache Mungu aseme nasi!"

<sup>244</sup> Yeye akasema, "Sasa nitasema nao katika nabii." Mnaona? "Tangu sasa na kuendelea, nitasema nao katika nabii."

<sup>245</sup> Naye nabii akasema, "Kutakuja; kutakuwa," na ikawa, na ikawa. Na ikawa, na ikawa, mnaona, namna hiyo tu. Mnalipata sasa?

<sup>246</sup> "Utimilifu wa wakati" umekuja baada ya wakati kutimizwa. Dhambi imeisha, baada ya ubatizo wa dunia, baada ya ubatizo wa dunia kuifanya mahali panapofaa; hakuna magojwa, hakuna vijidudu vya maradhi; hakuna miiba, hakuna michongoma; hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna majonzi; hakuna uzee, hakuna kitu cha kuwakilisha mauti; hamna kitu kimeenda kombo; sawa; hakuna kitu cha maumbile ya kawaida. Milele!

<sup>247</sup> Basi, sifa zake zimedhihirishwa kwa sababu zilikuwako, kwanza, mwanzoni. Hivyo ndivyo alivyofikiria. [Ndugu Branham anaeleza kwenye ubao—Mh.]

<sup>248</sup> Na kwa hiyo ni nini kilitukia? Yeye aliwaweka Adamu na Hawa hapa duniani, na kusema, "Ongezekeni sasa mkaijaze nchi." Miili yao yote ilikuwa imewekwa hapa nje, kusudi wewe ule na kuunda mwili wako. Hiyo ndiyo njia aliyokuwa nayo ya kufanya jambo hilo.

<sup>249</sup> Lakini dhambi ilikuja na kuukatiza mpango Wake. Nao unaendelea moja kwa moja, vile vile tu, wakati unaendelea moja kwa moja.

<sup>250</sup> Lakini Yesu alifanya nini? Mungu alishuka akajidhihirisha Mwenyewe katika mfano wa Mtu, mwanadamu; akautoa uhai Wake, badala ya kukaa hapa. Ambapo, Yeye alikuwa Mfalme, bali Yeye alijitoa Mwenyewe apate kuwaokoa hao wengine. Mnalipata?

<sup>251</sup> Na wakati yote yatakapokwisha, ndipo linarudishwa pale pale kabisa, na kusudi la Mungu linatimizwa. Huyo hapo

Mfalme wa Milele tena pamoja na raia Wake wa Milele, wamedhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, vile vile hasa alivyokuwa nao; dhambi imeondolewa; ibilisi ameondolewa; yote yamekwisha sasa.

<sup>252</sup> Ni kitu gani kitakachofanya jambo hilo? Dunia hii isingeweza kuwa mahali pa Mbingu kukaa sasa. Hebu iangalie, ile dhambi. Itapaswa kusafishwa.

<sup>253</sup> Hakuna mawamume, hakuna mtu, hakuna mwanamke, mvulana, msichana, sijali yeye ni nani, anayefaa kwenda mimbarani, ama hata kudai kwamba ni Mkristo, bila ya kujazwa na Roho Mtakatifu. Huna haki ya kuiendea meza ya Bwana, ama ushirika wo wote, kutawadha miguu, wala cho chote kile, mpaka umekwisha kusafishwa na Moto Mtakatifu wa Mungu.

<sup>254</sup> Hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri isipokuwa wewe, kama Musa, ukutane Naye huko nje kwenye ile ardhi takatifu, Nguzo ile ya Moto ikining'inia pale, mahali ambapo mtu anajijua alipo. Mnaona?

<sup>255</sup> Angalia jinsi, jinsi tunavyokwenda. Baada ya ubatizo wa Moto wa dunia, vijidudu vyote vya maradhi vimeondolewa, unapafanya mahali panapofaa kwa Mbingu basi kuishi hapa duniani.

<sup>256</sup> Mfano, sasa, wa kuketi katika Ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu; tumepita katika huu, mchafu kama maskini yule mwanamke alivyokuwa, akaingia katika sifa ya Mungu iliyodhihirishwa. "Sasa sisi ni Wana wa Mungu," si tutakuwa. Sisi ni sifa za mawazo ya Mungu. Mnaona?

<sup>257</sup> Sasa mnasema, "Vema, mwangalie kuhani huyu. Je! yeye hakuwa mwana wa Mungu?" Ilithibitika yeye hakuwa. Yeye hakuweza kutambua nini? Je! yeye alisema, "Ninaamini Biblia?" Hakika. Bali hakuweza kutambua Neno lillothibitishwa la wakati huo. Yeye alikuwa tu na kisomo cha kiakili cha kundi fulani lilolokuwa kule nyuma kabla yake.

<sup>258</sup> Na ni jambo lile lile leo! Mnaona? Ninajua hilo ni zito, bali ni Kweli.

<sup>259</sup> Kulikuwako na Neno, kama lilivyonenwa kwa ajili ya siku hiyo sawa sawa kabisa; na, yeye, ingawa alikuwa mwanachuoni, hata hivyo alikuwa mtu mashuhuri, bali hangeweza kulitambua hilo. Kwa nini? Haidhuru alikuwa mwanachuoni jinsi gani, kitu kama hicho, yeye bado hakuwa na uwakilisho wa kuchaguliwa tangu zamani. Mnaona?

<sup>260</sup> Waliochaguliwa tangu zamani ndio tu wafanyao jambo hilo; ndio tu wanaoweza... Kwa sababu, angalia, inathibitisha kuchaguliwa tangu zamani. Maana, kama una Uzima wa Milele, ilikubidi uwe sehemu ya Mungu wakati wote, maana. Yeye Ndiye tu wa Milele. Mnaona jambo hilo? Loo, jamani! Wazia jambo hilo.

<sup>261</sup> Sasa angalia jambo linalotukia katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Dhambi yote imeondolewa, Utawala wa Miaka Elfu sasa unaanza, ni wakati sasa wa Roho Mtakatifu kupachukua mahali Pake.

<sup>262</sup> Kama tu vile anavyofanya ndani yetu, “hupita kutoka mautini kuingia Uzimani,” tukiishi katika Ulimwengu wa roho katika Kristo, katika Uwepo Wake wenye utukufu. Hata mauti ya mwili yatapita wakati huo basi; kama tu vile mauti ya kiroho yamepita sasa.

<sup>263</sup> Hakuna kitu kama mauti ya kiroho sasa, kwa—kwa—kwa m—mtakatifu wa Mungu aliyebatizwa. “Ingawa amekufa, hata hivyo ataishi. Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakuwa kamwe.” Maandiko yote, hayana budi kutimizwa. Mnaona? Huwezi kuwa. Una Uzima wa Milele. Jambo pekee, Mkombozi amekufanya wewe utambue jambo hilo. Nawe daima ulikuwa Hivyo, na hiyo ndiyo sababu unaona siku unayoishi. Ni wangapi wanaoiona? Inua mkono wako. Mnaona? Asanteni. Mnaona? Siku tunayoishi, unaitambua.

<sup>264</sup> Sasa, Mmethodisti alisema, “Unapopiga makelele, umempata Huyo.” Wengi walipiga makelele, wala hawakumpata Huyo.

<sup>265</sup> Mpentekoste alisema, “Wakati unaponena kwa lugha, unaye Huyo.” Wengi walinenya kwa lugha, wala hawakuwa Naye.

<sup>266</sup> Angalia jinsi, kila namna ya taratibu walizokuwa nazo Mafarisayo wale, bali wakati Neno lilipodhihirishwa, wao hawakulitambua Hilo. Mnaona? Mnaona?

<sup>267</sup> Na iwapo wewe ni Bibi-arusi, Bibi-arusi ni sehemu ya Mume. Na kama... Mahali pekee utakapoweza kultambua Hilo, ni kutambua ni sehemu gani ya Mume (Neno hilo) uliyo, la sivyo huwezi kujitambua kwamba wewe ni Bibi-arusi. Ni wangapi wanaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Mnaona? Huna budi kutambua mahali pako.

<sup>268</sup> Huwezi kupatambua mahali pa mtu mwingine. Vipi kama—vipi kama Musa angalikuja na ujumbe wa Nuhu? Naye Nuhu alikuwa sehemu ya huo, lakini usingalitenda kazi. Vipi kama—kama—kama Yesu angalikuja na Ujumbe wa Musa? Usingalitenda kazi. Unaona, ulikuwa ni wakati mwingine, ulikuwa unabii mwingine, sehemu nyingine ya Neno ilipaswa kutimizwa pale. Wao walikuwa katika siku nyingine ya juma. Sio, kazi ya Jumanne haiwezi kufanywa Jumatano. Na ya Jumatano haina budi kufanywa Jumatano. Mnaona? Kazi ya Jumamosi haina budi kuwa ni kazi ya Jumamosi. Mnaona?

Na, wao, wao walitambua, “Loo! Musa, tuna Musa.”

<sup>269</sup> Yeye alisema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa kuwa Yeye ndiye aliyenena habari Zangu. ‘Bwana Mungu

wenu atawaondokeshea nabii kama nilivyo mimi.”” Mnapata hilo wazo? Loo! jamani! Mnaona?

<sup>270</sup> Kwa hiyo Yesu alisema, kwenye Yohana 14, “Wakati Yeye, Roho Mtakatifu, atakapokuja, atawakumbusha mambo haya, mnaona, awaonyeshe mnaishi katika siku gani. Na halafu, jambo lingine mtakalomjua kwalo, Yeye atawaonyesha mambo yajayo,” mnaona, mnaona, kurudi moja kwa moja kwenye ya kinabii tena, “atakapokuja.” Mnaona?

<sup>271</sup> Katika Nchi Mpya na Mbingu Mpya, hazitatiwa giza tena, wakati Nchi hii Mpya itakapokuja. Ibilisi atafungwa... Shetani, ye ye angali amefunguliwa sasa; ye ye ni mshitaki. Lakini katika Nchi Mpya, ye ye atafungwa na kutupwa kwenye Ziwa la Moto, katika Moto huu mtakatifu.

<sup>272</sup> Kwa hiyo, katika Nchi hii Mpya, hebu tuangalie kwa dakika chache sasa. Katika Nchi hii Mpya, Mbingu hazitakuwa nyeusi tena; la, huko ni kutokana na lile laana, mnaona. Hazitatiwa giza tena na mawingu yenyenye hasira. Pepo hazitavuma juu yake namna hiyo tena. La. Hazitaivunja-vunja miti kamwe, na kuzivunja-vunja nyumba, na kuangusha vitu. Radi na hasira hazitabubujika juu yake kutoka kwa Shetani, na kumwua mtu anayetembea barabarani, wala kuiunguza nyumba. Mnaona? La, hakuna tena. Hakutakuwako na tufani tena zitakazoshuka kwa nguvu, wala dhoruba na vimbunga, na kuzivunja-vunja nyumba, na kuwaua watoto wadogo, na kadhalika. A-ha, havitakuwako tena. Kujaribukuharibu, hakutakuweko huko. Shetani ametupwa nje!

<sup>273</sup> Laiti tungalikuwa na wakati sasa. Ninayaruka tu Maandiko, sasa, ili kwamba tusichelewe sana. Sina budi kuwaombea wagonjwa.

<sup>274</sup> Mbingu na nchi zimekutana; Mungu na mwanadamu wamepatanishwa. Edeni iliyorudishwa imeanza; mnaona, laana yote imeondolewa.

<sup>275</sup> Ni kama tu, laana yote ya dhambi imeondolewa wakati Roho Mtakatifu anapokukubali. Mnaona, wewe humkubali Huyo; Yeye hukukubali wewe, unaoa, maana ni sifa za Mungu. Mnaona, kama Huyo ni Roho Mtakatifu, inamaanisha, Roho wa Mungu; na ni ile sifa, wazo la Mungu, amekukubali kwa kuwa ulichanguliwa kwa kusudi hilo. Mnaona? Hata hivyo, ulizaliwa katika dhambi; bali Mungu alikuwa na sifa hiyo, na hapa ulijidhihirisha wewe mwenyewe hapa duniani, na Yeye anashuka anakuja na kukuchukua. Mnaona, umerudi *hapa; hapa* ndipo pako. Unaona? Unaona, dhambi imepoteza nguzu zake. Hiyo ni kweli. Tamaa ya dhambi tayari imetoka moyoni mwako, wakati Roho Mtakatifu anapoingia. Wewe ni mtu aliyerejezwa upya.

<sup>276</sup> Na kwa hiyo wakati dunia itakaporejezwa upya, na jambo lile lile, hapawezi kuwepo na kulaani tena, hakuna dhoruba tena, hakuna pepo tena, hasa hakuna tufani—tufani, tena. Wewe

umepatanishwa; mwanadamu na Mungu wamekutana. Ile Nchi Mpya itakuwa, imewekwa kwenye uzuri wake wa Edeni tena. Nchi Mpya itaenea, ninii yake, baada ya ubatizo wake wa Moto.

<sup>277</sup> Wazia tu, itashika moto na kuungua. Viumbe vy aasili vitaungua na—na kufumuliwa. Kazi zote duniani zitaunguzwa. Maji yote yatalipuka; yatashika moto na yote kulipuka. Kila kitu kitalipuka. Volkeno zitabubujika na, maili elfu nyngi hewani, matope moto ya mawe yataruka. Kila kirusi...Roho Mtakatifu wa Mungu atasafisha kila waa la dhambi zote na kila kitu. Pepo wote watafungwa na kutupwa kwenye lile Ziwa la Moto, ule Moto ulao, hasira ya Mungu ya Moto.

<sup>278</sup> Hakuna mnyama atakayekuapo huko kukuangamiza tena. Utakapotembea barabarani, katika bustani za maua, hakutakuwako na nyoka pale kukutolea ukali na kukuuma, na mate yake ya sumu kali. Loo, jamani! Si kutapendeza ajabu? Sikilizeni. Hakuna sehemu yo yote ya Nchi hiyo Mpya itakayoweka tuta la udongo wa majano na kulundikwa kufanya mahali palipoinuka, ama kaburi; hapatakuwako na yo yote ya hayo.

<sup>279</sup> Mwanadamu na Mungu wamekutana; Bibi-arusi na Bwana Arusi. Mbingu na nchi zimekumbatiana; Mungu ameshuka kuishi katya watu. Maskani Yake iko pamoja nao.

<sup>280</sup> Hakutakuwako na dhambi tena, hakuna huzuni tena. Kamwe hakutakuwako na tone la majonzi kutoka mashavuni mwa mama, kwa ajili ya mtoto wake mchanga. Amina. Hakutakuwako na hayo, kwenye Ardhi hiyo Mpya. La. Hiyo imekombolewa. Ni mali Yake, na kwa walio Wake waliokombolewa kutoka humo. Mnaona?

<sup>281</sup> Tena, angalieni, ninyi ni sehemu ya ardhi hiyo. Hiyo ni kweli? Na wakati Yeye alipowakomboa nyinyi, Yeye aliikomboa nchi kwa kitu kile kile, nanyi mko pamoja tena. Loo! inaweza kuwa dhahiri kiasi gani zaidi. Mnaona? Huna budi kukombolewa kwa sababu wewe ni sehemu yake. Na iwapo Damu haikukudondokea, hujakombolewa bado; hujaitwa. Ndipo Yeye anaisafisha; hilo ndilo jambo lile lile analofanya katika Moto. Hata ingawa, Damu ilimwagika, bado ingali haina budi kusafishwa kwa Moto, hiyo ni kweli, ipate kuwa mahali pa kukaa pa Mungu.

<sup>282</sup> Mungu tayari amechukua makao Yake, kwa uwezekano usio dhahiri. Ufalme wa Mungu umo duniani sasa, katika miyo ya watakatifu Wake. Ni sifa Zake alizoanza hapo mwanzo. Sasa sifa Zake zimekombolewa. Yeye anangojea nini? Kuikomboa ardhi, kuweka sifa Zake ndani yake, kutimiliza kikamilifu mpango Wake uliokusudiwa tangu zamani. Mnalionia?

<sup>283</sup> Angalia, hakuna makaburi, hakuna matone ya majonzi, hakuna, hakuna tena umwagaji damu. Haitaloweshwa na tone la majonzi au damu yo yote. La. Hakutakuwako na vita tena.

La. Hakuna mawingu ya kipupwe. Hakuna theluji yenyé baridi kifuani mwake; haitakuwapo tena juu yake. Jua kali halitaninii, halitachoma kamwe nyasi zake. Haleluya! Hata jangwa litazaa waridi. "Lile jangwa la kale lenye kunata litachanua, siku moja, kama waridi," Mungu alinena hilo; wakati itakapokombolewa, wakati itakapopata ubatizo Wake wa Moto. Mna kila aina ya mipungate na miiba na kila kitu pale sasa, bali inangojea ubatizo wa Moto unaokuja.

<sup>284</sup> Kama vile yule mtu alivyokuwa, wakati alipokuwa angali na chuki, husuda na ugomvi ndani yake; wakati ubatizo wa Moto ulipokuja, ulivisafisha kabisa. Hakuna vivu tena, hakuna kitu tena; ni mahali tu anapoishi Mungu kabisa. Pia, kumbukeni, hao ni raia Wake watakaokutana Naye kule ng'ambo. Amina! Loo! ni ninii jinsi gani . . .

<sup>285</sup> Hiyo si hadithi tu; hiyo ni Kweli. Hivyo ndivyo alivyosema Mungu. Hivyo ndivyo alivyoahidi. Hicho ndicho Bibi-arusi anachoendea. "Hata jangwa," Yeye alisema, "litatoa maua, na kuwa waridi."

<sup>286</sup> Shetani, dhambi, wenye dhambi, wameondolewa, milele. Yote yemetoweshwa; yakaingia katika Umilele. Na yote yalikuwa yamepotoshwa, yule malaika mkuu aliyeketi pale siku moja, Shetani, aliyetenda maovu haya yote, ataangamizwa. Mnakumbuka, Biblia ilisema, "Kama nafsi hiyo haitafanya kama alivyofanya Yeye, aliyosema yafanywe, Yeye ataiangamiza hata nafsi hiyo."

<sup>287</sup> Lakini, mnaona, Yeye hawezi kujiangamiza Mwenyewe na abaki Mungu. Kwa hiyo, kama nafsi hiyo ni ya duniani, haina budi kuangamizwa. Lakini kama ni ya Milele, pamoja na Mungu, kamwe haikuanza, kwa sababu ni sehemu ya Mungu na kamwe haiwezi kuangamizwa. Amina! Ni zuri jinsi gani! Ni—ni shukrani jinsi gani, ya kwamba Kanisa linapaswa kuona jambo hilo!

<sup>288</sup> Enyi watu, yote mliyotenda yapo hapa. Hivi ndivyo ninavyojaribu kusema. Ninaacha baadhi yake kwa sababu nataka kurejea kwenye jambo hilo tena.

<sup>289</sup> Hata mambo haya, Shetani, wenye dhambi, wameondolewa, Milele; kamwe hawatakuwako tena. Wote . . . Mnaona, Shetani hawezi kuumba. Kama anaweza, yeye ni Mungu. Mnaona? Yeye anaweza kupotosha tu yale yaliyokwisha kuumbwa. Mnaona? Na upotovu wote utaninii, kupotosha, kutaangamizwa. Na mauti ni upotoshaji wa uzima; na wakati upotovu utakapomalizika, hakuwezi kuwa na mauti tena. Uzee ni ishara ya mauti; na wakati uzee utakapoondolewa, uzima utaingia. Kila ishara za upotovu na kila kitu kinginecho kimeondolewa. Miiba na michongoma ni ishara ya dhambi, "dunia italaaniwa pamoja nayo," na vinaondolewa. Maradhi yanakuja, kwa njia

hiyo; yataondolewa. Mauti yataondolewa. Umwagaji damu utaondolewa.

<sup>290</sup> Hakuna kitu kitakachogusa bumba hilo la udongo ila utakatifu, hao Waliokombolewa. Loo, jamani! Naam. Loo! ninajisikia tu vizuri sana. Mungu, na viumbe Vyake; na viumbe Vyake nya uumbaji huu vimekombolewa kwa Damu Yake Mwenyewe. Vimesafishwa kwa hatua Zake Mwenyewe mbalimbali za kusafisha; za kuua Kwake virusi, na hatua mbalimbali za kuua dhambi!

<sup>291</sup> Ni kama vile kama kitu cho chote kimesafishwa kabisa kuondoa virusi, kusafisha kuzuri kuliko kote tulikowahi kupata kumekuwa ni kwa moto. Unaweza kuchukua cho chote na kukisafisha kwa sabuni na kemikali hizi zote wanazonena habari zake, bado si safi. Lakini hebu wewe kiunguze wakati mmoja!

<sup>292</sup> Na wakati Moto Mtakatifu wa Mungu unapoisafisha dunia kuondoa vijidudu kwa zile Kemikali; Yeye amempandisha Bibiarusi Wake, ambaye anaweza kuingia Mbinguni pamoja Naye, wakati jambo hili linapoendelea. Na kurudi duniani tena, Mbingu Mpya na Nchi Mpya. Kile kipupwe cha kale chenye baridi hakiwezi kudhuru. Vile viangazi vyenye joto kali haviwezi kudhuru. Majangwa yatatoa maua kama mwaridi. Dhambi pamoja na wenyе dhambi vimeondolewa.

<sup>293</sup> Mungu, na viumbe Vyake na uumbaji, wanaishi pamoja katika uhusiano mkamilifu. Kama ambavyo mbingu na nchi ni bwana na mke, ndivyo ilivyo Kristo na Kanisa, nao wote wanakutana katika mpango mmoja mkubwa wa ukombozi na wanaletwa moja kwa moja kwenye kifua cha Mungu tena. Mnaona jambo hilo?

<sup>294</sup> Na katika Nchi Mpya, kuna Mji Mpya. Loo, jamani! Sasa sikilizeni kwa makini. Msisahau jambo hili. Ya kwamba, Yesu alisema, katika Yohana 14, Yeye angeenda kuandaa. "Msifadhaike miyoni mwenu." Wakati anapoondoka, "Nina sababu ya kuondoka. Mmemwamini Mungu," Yeye alisema, "niaminini na Mimi." Wao hawakuweza kuona ya kuwa Yeye alikuwa Mungu. Kasema, "Mmemwamini Mungu, sasa niaminini na Mimi. Nami ninaenda kuwaandalia mahali. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; katika Ufalme wa Baba Yangu kuna majumba mengi ya kifalme." Kristo yuko kule, akiujenga Yerusalem huu Mpya sasa. Sasa sikilizeni kwa makini. Msiondoke. Msikose jambo hili. Kristo yuko Mbinguni, leo, akiandaa Yerusalem Mpya.

<sup>295</sup> Kama tu vile Mungu alivyoumba nchi katika siku sita, akaifanya nchi katika siku sita, ama miaka elfu sita. Kama alivyosema, "Msiwe wajinga," tunasoma katika Maandiko, "miaka elfu moja ni siku moja."

<sup>296</sup> Naye Kristo ameenda na anatuandalia Mahali, ambapo pamekuwa pakijengwa kwa miaka mingi, elfu nydingi sana, akituandalia Mahali. "Nami nikienda na kuwaandalia Mahali, nitarudi tena, na kuwapokea; ili po pote nilipo Mimi, nanyi mwepo." Angalia Mkombozi na Waliokombolewa!

<sup>297</sup> Laiti tungalikuwa na wakati sasa. Nimepaandika hapa, Sulemani akinukuu, "msichana huyu, Bibi-arusi." Loo, yatulazimu kupaacha tu; tumechelewa sana, mnaona. Nitaparejea, tena. "Wakati anapojaribu kumchukua, lakini ye ye ameposwa na mvulana wa kuchunga wanyama." Wengine labda walifikiri huo ulikuwa ni wimbo alioimba. Loo, la. Sulemani ndiye aliyekirithi kiti cha enzi cha Daudi, duniani, bali ilionyesha ya kwamba ufalme huo ilibidi upite. Ilikuwa ni mfano wa Kristo akipendana na Bibi-arusi. Mnaona?

<sup>298</sup> Angalia ya kwamba Yesu alisema, Yohana 14 sasa, "naenda kuwaandalia mahali."

<sup>299</sup> Loo! patakuwaje? Hivi mlipata kuwazia sasa, enyi Bibi-arusi, jinsi patakavyokuwa? Pameandalila na kubuniwa na Mjenzi hodari wa Kiungu. Huu Mji utakuwaje? Sasa tutazungumza habari zake kwa dakika chache. Mjenzi Hodari wa Kiungu amepaandaa, akapabuni. Na, angalia, Yeye amepabuni kwa mikono ya upendo, kwa ajili ya Bibi-arusi Wake mpenzi. Patakuwaje?

<sup>300</sup> Je! Ungeweza kuwazia mtu akioa mke, mtu mwenye uwezo, jinsi anavyojenga na kuweka kila kitu kidogo jinsi mkewe anavyopenda hasa, jinsi angetaka tu? Amina.

<sup>301</sup> Sasa, Mjenzi wa Kiungu ameubuni huo Mji Mpya, ambamo Yeye ataishi pamoja na Bibi-arusi Wake, kulingana na anavyopenda. Si ajabu mtume alisema, "Jicho halijayaona, sikio halijayasikia, wala hayajaingia katika moyo wa mwanadamu." Hebu tuone kama tunaweza kuliingilia kindani kwa muda kidogo tu, tuone jinsi utakavyokuwa.

<sup>302</sup> Mjenzi wa Kiungu ameubuni huu kwa ajili ya mpendwa Wake. Mnaona? Loo! ni mahali pa jinsi gani, wakati, Tabia ya Mungu, Mjenzi Hodari wa Kiungu ameubuni kwa ajili ya sifa za Kiungu ambazo zimechaguliwa Kiungu tangu zamani na Mungu Mtakatifu Ambaye—Ambaye ndiye Mwanzilishi wa Uzima wa Mungu! Huo Mji utakuwaje! Wazia jambo hilo.

<sup>303</sup> Kumbukeni, si Mbinguni. Yohana alisema, "Niliuona ukishuka kutoka Mbinguni." Utakuwa duniani. Mnaona?

<sup>304</sup> Si dunia hii itakayopita; ni dunia iliyokombolewa. Mungu hakusema atainua kizazi kipyta; Yeye atakikomboa kile kilicho hapa. Yeye hatainua kizazi kipyta; Yeye atakikomboa kile kilicho hapa tayari. Yeye hataufanya ulimwengu mpya; ni huu papa hapa. Yeye atauunguza tu kwa moto, autakase, kama alivyokufanyia wewe. Mipango Yake haina budi kudumu milele. Sasa, angalia, itakuwa.

<sup>305</sup> Kumbuka, hautakuwa Mbinguni. “Unashuka kutoka Mbinguni.” Ni Mahali pa kukaa, Mahali pa kukaa, kuchukua maskani Yake. Kama, ilikuwa ni Yohana, katika kisiwa cha Patmo, hapa katika Ufunuo 21, yeye aliuona “ukishika.” Yohana aliuona ule Mji, “ukishuka kutoka Mbinguni,” kama hua, kama alivyouona.

<sup>306</sup> Huyu hapa Mungu anakuja, anashuka juu ya maskani Yake duniani, Yesu, katika . . . “akishuka kutoka Mbinguni.” Yesu alibatizwa, akaenda moja kwa moja . . .

<sup>307</sup> Wakati alipokutana na nabii! “Neno humjia nabii.” Na Yeye alikuwa Neno. Naye nabii alikuwa amesimama pale, akikana madhehebu yao yote, kila kitu. Na, wakati alipoona Neno, Neno lilimjia moja kwa moja.

<sup>308</sup> Naye nabii alifadhaika sana, akasema, “Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe. Mbona waja kwangu?”

<sup>309</sup> Yeye akasema, “Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo (tunajua ujumbe) kuitimiza haki yote. Mimi ndiye ile Dhabihu; haina budi kuoshwa.” Akamkubalia.

<sup>310</sup> Wakati alipotoka majini, yeye alisema, “Niliona mbingu zimefunuka.” Nabii aliziona. Aliona mbingu zimefunuka.

<sup>311</sup> Naye huyu hapa anakuja, akishuka kutoka Mbinguni, mfano wa Hua; na Sauti ikitisema, “Hii ni sehemu Yangu ya nchi ambayo nimeikomboa, na kutoka kwenye sehemu hii ya nchi nitaikomboa ile nyngine iliyobakia, kwa kuwa Yeye ni Neno Langu lilitodhihirishwa.” “Na ulimwengu mzima, niliunena ukawepo kwa Neno Langu,” Wabrania 11. “Naye Shetani ameushikilia wakati huu wote, bali nimekuja kuukomboa. Kiasi fulani chake kimeufanya mwili Wake, Nami ninakuja kukaa ndani yake.”

<sup>312</sup> Yohana alisema, “Nikaona Mji ule mtakatifu, Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni, kama Bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa Mumewe.” Nao ulikaa wapi? Kama tu hasa ulivyofanya kule; juu ya nchi.

<sup>313</sup> Yesu alikuwa sehemu ya dunia ile ambayo Roho Mtakatifu alishuka kuikaa, (hiyo ni kweli?) na akakaa Kwake milele. Hawezi kumwacha kamwe. Yeye daima yuko. Yeye na Mungu ni Mmoja. Hana budi kudumu daima!

<sup>314</sup> Na kwa hiyo Yohana akaona Mji ule Mtakatifu, ule Yerusalemu Mpya, ukishuka kama kimondo, ama hu-hua, ukishuka kutoka Mbinguni na kukaa juu ya dunia nzima, iliyokombolewa, (kufanya nini?) kudai kila sifa kwa kusudi aliloifanya dunia. Kila mtu aliywakilishwa katika ule Umilele, na kila mwanamke, basi amekombolewa. Imeunguzwa na kusafishwa kwa Moto.

<sup>315</sup> Yesu, katika majaribu Yake makali jangwani, kwa siku arobaini. Baada ya hayo, angalia, alikuwa tayari kwa huduma Yake wakati huo.

<sup>316</sup> Wazia jambo hilo, Roho Mtakatifu akishuka juu ya nchi, Yesu, na hiyo Damu takatifu! Sasa angalieni, nami ninatumainia sitaingia kwenye kilindi sana kwenu ninyi, mnaona. Damu ile takatifu iliyoumbwa [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara kadha—Mh.] na Mungu; ile Damu, ule Uzima, uumbaji wa Mungu. “Yesu alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu.” Loo! Mnaona jambo hilo? Mungu, akifanywa katika uumbaji. Yeye alikuwa ni Roho. Biblia ilisema, “Yeye ni mwanzo wa kuumba kwa Mungu.” Yeye alianza namna gani? Katika tumbo la uzazi la mwanamke. Ambaye ni nini? Mwanamke si . . .

<sup>317</sup> Kama vile hao vipofu wasivyoweza kuona ule “uzao” wa nyoka papa hapa. Mnaona? Hawa aliwekwa hapa duniani, na, kabla Shetani hajamgusa bado, ama kitu cho chote kile, Mungu aliwaambia, “Ongezekeni mkajaze nchi.” Hiyo ni kweli, lakini Shetani anaingia hapa. Na, kama huyo alikuwa mwana wa Adamu, basi ni wapi . . .

<sup>318</sup> Adamu alitoka moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Nawe unachukua tu tabia ya wazazi wako.

<sup>319</sup> Nawe unapozaliwa mara ya pili, unachukua tabia ya Mzazi Wako, wa Mbinguni. Na Mzazi wa Mbinguni ni sifa za Neno . . . Ama, Neno ni sifa za Mzazi wako. Basi, unawezaje kukana, kwa ajili ya madhehebu fulani? Loo, jamani!

Na—na—natumaini hutakosa jambo hili. Ninajua linatoka kwa Mungu.

<sup>320</sup> Yesu. Huyu hapa anakuja, akishuka; na pale alikuwako Yesu, ile sifa ya Mungu.

<sup>321</sup> Sasa, “yule mwanamke,” yeye. Angalia. Mungu alisema, “Sababu wamefanya jambo hili,” kasema, “nitaweka uadui kati ya Mzao wako na Uzao wa nyoka.” Hiyo ni kweli? Na mwanamke hana mbegu yo yote. Hivi ulipata kuwazia jambo hilo? Yeye ana shamba, si mbegu. Mnaona, nyoka tayari alikuwa amepanda “mbegu” yake mle.

<sup>322</sup> Basi, kama mwanamke hana mbegu, hana budi angojee kusudi apate Uzao.

<sup>323</sup> Mnaona, kuititia kwa kujuana kimwili hapa, aliletu kutoka kwa Shetani, yule nyoka, ambaye hakuwa kiumbe kitambaacho; alikuwa na miguu, maana miguu yake iling’olewa. Yeye alikuwa ndiye mwerevu sana, mnyama pekee ambaye ange—angeshirikiana na mwanamke.

<sup>324</sup> Mbegu ya mnyama isingefanya jambo hilo sasa, wala cho chote kile. Wamejaribu. Haiwezekani. Mnaona, mbegu ya uhai kutoka kwa dume la mnyama fulani haiwezi kuingia katika mwanamke. Haiwezekani.

<sup>325</sup> Bali hicho ndicho kitu kilichokuwa cha karibu sana. Mnaona, wao hawawezi kupata hicho kiumbe kati ya sokwe mtu na mwanadamu. Mnaona, kila kimoja, kilipokuwa kikipanda kwenda juu, kutoka kwa ndege, na kuendelea juu hata kufikia tumbili, na kadhalika, kufikia sokwe mtu, halafu kuna “kilichopotea.” Hicho kilikuwa nyoka, si nyoka wa kawaida; amepoteza kila umbo, kwa sababu alilaaninwa.

<sup>326</sup> Sasa, Mungu hakumlaani Adamu; huenda alifanya jambo lile lile, bali Yeye aliilaani nchi, “miiba na michongoma.”

<sup>327</sup> Hakumlaani Hawa, bali alisema Adamu atakuwa “mtawala” wake. Tangu sasa na kuendelea, yeye hajaribu kuhubiri lo lote wala cho chote kile, Adamu ndiye mtawala wake. “Na siku zote za maisha maisha yako, na kwa utungu, na uptaleta uhai wako duniani.” Lakini Yeye alisema, “Nitaweka uadui kati ya Mzao wako . . .”

<sup>328</sup> Sasa, yeye hakuwa na mbegu yo yote, hajawahi kamwe kuwa nayo, kwa hiyo, ilimbidi kupokea Mzao kwa njia fulani. Mungu alimpa Mzao, si kwa kujuana kimwili, bali kwa kuumba.

<sup>329</sup> Hivi ninyi vipofu hamwezi kuona huo ndio “uzoa” wa nyoka? Loo, jamani! Shetani alifika pale kabla ya Adamu; huo ndio uliokuwa ule “uzao.”

<sup>330</sup> Bali mwanamke alipokea Mzao. Ilikuwa ni nini? Mungu Mwenyewe. “Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu.”

<sup>331</sup> Sasa angalia wakati Sethi alipozaliwa, ama Habilii, yeye alikuwa mtu mwenye haki, kutoka kwa babaye. Sethi ni vile vile.

<sup>332</sup> Hivyo huyo mtu mwovu alitokea wapi: mwuaji, mwongo? Mnaona, mnaona mahali alikotoka? Ilibidi iwe ni “uzao,” kwa sababu yeye alikuwa mzao; Kaini alikuwa mtu.

<sup>333</sup> Loo! wako wapi hao watu vipofu? “Mungu wa dunia hii amewapofusha.” Vema, bila shaka Yesu alisema hakuna mtu anayeweza kuliona jambo hilo. Mnaona?

Unasema, “Mbona wao hawalioni?”

<sup>334</sup> Yesu alisema wakati mmoja, akawaambia wanafunzi Wake, “Ninyi mmejaliwa kuujua Ufalme wa Mungu, bali kwao sivyo.”

<sup>335</sup> Na hiyo ndiyo sababu mnatoka kutoka maili elfu na mia tano mraba, mnaona, “Mmejaliwa kuujua Ufalme.” Angalieni, watu wanakuja hata kutoka Afrika Kusini na kila mahali, saa hii iliyoenda wakati Bibi-arusi amekamilika apate kuingia katika ule Ufalme.

Sina tu wakati wa kutosha. Angalia. Angalia sasa, mnaona.

<sup>336</sup> Sasa mwawenza kuona “uzao” wa nyoka pale, kuona jinsi alivyofanya hilo? Kikamilifu kabisa, mnaona. Sasa baadhi yao walisema . . .

<sup>337</sup> Sasa, kama yule jamaa kule Tucson juzijuzi, akijaribu . . . A-ha, huenda anasikiliza kanda hii. Lakini, kama ndivyo, ewe mtu, ninataka kukwambia jambo fulani.

<sup>338</sup> Wakati ye ye aliposema, “Hawa alisema,” hapa ndipo wanapoelekea, “Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana, ama mtu kwa Bwana.”” Mbona, bila shaka. Mungu ana sheria.

<sup>339</sup> Angalia, hebu chukua mbegu na uipande hapa nje shambani ambako kuna ngano, kisha upande michongoma huko. Sijali, jua lile lile na mvua ile ile huotesha mbegu hiyo. Mungu ana sheria, na sheria hiyo haiwezi kuvunjwa.

<sup>340</sup> Sijali kama—kama . . . mwanamke aliye mchafu sana mjini na mwanamume aliye mchafu sana, na hawajafunga ndoa na kila kitu, wangefanya ki—kitendo, na kuishi pamoja na kuzaa mtoto; huyo mtoto hana budi kuja kwa sheria ya Mungu, maana hakuna njia nyingine yo yote. Usipofanya hivyo, unamfanya Shetani kuwa muumba, na basi ni mungu. Loo! jinsi mnavyoweza kuwa vifopu! Mnaona, sheria ya Mungu, bila shaka.

<sup>341</sup> Kama ukiwahi kupata mtoto, sijali kama alikuwa ni Esau, Yakobo, ye yote yule angekuwa, ama mtu ye yote mwenye sifa mbaya, kama ilikuwa ni Yuda, ilimpasa aje kwa njia ya Mungu. Mungu ana sheria.

<sup>342</sup> Biblia ilisema, “Jua huwaangazia wenyewe haki na wasio haki, mvua huwanyeshea wenyewe haki na wai- . . .” Waebrania sura ya 6, na inasema ya kwamba, “M—mvua huinysesha nchi mara kwa mara, kuinywesha, na kuitayarisha kwa kile inacholimiwa, mwajua, hushiriki baraka; bali miiba na michongoma huishi kwa maji yale yale, jua lile lile.” Kwa kuwa, ni sheria ya Mungu, kuivisha kila mbegu, kuifanya kila mbegu ijizae yenye.

<sup>343</sup> Kwa hiyo, ilibidi izae “uzao” wa nyoka. Na hilo daima—daima jambo hilo halikumzuia Mungu; lilitimiza mpango Wake mkamilifu, lilimfanya Yeye kuwa Mkombozi. Kipofu ye yote anapaswa karibu kuona jambo hilo, isipokuwa liwe limefichwa. “Mungu wa ulimwengu huu” amewaficha hilo. Ni dhahiri tu kama jambo lo lote unaloweza kuona. Hivyo ndivyo ilivyo. Huo hapo “uzao” wako wa nyoka. Sasa angalia.

Lakini, “Yesu alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu.”

<sup>344</sup> Sasa mwanamke anafanya nini? Wakati, chembechembe ya uhai inapotoka kwa mwanamume. Sasa utakataa jambo hilo? Mwanamke hana uhai ndani yake, hata kidogo. Yeye ana yai do go tu, ambalo ni shamba hapa nje.

<sup>345</sup> Ni kama ukichukua shamba na kulilima lote, na—na kulipiga dawa ya waduu, na kunyunyizia vijidudu vy ya magonjwa vyote uvimalize. Na wala—wala hakuna hata nyasi wala cho chote kile kingeweza kukua humo; kisha ultie mbolea tena, upande mbegu nzuri humo. Na, kama adui akija na kupanda mbegu za namna nyingine, kanuni ile ile ya Mungu itachipusha mbegu hizo mbili.

<sup>346</sup> Vema, Mungu hakuwa anakusudia jambo hilo kutokea, mnaona. Lakini ni nini kilitukia?

<sup>347</sup> Mnaona, mbegu inayotokana na mwanamume ndiyo huwa na ile sehemu nyekundu ya damu, ambayo ni damu. Katika damu mna uhai. Na kama ukiwahi... Nimeangalia jambo hilo, katika kuwazalisha ng'ombe na mambo kama hayo. Mimi na Ndugu Shakarian tumepita kwenye jambo hilo, na madaktari na kadhalika, tukiangalia jinsi hizo zinavyoingia, wale wakemia. Mnaona? Ndipo hizi hapa zinakuja mbegu kutoka kwa jike, ambazo ni kundi la mayai. Hizi hapa zinakuja mbegu kutoka kwa dume, ambazo ni kundi la chembechembe za uhai.

<sup>348</sup> *Huyu* hana chembechembe za uhai hata kidogo ndani yake. Ni kitu tu kichotolewa kwa mwanamume. Hivyo ndivyo mwanamke alivypata kuwa hapa, kwanza, naye ni shamba tu. Kuna yai; lina udongo wenyewe rotuba kwa ajili ya uhai huu. Na uhai huu unasogea kuingia na kutambaa. Hiyo hapo siri, jinsi ambavyo hiyo...

<sup>349</sup> “Labda,” unasema, “vema, ya kwanza inakutana. Hizo zingine zinakufa.” Vema, vipi, ni nami anayeanzimia jambo hilo. “Vema, ya kwanza.” Itakuwa ni ile iliyo mbele; yai la kwanza lililo mbele, na chembechembe ya uhai ya kwanza? La, la.

<sup>350</sup> Huenda likawa ni yai moja; kule nyuma kabisa, kule nyuma, katikati ya hizo mbegu, itatokea chembechembe ya uhai iende ikutane nalo. Inaonyesha ya kwamba akili fulani huamua kama atakuwa na nywele nyekundu, nywele nyeusi; kama atakuwa mdogo, mkubwa; wa kiume ama wa kike. Mnaona? Huwezi, huwezi kufanya jambo lingine juu yake; halitafanikiwa. Unaweza kuyachanganya pamoja, na kila kitu, haitaleta tofauti yo yote. Mungu ndiye anayeamua jambo hilo. Na baada ya kitambo kidogo, chembechembe ya uhai moja ndogo itatambaa na kuingia kwenye shamba hilo, yai. Ile iliyo na mkia mdogo, kitu kama hicho, kwake, ikijitikisa-tikisa; inaanguka, na hapo uti wa mgongo wa mtoto mchanga unaanza.

<sup>351</sup> Mwanamke ni nini basi? Yeye hana mbegu. Ana shamba la kupokea mbegu. Kwa hiyo ninii...

<sup>352</sup> Mnaona, kuhusu adui aliyetoka kwenda. Wakati yule mpanzi mwema alipotoka kwenda, akaipanda Mbegu njema; ndipo adui akaja nyuma yake, akapanda mbegu za upotovu. “Lakini mvua huwanyeshea wenyewe haki na wasio haki; jua.” Zote hazina budi kukua.

<sup>353</sup> Yesu alisema, “Ziachenii zikue pamoja. Siku ile yatakusanywa yafungwe matita-matita, yale magugu.” Na yanakusanyika sasa, katika madhehebu makubwa; yakielekeea kwenye lile tita kubwa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na mwisho wake ulikuwa ni nini? Ni kuteketezwa. Bali nafaka itawekwa ghalani. Mnaona? Ambapo, zote mbili zinaishi kwa kitu kile kile, maji yale yale, mvua ile ile.

<sup>354</sup> Na mti wa jamii ya mchungwa, huo ni—huo ni nchungwa, utazaa, itabidi uzae; utazaa, kama umepandikizwa, komamanga. Utazaa limau. Utazaa balungi. Mnaona? Lakini halitakuwa chungwa, bali linaishi kwa uhai ule ule unaotolewa na mchungwa.

<sup>355</sup> Madhehebu yameingizwa kwenye Mzabibu. Kwa sababu, kama wao wanadai ni “Wakristo,” wao wanaishi huo. Kayafa alikuwa, mnajua alichokuwa, na yeye hata hivyo alitabiri. Mnaona? Mnaona, wanaishi kwa huo.

<sup>356</sup> Loo! laiti ningalikuwa na juma moja, ambapo tungejifunza jambo hilo lote, na kulifanya wazi sana ha—hamwezi mkakosa kuliona. Sasa nitaacha baadhi ya mambo haya.

<sup>357</sup> Sasa angalieni. Angalieni, mikono hiyo iliubuni huu kwa ajili ya Bibi-arusi Wake Mpendwa, ikaubuni kwa upendo mwema kwa ajili ya Bibi-arusi Wake.

<sup>358</sup> Kumbukeni ya kwamba Roho Mtakatifu alishuka juu ya Yesu, ambapo, Yesu alikuwa sehemu ya dunia. Kwa nini? Chembechembe ya uhai ya Mungu, Uzima wa Mungu, ulibuniwa katika tumbo la uzazi la mwanamke (hiyo ni kweli?), ambalo lilikuwa ni dunia. Vema. Ndipo Uzima wa Mungu ukaingia, kwa hiyo, “Yeye alikuwa mwanza wa kuumba kwa Mungu.” Mnaona? Halafu Damu hiyo ya Mungu, iliyokuweko mle kwa njia ya chembechembe hiyo hai; ilipomwagwa pale Kalvari, ilidondoka juu ya nchi. Kwa ajili gani? Kuikomboa dunia. Sasa, imehesabiwa haki; imetakaswa; ikaitwa, ikadaiwa; na sasa itapokea ubatizo wa Moto, na kusafishwa kwa ajili ya Yesu na Bibi-arusi Wake.

<sup>359</sup> Nawe ndiwe sehemu hizi zingine zilizotolewa kutoka katika dunia hii. Dunia, wewe ni sehemu ya dunia; mwili wako. Nafsi yako ni sehemu ya Mungu, sifa ya Mungu, iliyodhihirishwa hapa duniani katika mwili. Huo mwili utakombolewa.

<sup>360</sup> Sasa, nafsi imekombolewa, kwa maana ilikuwa katika dhambi. Kwa hiyo Mungu akashuka, kwa hatua za kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuikomboa nafsi yako.

<sup>361</sup> Nawe, ukiwa sehemu ya dunia, umekombolewa nayo. Uko katika hatua sasa. Inaendelea kukua. Mwili wako ulihesabiwa haki chini ya ubatizo wa Nuhu. Amina! Na, mwili wako, wakati Hiyo ilipodondoshwa kule juu yake. Nayo dunia itatakaswa kwa Moto, mahali utakapoishi, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu; Mahali atakapokaa Kristo na Bibi-arusi Wake, Yerusealemu Mpya.

<sup>362</sup> Angalia Mji huu; dunia, utakaa duniani. Sasa manaweza kuona dhahiri kama nilivyosema mimi, ninii...badiliko hili, dunia haina bui kubadilishwa. Haiwezi kubaki hivi. Kanisa lisингeweza kwenda...Ama, ulimwengu usingeweza kuendelea, baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, bila ya kubadilishwa.

Mnaona? Kuwa na Mahali kama hapo ndani yake, itabidi ubadilishwe.

<sup>363</sup> Ni kama tu hivi, hatuna budi kubadilishwa na Moto Wake mtakatifu, kusudi tutayarishe na kuandaa mahali Yeye anapoweza kukaa ndani yetu; hiyo ni kusema, Roho Mtakatifu.

<sup>364</sup> Angalia sasa, kutakuwa na nafasi tele katika Nchi Mpya. A-ha. Mnaona, nafasi tele! Itafanywa upya, hiyo ni kweli, kwa Moto, bali hakutakuwa na bahari tena. Angalia, ule Mji ni maili elfu na mia tano mraba.

<sup>365</sup> Sasa sikilizenin kwa makini sana tunapochora vipimo hivi. Ninataka kufuta ubao, kwa muda kidogo tu. [Ndugu Branham anafuta michoro yake ya kwanza—Mh.]

<sup>366</sup> Huu hapa ufunuo wenyewe kilindi sana kutoka kwa Mungu. Nitasimama tu. Hakuna moja ya haya mengine... Nitaleta haya mengine, Bwana akipenda.

<sup>367</sup> Angalieni sasa dunia ni... Vema, hebu fungueni katika Kitabu cha Ufunuo, mnawenza kuona jinsi alivyoupima kwa dhira na kwa maili. Elfu mbili na mia tatu... Kwa hiyo sasa tunaona ya kwamba ule—ule Mji umepimwa, “maili elfu moja na mia tano” mraba.

<sup>368</sup> Mnajua huo ungefika wapi? Niliupima, juma hili. Ungetoka Maine mpaka Florida, na kutoka pwani ya magharibi mpaka maili sita mbele, magharibi ya Mississippi. Kwa maneno megine, nusu ya Marekani, kwa ajili ya huo Mji tu.

Mnasema, “Hakuna nafasi.”

<sup>369</sup> Wakati bahari itakapoondoka kutakuwa na nafasi, maana karibu sana sehemu nne kwa tano zake ziko kwenye maji. Hiyo ni kweli? Ule mlipuko utaikausha bahari, utailipua dunia. Loo, jamani! Kumbukeni, maili elfu na mia tano mraba, ni Mji wa namna gani! Na, lakini, kumbukeni, bahari imekwisha ondoka.

<sup>370</sup> “Na mapana yake na marefu yake ni sawa.” Hilo lingueufanya maili elfu na mia tano upande *huu*, na maili elfu na mia tano upande *ule*; maili elfu na mia tano marefu kwa mapana na kwenda juu. Maili elfu moja na mia tano, wazieni jambo hilo, dhahabu safi sana. Na huo Mji ulikuwa umezungushiwa ukuta.

<sup>371</sup> Sasa, sasa, hiyo haimaanishi, kwa kuwa sawa... Ilisema, “Na zile kuta zilikuwa sawasawa na msingi wake,” hiyo haimaanishi ya kwamba ni kitu cha miraba sita ama cha mraba. Kuna kipimo kingine cha kijiografia, ambapo vipimo ni sawasawa, hicho ni, piramidi. Mraba, “ni wa mraba,” na kuta zilizokuwa sawasawa.

<sup>372</sup> Hebu niuchore. [Ndugu Branham anachora mifano kwenye ubao—Mh.] *Mnaona*, mapana, marefu, urefu wa kwenda juu. Tutaingilia jambo fulani, hakika kabisa. Mnaona? Angalieni, vipimo vyta pembe *hii* ni sawasawa kabisa, vyote, marefu

kwa mapana na urefu wa kwenda juu. Kuna kipimo kingine, piramidi, kinachothibitisha jambo hilo.

<sup>373</sup> Hii, ikiwa namna hii, ingejibu kabisa ishara ya Henoko kule Misri, ile piramidi. Sivyo? Henoko, kabla ya yale maangamizi ya gharika, wakati kule kuhesabiwa haki kulipokuwa kunakuja, yeye alitoa ishara, na ndani ya piramidi hii kuna hatua saba zinazoelekeea kwenye chumba cha mfalme. Angalieni kwenye ile hatua ya saba, kama ulipata kuchunguza vile vipimo vyta piramidi, kwamba ni nani anayekuja kumlaki mja, kumjulisha kwa mfalme. Angalia ni vituo vyta nani vinavyosimama pale, nawe utaona siku unayoishi, katika ile piramidi.

<sup>374</sup> Sasa, Mungu alitengeneza Biblia tatu. Sasa, kuna fundisho fulani la piramidi ambalo ni upuuizi, bali kuna piramidi halisi. Mnaona? Angalia. Sasa, Mungu, Biblia ya kwanza... Yeye alitengeneza tatu. Hapana budi kila kitu kiwe katika tatu.

<sup>375</sup> Yesu anakuja mara tatu. Akaja, mara ya kwanza, kumkomboa Bibi-arusi Wake; mara ya pili, kumchukua Bibi-arusi Wake; mara nyingine, pamoja na Bibi-arusi Wake. Mnaona?

<sup>376</sup> Sasa angalia jinsi linavyopendeza. Mnaona? Na katika piramidi hii kulikuweko na hatua saba, na halafu chumba cha mfalme. Nasi tuko katika wakati wa saba wa kanisa, kabla Mfalme hajachukua Kiti Chake cha Enzi. Pia, kumbukeni, ile piramidi haijawekwa jiwe la kifuniko juu yake.

<sup>377</sup> Biblia ya kwanza ya Mungu ilikuwa angani, ile Zodiaka; inaanza na kupitia katika kila wakati. Wa kwanza, mwanzo wa Zodiaka, ni bikira; hivyo ndivyo alivyokuja, mara ya kwanza. Umbo la mwisho katika Zodiaka ni Leo yule simba; kule Kuja Mara ya Pili. Kabla tu hakujakuwako na wale samaki waliokingamana, ambao ni wakati wa kansa; ambao tunaishi sasa.

<sup>378</sup> Kulikuweko na piramidi baada ya jambo hilo, Henoko, ambalo lilishuhudia sawasawa kabisa. Hatungekuwa na wakati wa kuingilia jambo hilo, lakini, siku moja, kwa msaada wa Mungu, nitawaonyesha, inachora hasa vipimo vyta wakati tunaishi. Mnaona?

<sup>379</sup> Angalia, lakini kipimo hiki cha kijigrafia sasa tulicho nacho, ambacho vipimo vyake ni sawasawa, hakimaanishi ya kwamba lazima kitu cha mi—miraba sita. Angalia, hii ingejibu ninii ya Misri... ama ile ishara ya Henoko huko Misri.

<sup>380</sup> Katika wakati wa kusafishwa kwa dunia, kwa ubatizo wake wa Moto, kutakuweko na ninii ya kivolkeno, kitu kama kulipuliwa kwa dunia hii, nayo itasukuma juu kitu kama Mlima mfano wa piramidi. Mnaona? Nafasi tele ya kufanya jambo hilo! Kitu hiki chote kitabadilishwa. Uso wote utabadilishwa. Mnalipata jambo hilo? Itasukuma juu Mlima kama piramidi.

<sup>381</sup> Hii ingelingana hasa na Neno kama ikifanya hivyo, ambalo itafanya. Sasa angalia, kwa kuwa, katika Isaya 65:25, ambapo ndiyo kwanza tusome, Yeye alisema.

*Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema BWANA.*

<sup>382</sup> Loo! “Mlima Wangu mtakatifu wote!” Kumbukeni, daima ni “Mlima.”

<sup>383</sup> Kama kuta zingekuwa zimenyoka juu-na-chini, huo Mji ungeweza tu kuonekana kutoka upande wa nje... ama kutoka ndani, Kiti cha Enzi kinaweza tu kuonekana kutoka upande wa ndani; lakini angalia ungeonekana tu kutoka upande wa ndani.

Lakini sasa tunaona ahadi ya Isaya 4:5. Hebu tuisome tu.

<sup>384</sup> Mna haraka? [Kusanyiko liasema, “La.”—Mh.] La, msiwe na haraka sasa. Sisi—sisi—sisi tunaelekea—tunaelekea kwenye jambo fulani maalum sasa, wakati mwangi—wakati mwangi—mwangi sana ambapo hamna budi kuelewa sasa papa hapa. Maana, ninataka kufanya jambo hili dhahiri. Na kwa hiyo wakati tutakapolirudia tena, nita—nitawaonyesha basi ambapo —ambapo tunazungumzia, ambapo, katika somo letu lifuatalo juu ya jambo hili, kwenye wakati mwagine.

<sup>385</sup> Loo! Bwana Yesu asifiwe! Angalieni hapa, jinsi Maneno yasivyoweza kushindwa. Sasa angalia hapa katika Isaya. Nimeandika hapa, kama ninaweza kulipata tena, hebu kidogo. Isaya 4:5. Sasa sikilizeni, yeye ananena juu ya Kuja kwa Bwana, jinsi ambavyo wanawake wangekuwa wenye tabia mbaya sana. Loo! yeye alisema, “Wanawake saba...” Sikilizeni. Hebu tu tulisome. Angalieni hapa.

*Na siku hiyo wanawake saba watamshika mtu mume mmoja wakisema, Tutakula chakula chetu,...kuvaa nguo zetu wenyewe, lakini tuitwe tu kwa jina lako; utuondolee aibu yetu.*

<sup>386</sup> Huo ni wakati wa mwisho, ambao tunaishi sasa; kuoana, kutaliki, na ukahaba na kila ghasia.

*Siku hiyo chipukizi la BWANA litakuwa zuri, lenye utukufu,...matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza...ajili ya Waisraeli...waliookoka. (Jinsi mlivyookoka hukumu hiyo yote! Mnaona?)*

*Tena itakuwa ya kwamba yeye aliybaki katika Sayuni, na yeye ambaye ameachwa ndani ya Yerusalem, ataitwa...(hebu tuone)...ndani ya Yerusalem ataitwa mtakatifu; yaani kila mmoja aliyeandikwa mionganii mwa hao walio hai ndani ya Yerusalem;*

*Ambapo Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao binti wa Sayuni (kumbukeni, huyo daima ni Bibi-arusi, mnaona)...na atakuwa ameisafisha damu ya*

*Yerusalemu (hao ni Wayahudi waliosalia, pamoja na Bibi-arusi, mnaona) . . . na kati yake, pamoja na roho ya hukumu, moto . . .*

<sup>387</sup> Hiyo daima ni hukumu ya Mungu, wakati atakapotoa hukumu Yake ya mwisho. Anakuuta, anakuhesabia haki, na kukuleta kwenye ukombozi; ndipo hukumu Yake inakushukia, na Roho Mtakatifu na Moto husafisha dhambi. Ndipo wewe ni Wake.

<sup>388</sup> Anaifanyia dunia jambo lile lile, wakati anapoisafisha kwa moto, “na kwa roho wa kuunguza.” Sasa angalieni. Sikilizeni! Mko tayari?

*Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya kusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa . . . moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa Sitara.*

<sup>389</sup> [Ndugu Branham anafafanua kwenye ubao—Mh.] “Bwana, katika siku hiyo, juu yake, ataumba Moto wa Nuru uangaze wakati wa mchana.” Na inaendelea na kusema, “Itakuwa mahali pa kukimbilia, mahali pa kustarehe, mahali pa kujificha.” Angalia, kufanya hasa yale Biblia inenayo, sawa kabisa. Kuta zingalikuwa zimenyoka juu-na-chini, usingeweza kuona. Hazina budi kulala upande. “Mlima Wangu mtakatifu wote . . .” “Yeye ataumba Nuru hii juu ya Mlima huu, nao utakuwa kwa ajili ya sitara.” Loo! tunaimba wimbo ule:

Loo! Mji ule juu ya Mlima,  
Ingawa mimi ni msafiri, ningali ninaupenda;  
Sasa na kote katika nyakati zile,  
Nitakapofika kwenye ule Mji ulio Kilimani.  
Mnaona?

<sup>390</sup> Angalia, Mlima Sinai ndiko Mungu alikoshuka kwenye kilele chake, wakati aliponena na Israeli katika Nguzo ya Moto. Yeye alishuka juu ya kilele cha mlima, Mlima Sinai.

<sup>391</sup> Kwenye ule Mlima wa Kugeuzwa Sura, wakati alipotangaza, “Huyu ni Mwanagu mpendwa; msikieni Yeye,” Yeye alishuka katika Nguzo ya Moto na mwangaza mkuu, juu ya kilele cha mlima, mbele ya Petro, Yakobo, na Yohana. Na, pale ndani, ye ye aliwakilishwa akiwa wote wawili Musa na Eliya; na walionyakuliwa, na wafu waliofufuliwa. Utukufu!

<sup>392</sup> Ule Mji Mpya na Nchi Mpya; ule uumbaji mpya; ule Mji ulio Kilimani, huku Kiti cha Enzi kikiwa juu yake. [Ndugu Branham anachora vielelezo kwenye ubao, katika aya chache zifuatazo—Mh.] Kile Kiti cha Enzi hapa, kwenye kilele; na wakazi, kote kote juu-chini, kwenye Mlima huu.

<sup>393</sup> Na ukuta unaouzunguka huu, ulikuwa na misingi kumi na miwili. Na kila mmoja wao ulikuwa na lile jiwe la kifuani

lililokuwa na Haruni, ambayo yaliwakilisha yale makabila kumi na mawili ya Israeli.

<sup>394</sup> Na, kule milangoni, walikuwa na milango minne imewekwa vile vile kabisa kama lile hekalu kule jangwani, kama lile hemalilivyokuwa jangwani. Angalia kila mmoja, ulikuwa—ulikuwa na mitume, watatu kila upande, mitume kumi na wawili. Kila mmoja... Na marefu yake yalikuwa dhiraa mia na arobaini na nne. Dhiraa mia na arobaini na nne ni kulingana kabisa na futi mia mbili na kumi na sita, zikifanya urefu wa kila moja ya mawe hayo makubwa karibu futi ishirini urefu wa kwenda juu, ile dirii kwenye lango lile, zikifanyiza ukuta huo uliouzunguka ule Mji.

<sup>395</sup> Sasa huo, huo Mji, haukai juu ya ule ukuta, maana mji, maili elfu na mia tano, usingeweza kufanya hivyo. Ni ukuta hapa unaoingilia, kama zile kuta za Yerusalem ya kale. Uliingilia kwenye ukuta, ukaingia mle.

<sup>396</sup> Na kila mmoja wa hizi, ulikuwa na misingi kumi na miwili, na kila mmoja ulikuwa na zumaradi na mawe mabalimbali, ambayo yaliwakilisha makabila kumi na mawili ya Israeli.

<sup>397</sup> Na wale mitume, kila mmoja, kwenye hilo lango moja kubwa, la lulu tupu, kuna jina la mtume mmoja. Na je! Yesu hakusema, “Mtaketi kwenye viti kumi na viwili nya enzi, mkiyahukumu yale makabila kumi na mawili ya Israeli”? Ni nani aliyeketi kwenye lango, kuhukumu, walipoingia kwenye ule Mji? Loo, jamani! Hivyo ndivyo ilivyo. Wafalme wa nchi wakiingia kwenye ule Mji, wanakuja mbele ya hakimu wa kimitume, kama Yesu alivyoahidi. Loo, jamani!

<sup>398</sup> Kwenye Kiti hiki cha Enzi, juu yake, maili elfu na mia tano kwenda juu, ulimwengu mzima utaona Nuru ya ulimwengu, Yesu, ameketi kwenye Kiti cha Enzi juu ya ulimwengu, juu ya Kanisa, juu ya Mlima Sayuni; amba ni maili elfu na mia tano, nusu ya ukubwa wa Marekani, na unainuka juu moja kwa moja hata unaweza kumwoa Yeye kutoka kila mahali ulimwenguni, maili elfu na mia tano kwenda juu.

<sup>399</sup> Na pote juu-na-chini *hapa*, watakuwako Waliokombolewa. Kutakuweko na majumba ya dhahabu safi sana. Kutakuweko na barabara kuu, na bustani kubwa, na bustani. Na Mto wa Uzima ukija, ukitiririka kutoka kwenye Kiti cha Enzi, na kububujikia kwenye magenge madogo na, loo, sehemu za miinuko iliyo sawazishwa. Na Mti wa Uzima utakuwa ukichanua katika kila uwanja; na kuzaa matunda Yake, mara kumi na mbili kwa mwaka, tunda tofauti kila mwezi.

<sup>400</sup> Na wafalme wa dunia watakuja ndani yake na kuleta heshima zao. “Na hayo majani ni ya kuwaponya mataifa,” wakati wafalme watakuwa wanaishi kwa amani kule nje. Wanapotoka nje, watakata mti, kukata jani namna *hiyo*. Kama vile yule hua alivyorudi, kwamba hasira ya Mungu ilikuwa imetulizwa, naye akaleta lile jani la mti kwenye safina. Kwa hiyo wakati mfalme

huyo anapoondoka, akileta utukufu wake kwenye chumba cha Bibi-arusi hapa kwenye ule Mji, ye ye atamwinulia jani jirani yake mfalme, na, "Sisi tuna amani milele." Amina! Kuwaponya mataifa! "Yote yamekwisha. Wakati mmoja tulipigania damu za mmoja kwa mwингine, ndugu. Nasi tumefurahia, na kupiga makelele; na kutupiana risasi, na kuwachoma moto watoto, kila kitu. Lakini sasa kuna amani, kule kuponywa." Si kuponya magonjwa; yote yamekwisha. Kuwaponya mataifa! Amina!

<sup>401</sup> Mji wenyne Kiti cha Enzi kule juu. Ufunuo 21:23, "Nao hawahitaji taa, kwa maana Mwana-Kondoo na Bwana Mungu ndiye Nuru yake." Mnaona? Bwana Mungu ndiye ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli kote jangwani. Naye amepanda kwenye Kiti cha Enzi, katika ule Ufalme mkamilifu... ambapo wakati... "Ule Ufalme ambao Yesu atautoa kwa Baba, ili Mungu apate kuwa yote, na katika yote. Yesu anaketi kwenye Kiti cha Enzi hapa, kama Yusufu wetu. Naye Mfalme ndiye Nuru itakayokuwa juu ya Mlima Sayuni, na Nuru Yake takatifu itaujaza Mji mzima. Haleluya!

<sup>402</sup> Maili elfu na mia tano kwenda juu, na maili elfu na mia tano mraba, pamoja na paradiso za Mungu zimejengwa kote katika Mji huo; mitaa, barabara kuu! Someni Ufunuo 21, mwone kama si kweli. Mnaona, "Hawana haja ya nuru kule, kwa kuwa Mwana-Kondoo ndiye Nuru." Na kwenye kile Kiti cha Enzi anaweza kuonekana, ameketi, maili elfu moja na mia tano.

<sup>403</sup> Hauendi juu moja kwa moja namna *hii*. Unalala upande, kama piramidi. Kama ungekuwa ni nusu ya huo urefu, basi hiyo ingeenda juu namna *hii*, mnaona, kutoka mji mmoja hadi mwингine... sasa kama ukitazama, kutoka kwenye upande mmoja wa Mji hadi mwингine.

<sup>404</sup> Ningeweza kuingiza kitu fulani kidogo hapa kama mnataka nikiingize. Mmeliona kundi hili dogo hapa? Ni kama tu sehemu hiyo, ukubwa wa mzunguko wa eneo lake. Georgia, California, mpaka Saskatchewan; kutoka Kansas, mpaka kwenye pwani ya miamba ya Maine; hizo ndizo zilizokusanyika. Hizo ndizo zinawakilishwa papa hapa, yapata maili elfu na mia tano mraba.

Loo! wanakuja kutoka Mashariki na  
Magharibi,  
Wanakuja kutoka nchi ya mbali;  
Kula pamoja na Mfalme wetu; kula... (kula  
nini? Mtu hataishi kwa mkate tu.) Kwa  
Mkate, Neno!)... kula kama wageni Wake;  
Jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa!

Ulimwenguni, sina budi kusema, sijaona watu kama hao.

Loo, wanautazama uso Wake mtukufu  
Unaometameta kwa Nuru ya Kiungu;  
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,  
Watang'aa kama vito taji Yake.

Loo! Yesu yuaja hivi karibuni,  
 Shida zetu zitakwisha wakati huo.  
 Loo! viyi kama Bwana wetu angekuja wakati  
 huu?

<sup>405</sup> Haitakawia. Kila kitu ni kikamilifu. Kijiografia, Sodoma, wale wajumbe; kila kitu kimekaa sawasawa kabisa. Mnaona? Ina maana gani? Wazieni tu, wakija kwenye Maskani hii moja ndogo, maili elfu moja na mia tano mraba, wakitoka kwenye eneo lile lile.

<sup>406</sup> Ni kwa nini Mungu aliwazia sana na kupajali sana mahali pale padogo pa Palestina, mnaona, pakiwa tu mahali padogo sana? Lakini pale pale ndipo lile hekalu limewekwa. Hapo ndipo Yerusalem Mpya itakapotokea, papo hapo. "Mizeituni, Mlima wa Mizeituni utapasuka, sehemu moja iende kulia na kushoto," hakika, wakati utakaposukuma kutoka chini. Sio, wao wanavyosema, unasukuma na kuachana namna hii. Unasukuma kwenda juu, "Katika siku ile atakapoweka miguu Yake mitakatifu juu ya ule Mlima." Angalia, kwenye Kiti Chake cha Enzi, maili elfu moja na mia tano kwenda juu!

<sup>407</sup> Kumbukeni, Shetani alijitahidi kumjaribu, wakati mmoja, juu ya mlima. Mnaona?

<sup>408</sup> Ule Mji Mpya una misingi kumi na miwili, kama tulivyopitia, wale wazee kumi na wawili; dhiraa mia na arobaini na nne; zikiwa ni ile dirii ya Haruni; milango kumi na miwili ya lulu, majina kumi na mawili ya wanafunzi.

<sup>409</sup> Yesu atasimama, lile Jiwe la Kichwani, kwenye Kiti cha Enzi, wakati watakatifu Wake wamekwisha kumyika taji, "Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana." Naye ndiye lile Jiwe la Kichwani.

<sup>410</sup> Sina kitabu changu cha mfukoni. Lakini kama utaangalia katika kitabu chako cha mfukoni, kama una noti ya dola moja, wana muhuri ya Marekani; tai upande mmoja, ameshika mikuki, kama nembo; na mwisho wa upande wake wa pili, ina piramidi, pamoa na jicho lionalo kila mahali juu yake. Unaona, wao hawakujua walichokuwa wanafanya. Na pale juu imeandikwa kwa Kilatini, nawe utaona ya kwamba inanena hilo, huu ni "ule muhuri mkuu." Wao hawakujua walichokuwa wanafanya. Wala Kayafa hakujuu alikuwa anatabiri.

<sup>411</sup> [Ndugu Branham anaeleza ubaoni—Mh.] Huo hapo ule Muhuri mkuu. Huu *hapa*, mnaona, ule Mji. Si kitu tambarare chenye miraba sita kama hiki, mnaona, bali umekaa upande kusudi upate kuonwa. Na juu ya Mlima huu mtakatifu wa Bwana, Bwana atashuka juu ya Mlima Wake; Huyu *hapa*. Hiyo ndiyo sababu lile jiwe la Kifuniko halikuwekwa na Henoko. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu lile jiwe la Kifuniko halina budi kuja sasa. Nao huo Mlima utasukumwa juu, nao utakuwa Mlima wa Bwana.

<sup>412</sup> Na *hapa* ndani watakaa Waliokombolewa. *Hii*, mitaa mikubwa yenyeye miti na barabara kuu, basi, mashamba mazuri ya kutembelea, na Mto wa Uzima utabubujika, upitie moja kwa moja mle. Na kila nyumba itajengwa kwa dhahabu safi sana. Na barabara zitatengenezwa kwa dhahabu. Na miti ya Uzima itakuwako kule, nayo itazaa aina kumi na mbili za matunda. Na wafalme na watu wenye heshima duniani wataleta heshima zao na utukufu ndani ya yale malango. Na hayo malango hayatafungwa usiku, kwa kuwa hakuna usiku kule.

Katika Mji ule ambako Mwana-Kondoo ndiye Nuru.”

Katika Mji ule ambako hakuna usiku;  
Nina jumba kubwa kule, ambalo halina taabu  
wala mashaka,  
Loo! Ninaenda ambako Mwana-Konoo yule  
ndiye Nuru.

<sup>413</sup> Hivi huoni ya kwamba miji, majiji, majumba, makazi, yana—yananena habari zake sasa hivi? Mambo haya yote ya kawaida ni kivuli.

<sup>414</sup> Chukua kivuli, umbali fulani, kama mkono wangu. Kabla hakujawenza kuwa na kitu ha—halisi... ama negativu, hakuna budi kuwe na kitu halisi. Na, unaona, kivuli hicho, inaonekana kama kwamba nina vidole dazani, lakini basi unapoanza kuvileta pamoja, vinaonekana vizuri kama kimoja, ndipo hicho kivuli kinaishia kwenye mkono.

<sup>415</sup> Na hivyo ndivyo, mara nydingi, watu wanafikiri kuna Miungu watatu au wanne. Unaangalia kule nyuma kabisa kwenye yale natengenezo ya mwanzoni. Unaona? Shuka chini sasa na, unaona, uangalie vizuri sana mpaka uone Mmoja. Hiyo ni kweli kabisa.

<sup>416</sup> Kuna Bibi-arusi mmoja; si dazani, madhehebu. Bali Bibi-arusi mmoja, huyo ni yule aliyyeteuliwa, kutoka kwenye kila... kutoka kwenye—kutoka kwenye dunia ambaye amechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya jambo hili, wale wanaoweza kutambua mahali pao katika ule Ufalme.

<sup>417</sup> Kwenye Kiti hiki cha Enzi, angalia, juu sana! Ule Mji Mpya; wenye misingi; milango kumi na miwili; Yesu, Jiwe la Kichwani; mitume, wakihukumu; makabila kumi na mawili.

<sup>418</sup> Lile piramidi la Henoko halifanyi kivuli wakati wo wote wa mchana. Nimekuwa kule Misri, kwenye yale mapiramidi. Imewekwa kijiografia kabisa, na kwenye vipimo vyta umbo hili kuu la kijiometri; ambapo, hata juu liwe upande gani, hakuna kamwe kivuli kando ya piramidi. Mnaona jinsi ilivy?

<sup>419</sup> Wala hakutakuweko na usiku kule. Yeye akiwa kule juu ya Mlima, anaujaza na utukufu Wake. Nuru ya utukufu Wake itakuwapo kule wakati wote. Hakutakuweko na usiku kule. Yesu, Jiwe la Kichwani!

<sup>420</sup> Sasa angalia. Kwa hiyo, Waliokombolewa watatembea katika Nuru. Sasa sisi huimba, "Tutatembea Nuruni, Nuru ile nzuri." Kuna kitu ndani yetu kinachoita. "Tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ni kwa sababu hiyo inangoja. Mnaona? Hiyo ndiyo sifa, vile tunavyojisikia.

<sup>421</sup> Kweli, hii ni...Mko tayari? Huu ndio Mji ule ambaو Ibrahimu alikuwa anaутаfuta. Mnaona? Akiwa nabii, alijua ya kuwa Mji huo ulikuwa mahali fulani. Biblia ilisema hivyo. Naye akauacha mji alioishi, akaenda kule; angalia mahali alipokwenda, mahali pale pale hasa utakapokuwa. Mnaona? "Alikuwa akiutazamia Mji ambaو Mwenye kuubuni na Kuujenga ni Mungu," mnaona, akiwa nabii.

<sup>422</sup> Yesu ameenda kuandaa, kwa mikono ya Kiungu, Mji wa Kiungu; Mjenzi hodari wa Kiungu, kwa ajili ya watu walionunuliwa na Mungu, kwa ajili ya watu waliochaguliwa tangu zamani. Yeye ameenda kuandaa.

<sup>423</sup> Ibrahimu alikuwa anaутаzamia. "Naye akakiri ya kwamba alikuwa msafiri na mgani, kwa kuwa aliutazamia Mji ambaو Mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu." Nabii huyo, akiuju ulikuwa mahali fulani! Yohana aliouna ukishuka, bali Ibrahimu alifikiri hauna budi kuwa duniani wakati uo huo. Kwa nini? Yeye alikutana na Melkizedeki, Mfalme wake, na kumpa fungu la kumi. "Asiye na baba, wala mama. Hakuwa na mwanzo wa uhai Wake wala mwisho wa uhai Wake." Ibrahimu alikutana Naye, nao wakafanya ushirika mahali pale pale hasa ambapo huo Mji utakapojengwa, ule Mlima Mtakatifu wa Bwana, ambapo Waliokombolewa wataishi. Loo, jamani!

<sup>424</sup> Ile saa haisimami kamwe. La, tuka katika wakati; baada ya kitambo kidogo tutaingia katika Umilele.

<sup>425</sup> Loo! Mlima mtakatifu! Kutakuwako na barabara za dhahabu safi sana, mitaa mikubwa yenye miti; na majumba, na mashamba ya kutembelea. Kama ukitaka kusoma jambo hili, Ufunuo 21:18. Mti wa Uzima utakuwako; aina kumi na mbili za matunda, moja kila mwezi, yatazaliwa juu yake. Watu watakaokula matunda haya, watabadilisha mlo wao kila, kila mwezi.

<sup>426</sup> Na ni—ni kutoka...kwa ajili tu ya wenye kushinda. Mnajua jambo hilo? Si kwa ajili ya madhehebu.

Unasema, "Unamaanisha jambo hilo, Ndugu Branham?"

<sup>427</sup> Na tufungue Ufunuo 2, kwa dakika moja tu, tuone hilo. Ufunuo 2:7. Hebu tuone sasa kama ni Kweli ama si Kweli. Ufunuo 2:7 inasema hivi.

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo  
Roho...*

<sup>428</sup> Sasa, kumbukeni, Yeye hazungumzi na Wayahudi sasa. Hili ni Kanisa, Mataifa.

*Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo  
Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye, nitampa  
kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya  
Mungu.*

<sup>429</sup> “Washindao peke yao, watakaomshinda yule mnyama, kushinda alama yake,” hiyo ni Ukatoliki, Uprotestanti, umadhehebu, “yeye atakayemshinda yule mnyama, alama yake, chapa ya jina lake.” “Yeye atakuwa na amri kuuendea huo Mti wa Uzima, kuingia katika milango ambamo hakuna kinachotia unajisi kinaweza kuingia.” Mnaona? Wazia jambo hilo. Sasa, hebu kidogo sasa, tunapoendelea mbele kidogo. Ule Mti wa Uzima utakuwa kwa ajili ya wenye kushinda peke yao.

<sup>430</sup> Yale majani yatakuwa ya kuwaponya mataifa. Hiyo ni kusema, wafalme wanaoishi mle ndani, wakileta heshima zao ndani, watakapokuwa wanaleta heshima zao ndani na kuziweka mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu. Ni kama tu kule nje, yale kumi... yale makabila kumi yaliletta, kila mmoja wao, fungu la kumi kwa Lawi, mnaona. Wanapoleta heshima zao kwenye... kutoka kwenye nchi iliyobarikiwa, kwamba, wao watanyosha mkono wao kwenye ule Mti wa Uzima, na kuvunja jani la mti... ama jani la Mti wa Uzima, nao watatoka watembee pamoja. Hakuna vita tena. Kila kitu kina amani. Yale majani ni kumbukumbu, kwa ajili ya uponyi wa taifa.

<sup>431</sup> Mti ule ule, si kama Adamu, yeye... Kulikuweko na Mti wa Uzima katika bustani ya Edeni, ambao angaliweza kula kama hakuanguka. Huo Mti wa Uzima ulimkumbusha, wakati wote, ya kwamba ninii yake mpya... ujana wake ulikuwa unaendelea daima. Mnaona?

<sup>432</sup> Vivyo hivyo na mataifa. Majani yatakuwa ya kuwaponya mataifa; angalia, si magojwa sasa. Ungekuwa na haki zile zile alizokuwa nazo Adamu, kama yule ja... hua aliye kuwa na lile jani la mzeituni, yote ni... kila mfalme akichukua jani.

<sup>433</sup> Angalia, ule Mto wa Uzima, labda ukifanywa na vijito vingi vidogo. Sasa, katika dunia hii...

<sup>434</sup> Nitafunga katika dakika chache tu. Katika dunia hii... Ama, nitakoma hivi punde tu. *Hicho* ndicho kiasi cha mihtasari niliyo nayo, sasa kama kurasa thelathini. Naam. Angalieni.

<sup>435</sup> Katika haya—katika maisha haya, sijaona kitu ambacho kinaondoa kiu sana kama kuwa milimani na kupata, kama nilivyo hubiri hivi majuzi usiku, kijito hicho kikibubujika, nguvu zake ziletazo uzima. Ungekuwa mchovu na una kiu, uanguke karibu na kijito kizuri; huko chini kabisa ambako virusi haviwezi kwenda, huko chini kabisa futi mia kadha ndani ya ardhi, yanabubujika maji safi, halisi, yaletayo uzima. Tunathamini jambo hilo. Hilo ni dogo. Sasa, dunia ina vijito vyake vingi vilivyo na maji yaburudishayo. Wakati unapoona kiu

na unakufa, ukipata maji mazuri na baridi kutoka mle, yata—yatakusaidia kuishi.

<sup>436</sup> Lakini angalia mahali Haya yanakotoka. Kutoka kwenye Kiti cha Enzi, huko ndiko yanakopata nguvu zake ziletazo Uzima. Yanatoka chini ya Kiti cha Enzi cha Mungu, ambapo Mungu anaketi.

<sup>437</sup> Yote, dunia hii yote, dunia hii hapa tunamoishi sasa; kila mmoja, awe Mkristo ama mpagani, ana hekalu. Ulipata kufikiria jambo hilo? Makanisa, yote.

<sup>438</sup> Lakini Huu hauna lo lote. Biblia ilisema, “Wala hakukuwepo na hekalu kule. Bali Bwana Mungu na Mwana-Kondoo ndiye Hekalu lake.” Mwana-Kondoo ndiye Nuru. Mwana-Kondoo ndiye Hekalu. Mwana-Kondoo ndiye Kiti cha Enzi. Mwana-Kondoo ndiye Uzima. Yeye ndiye Hekalu lile. Mnaona, mahekalu haya yote yana kitu wanachoabudu; walakin, katika Mji huu, Yeye ndiye hicho kitu. Yeye yuko pamoja na watu Wake. Nuru ya Roho Wake inaangaza Mji ule wa piramidi.

<sup>439</sup> Kama vile Petro na Yohana, wakiwa kule juu ya mlima. Nuru ilifunika kilele cha mlima, kisha sauti ikanena, ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa.”

<sup>440</sup> Katika Ufunuo 21:3 na 4, “Maskani ya Mungu ni pamoja na mwanadamu.” Mungu amefanya maskani Yake katika mwanadamu, kwa kumkomboa, kwa hatua hizi tatu. Sasa Mungu ataikomboa dunia na kufanya maskani Yake duniani, pamoja na raia Wake wa duniani, aliowaleta kutoka katika nchi. Na kwa dhambi ikaanguka, lakini ile... Ilimbidi kuiachilia iendelee. Lakini sasa Yeye alimtuma Yesu kuikomboa dunia ile iliyoanguka, ambayo sisi ni sehemu yake. “Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chenu utakaoangamia.” Yesu alisema hivyo. Yeye alisema, “Nitaufufua tena katika siku ya mwisho.” Mnaona? Kwa nini? Wewe ni sehemu ya dunia.

<sup>441</sup> Unaona, nilikuwa na utani mdogo kuhusu mke wangu kuniambia ya kwamba nimepoteza nywele zangu. Nikamwambia sikuwa nimepoteza hata mmoja.

Akasema, “Ziko wapi?”

<sup>442</sup> Nikasema, “Huko zilikokuwa kabla sijazipata.” Ko kote zilikokuwa, kitu halisi; po pote zilipo, zinaningoja mimi. Mnaona? Hiyo ni kweli. Nitaenda ziliko, siku moja.

<sup>443</sup> Mwili huu mzee, wenye makunyanzi na unaoanguka, na mdhoofu mabegani, na kuuma magotini, na—na umepwelewa na sauti kooni. Hayo ni sawa. Unaweza kuuzika baharini, lakini Baragumu itaniamsha!...?...Naam, bwana. Tutabadilika, moja ya siku hizi. Mimi ni sehemu ya ulimwengu huu uliokombolewa. Wewe uko ulimwenguni, bali hu wa *kidunia*. Wewe ni wa utaratibu mwingine, uliokombolewa.

<sup>444</sup> Angalia, “Maskani ya Mungu itakuwa pamoja na mwanadamu.” Angalia, “Mambo ya kale yamepita. Hiki, kitu hiki, kimepita. Hii ina maana kwamba Mbingu zimeshuka chini kukaa pamoja na mwanadamu. Mnaona? Mbingu na nchi zimekumbatiana.

<sup>445</sup> Jinsi hasa yule Hua alivyokuja juu ya sehemu ya nchi, ambaye alikuwa ni Yesu; Yeye alikuwa mavumbi ya nchi, mwanadamu. Mungu, akitoka kwenye ile chembechembe moja ndogo ya Uzima, kwa nguvu za kuumba. Nayo hiyo Damu iliyokuwa kwenye ule... Ule Uhai uliokuwa katika Damu ile ulipaa ukarudi kwa Mungu, bali Damu ilidondoka juu ya nchi, ipate kuidai. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.]

<sup>446</sup> Kwa sababu ya damu iliyotewa, kutoka kwenye chembechembe hai iliyotoka kwa Kaini, mnaona; sasa Yeye anarudi na nguvu za kuumba kama tu alivyomfanya Adamu, akimuumba Adamu, huyu hapa Adamu wa Pili. Na kupitia kule kuvunjika kwa chembechembe pale, ambapo (dhambi) Kaini aliivunja ile chembechembe ya damu juu ya yule mwenye haki, unaona, sasa Chembechembe hii ya Damu... Kwa sababu, yeye alimwua Habili, lakini Habili alizaliwa kwa kujuana kimwili.

<sup>447</sup> Lakini Huyu hakuzaliwa kwa kujuana kimwili. “Ilikuwa ni kuumba kwa Mungu, mwanzo wake,” na Hiyo ilikomboa dunia. Na kasiamu yote, potasiamu, mafuta, mialimwengu, ulizofanyizwa kwazo, zimekombolewa. “Hakuna unywele hata mmoja utakaodhuriwa. Nami nitaufufua tena katika siku ya mwisho.”

<sup>448</sup> Tena nini? Mungu anashuka kuja kuishi duniani. Ambapo, Yeye ni sehemu ya hiyo, mwili Wake Mwenyewe. Yeye aliufufua kwa kuhesabiwa haki kwetu, nasi tunahesabiwa haki kwa kuamini jambo hilo na kulikubali hilo. Angalia katika mifano, Yesu anakuwa... Katika mfano, Yesu anakuwa mwanadamu; Mungu... ama amechaguliwa tangu zamani kupachukua mahali pake, kutukomboa sisi, kuyafanya mambo haya yote yawezekane.

Angalia, nje ya kuta zake zinazopendeza za Mji huu...

<sup>449</sup> Sasa mmeupata “ule Mji”? Mnaona, ni Mlima mtakatifu. [Ndugu Branham anaeleza kwenye ubao—Mh.] “Hakuna kitakachodhuru wala kuharibu katika Mlima Wangu wote mtakatifu, asema Bwana.” Huo Mji si miraba sita. Ni Mlima. Na ma—mapana kwa marefu na urefu wa kwenda juu, ni sawa, mnaona; maili elfu na mia tano kwenda *hivi*, maili elfu na mia tano kwenda *vile*, maili elfu na mia tano kuzunguka kote; na maili elfu na mia tano kwenda juu. Kwa hiyo ni Mlima mkuu tu, kama piramidi, nao ule Mji uko juu ya Mlima. Utukufu!

<sup>450</sup> Hivyo ndivyo ilivyo, hizo hapo paradiso za Mungu, Nuru ya ulimwengu, Ufalme ule mkamilifu. Si siku ya saba; ya Milele! Mnaona? Si Utawala wa Miaka Elfu; Nchi Mpya! Mnaona?

<sup>451</sup> Wakati inapopitia kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, inapitia kwenye hatua yake ya utakaso, bali ingali bado haina budi kutekekezwa. Mnaona? Ambapo, ile Damu iliwakomboa watu, inaonyesha kumbukumbu hii ya kwamba ni...gharama imelipwa, miaka hiyo elfu moja. Lakini basi haina budi kusafishwa kwa Moto; kama tu ilivyokuwa kwako wewe, raia Wake wa Mji huu, wale raia.

<sup>452</sup> Kwa hiyo kama ukifa ama ukiishi, kuna tofauti gani? Kama Yeye akija leo, ama aje miaka mia moja, ama miaka elfu, mimi nitapumzika tu mpaka kubadilishwa kwangu kuje.

<sup>453</sup> Kwa hiyo, mzee mwanamume na kizee mwanamke, msife moyo. [Ndugu Branham anaelezea ubaoni—Mh.] Kama wewe umewakilishwa *hana* juu, katika sifa hii ya Mungu; *hii*, Mungu; kama unayo, kama wewe umewakilishwa *hana* juu, katika sifa hii ya Mungu; *hii*, Mungu; kama unayo, kama wewe umewakilishwa *hana*, huwezi... Wewe uko katika Umilele. Na kama umevuka kutoka kwenye siku hiyo ya saba, ukaingia kwenye ya nane, umeingia katika ya Milele kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, umehusishwa katika *Hii*. Sasa, kama wewe unatumainia tu uamsho, ama kurukaruka juu, ama, "Ninafanya *hili*. Ninaadhimisha siku yangu ya saba. Mimi sili nyama," na mambo kama hayo, hayo yatakwisha, hata hivyo. Mnaona? Lakini *Hii* ni ya Milele. Mnaona? *Hii* ni ya Milele, ile sikukuu baada ya sikukuu ya vibanda. Unaona?

<sup>454</sup> Sikukuu ya vibanda ilikuwa ndiyo sikukuu ya mwisho, sikukuu ya saba. Sisi tunaabudu sasa chini ya sikukuu ya vibanda, wakati wa saba wa kanisa.

<sup>455</sup> Katika ule Utawala wa Miaka Elfu, tutakuwa chini ya sikukuu ya vibanda, tena, katika siku ya saba.

<sup>456</sup> Lakini, basi, baada ya siku saba, tuna Kusanyiko Takatifu, kurudi katika Umilele. Vipi? Kwa njia ya Yule wa Milele aliyekuja na kutukomboa na kuturudisha, katuacha tutambue kwamba sisi tu sehemu ya *Hili*.

<sup>457</sup> Sasa, unajuaje wewe u sehemu? Kwa sababu, Neno la wakati huu, ahadi ya siku hii. Ni kitu gani? Kurudishwa kwenye siku ya kwanza, ya kwanza. "Naye ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba *zao*," akileta kurejezwa tena kwa upentekoste halisi, si miamsho; na atadhahirisha Nuru ya jioni, Mwana yule yule aliyonekana katika Nuru ya asubuhi, kama ilivyoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Amina na amina!

<sup>458</sup> Tuko wapi, marafiki, tuko wapi? Tunangojea tu kuondoka njiani, kusudi Ufunuo 11 ininii... ijulikane kwa Wayahudi; hiyo ni kweli, kule Kunyakuliwa kunakokuja.

<sup>459</sup> Angalia, nje ya hiyo milango ya hizo kuta, yakiwa yametapakaa kila mahali katika Nchi Mpya, mataifa yataishi kwa amani Milele. Sasa ni nini? Wafalme wenye heshima wataleta utukufu wao ndani yake. Hakuna dhambi inayoweza kuwa kule. Hakuna tena wanawake waliokata nywele zao watakaoingia kwenye Mji huo. Nitawahakikishieni jambo hilo. Hakuna tena kuvaah kaptura, kuvuta sigara. Waasherati, makahaba, waongo, waabudu sanamu, cho chote walichokuwa, hawataingia Mji huo. La, yote yatakuwa yamekwisha. Dhambi itakuwa imeondolewa. "Hakuna kitu cha kuunajisi utakatifu wake kitakachoingia mle." Hivyo ndivyo alivyosema. "Yote yamepitaa, milele."

<sup>460</sup> Angalia kule kondeni mwake na kuzunguka malango yake:

Dubu atakuwa mpole, mbwa mwitu atakuwa mtulivu;  
 Na simba atalala pamoja na mwana-kondoo;  
 Na wanyama pori, wataongozwa na mtoto mchanga;  
 Nitabadilishwa kutoka kiumbe hiki nilicho mimi.

<sup>461</sup> Huku mauti haya yakifanya kazi katika mwili wangu upatikanao na mauti, uzee ukiingia, nitabadilishwa.

<sup>462</sup> Mmeusikia huo wimbo? "Dubu atakuwa mpole. Mbwa mwitu atakuwa mtulivu." Yeye hataruka, na kuinuka juu na kujaribu kukuua. Yeye atatembea pamoja nawe njiani.

Ni nani atakayeirithi? Walikombolewa. Itakuwa ni akina nani?

Angalia, ninaweza tu kufundisha mifano yangu sasa peke yake. Angalia, Ndugu Lee.

<sup>463</sup> Ni akina nani waliokuja kwenye nchi mpya pamoja na nabii Nuhu? Hao walioingia pamoja naye safinani. Hiyo ni kweli? Hao ndio wanaotoka na kutembea mle. Mnaona? Hao walioingia pamoja na Nuhu, kwa ujumbe wake, hao ndio waliotoka wakatembea juu ya nchi mpya baada ya ubatizo wake wa maji.

<sup>464</sup> Wale wanaoingia pamoja na Yesu sasa. Unaingaje ndani Yake? Kwa Roho Mmoja; Naye ni Neno. Unakuwa sehemu Yake. Wewe ni sehemu Yake ipi? Neno linaloishi la wakati huu, kutambua. Utatembea pamoja Naye katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Hapo ndipo utakapotoka ukatembee. Angalia, si kizazi kipyaa. Kupandikiza!

Unasema, "Loo! Ndugu Branham!" Loo!

<sup>465</sup> Angalia, kama Mungu aliweza kumwinua Eliya na kumchukua juu, miaka elfu mbili na mia tano iliyopita, akampandikiza duniani tena, apate kuwa nabii kwa Wayahudi, ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza kumfanyia Bibi-arusi!

<sup>466</sup> Baada ya Nuhu kutoka kwenye safina, angalia yale aliyaombiwa Nuhu baada ya kutoka kwenye ile gharika, kama tu ilivyokuwa Adamu hapo awali. Baada ya yeze kutokeea, juu ya nchi mpya; kasema, “Zaeni mkaongezeke, mkajaze nchi,” baada ya ile gharika. Angalia, “alikuwa aongezeke, akaijaze nchi,” kama Adamu mara ya kwanza.

Sasa mnawenza kuona vizuri hapa. Sasa sikilizeni kwa makini sana.

<sup>467</sup> Adamu alikuwa “aongezeke akaijaze nchi.” Hiyo ni kweli? Nuhu alikuwa, baada ya ule mpya, (ulimwengu kuangamizwa), alikuwa “aongezeke akaijaze nchi.” Mnalipata? Sasa hamwezi kuona “uzao” wa nyoka ni kitu gani? Ni kitu gani kilijaza nchi? Mnalipata? Vema. Mnaona jinsi Shetani alivyompata Hawa sasa. Hiyo ndiyo sababu mauti yameitawala nchi tangu wakati huo. Na mbingu, nchi, mnyama, anga, vyote vimelaaniwa na Mungu kwa ajili yake. Hilo ndilo laana, kwa sababu Shetani alimfikia huyu wa kwanza.

<sup>468</sup> Yesu alikuja kuikomboa airudishe kwa Baba. Ili apate kufanya jambo hili, Yeye akawa sehemu yake; kama nilivyoeleza hivi punde. Na kutokana na vumbi lilo hilo (ile sehemu aliyokuwa Yesu, Mwenyewe) ikikombolewa, kupitia Kwake sifa zote za Mungu zinakombolewa pamoja na dunia.

<sup>469</sup> Yeye alikuwa Neno lililonenwa. Sisi ambao tumekombolewa ni sehemu Yake. Ndipo, laiti ungaliweza kutambua! Unaona?

<sup>470</sup> Mafarisayo walidai walikuwa hivyo. Lakini, mnaona maelezo yangu ya kwanza, walikuwa hivyo tu kiakili. Wao hawakuweza kulitambua Neno wakati lilipodhihirishwa moja kwa moja mbele yao. Wao walisema, “Mtu huyu ni pepo mchafu.”

<sup>471</sup> Sasa, leo, tunaitwa manabii wa uongo. Tunaitwa kila kitu kichafu tunachowenza kuitwa, na watu wa dini, mnaona, na watu mashuhuri na wenye akili nyingi. Mnaona, wao tu hawafahamu. Mnaona?

<sup>472</sup> Ubatizo wake wa maji haukutosha kuisafisha; wala wa kwao. Utakaso, wa Damu, uliirudisha, ukaidai. Bali ubatizo wa Moto uliisafisha; kama ulivyomfanyia Bibi-arusi Wake. Kama vile kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

<sup>473</sup> Hakuahidi kamwe kuinua jamii mpya, kama nilivokwisha kusema, bali Yeye aliahidi kuwakomboa walioanguka. Hao walio—waliochaguliwa tangu zamani, watairithi kama Yeye alivyokwisha kuahidi. Naye ni Mungu asiyebadilika; tunajua jambo hilo.

<sup>474</sup> Kumbukeni, Mungu alimchukua Eliya, baada ya kunyakuliwa, na kumhamisha, akampandikiza akamrudisha kwa watu, kuchukua nafasi kama nabii kati ya watu wake; hivi

karibuni sana atafanya jambo hilo. Naye amemweka, akiwa hai, miaka hii elfu mbili na mia tano. Yeye atatokeea tena.

<sup>475</sup> Angalieni tena, Yeye alimfufua Musa katika wafu. Kaburi lake liko wapi? Kuna mtu ye yote anayeweza kulipata? Soma Kitabu cha Yuda. Mnaona? Shetani... Yule Malaika Mkuu akihojiana na malaika mkuu, Shetani, alisema, ninii... "Bwana na akukemee," wakihojiana kwa ajili ya mwili wa Musa. Na hapa Petro, Yakobo na Yohana walikuwa wamesimama pale wanamwangalia, juu ya Mlima wa Kugeuzwa Sura, pale pale ambapo ule Mlima utakapoinuliwa kuishi ndani yake. Mnaona?

Naye akaja kuikomboa.

<sup>476</sup> Mnaona, kulikuweko na Kanisa lililonyakuliwa wakati huo, limewakilishwa; kulikuweko na hao waliolala, walowakilishwa. Wapi? [Ndugu Branham anaelezea ubaoni, katika aya chache zifuatazo—Mh.] Katika ule Mji; kule juu mlimani. Mnaona?

<sup>477</sup> Kulikuweko na Petro, Yakobo, na Yohana, wakiangalia; watatu, ushuhuda. Kulikuweko na Eliya, Musa, na Yesu; kama ushuhuda wa Mbinguni. Mnaona?

<sup>478</sup> Na kulikuweko na Musa, waliokufa, waliokufa, wamekwisha kufufuliwa. Kulikuweko na Eliya, kule kunyakuliwa, alikuwa angali hai. Nao wote wawili walikuwa wamewakilishwa kwenye mlima huu mtakatifu.

<sup>479</sup> Na, Yesu, Mkombozi. Wakati Mungu, huko juu Yake namna *hii*, alipomtia Yeye uvuli, alisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu."

<sup>480</sup> Kumbukeni, Yesu alisema, yapata siku moja kabla ya wakati huo, alisema, "Amini nawaambieni, ya kwamba wengine wanaosimama hapa sasa, hawataona mauti, mpaka watakapouona Ufalme wa Mungu umesimamishwa katika nguvu."

<sup>481</sup> Ilikuwa ni nini? Wafu waliofufuliwa na watakatifu walionyakuliwa, pamoja, wakinyakuliwa pamoja kumlaki Yeye hewani. Huku Mungu akimtia Yeye uvuli, na Yesu akisimama pale katika kivuli hiki, akisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye," utaratibu wa ule Ufalme Mpya. Loo! ndugu, dada!

<sup>482</sup> Mauti hayakubadilishi. Mauti hubadilisha tu mako yako. Unaona?

<sup>483</sup> Kumbuka, Samweli, alipokuwa amekufa na amezikwa kwa miaka miwili, yeye alikuwa Paradiso. Naye mchawi wa Endori akamwitwa, naye Sauli akamtambua; na mwanamke huyo akamtambua, pia, na akaanguka kifudifudi. Yeye hakuwa amebadilika, hata kidogo. Yeye alikuwa akali Samweli yule yule, baada ya kufa miaka miwili, na alikuwa angali ni nabii. Akasema, "Kesho utaanguka vitani, wewe pamoja na mwanaao,

na wakati kama huu kesho usiku utakuwa pamoja nami.” Na hilo ndilo lilitotukia hasa.

<sup>484</sup> Mnaona? Na wakati Musa atakaporudi, na Eliya, kwa ajili ya Ufunuo 11, wao wangali watakuwa manabii. Haleluya! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.]

<sup>485</sup> Na kule ng’ambo, Nchini, ule Mji ambamo Mwana-Kondoo ndiye Nuru, nitakuja wewe, Ndugu McKinney. Nitawajua ninyi, watu wangu, enyi vito vyangu kwenye taji. Watakapokuja kutoka Mashariki na Magharibi, kwenye ule Mji; wakati kwenye maili elfu moja na mia tano mraba, utakuwa umekaa pale, na ule Mji uliojengwa mraba. Mtakapokuwa mmekeeti kule kwenye ule Mlima mtakatifu, ambapo Mungu anaketi juu ya ule Mlima, na Yesu kwenye Kiti cha Enzi. Na ile baragumu ya dhahabu inalia wakati Yusufu anaondoka, na kutembea chini katika Paradiso, na watoto wa Mungu wanapiga magoti na kumwabudu Yeye, wakijua ya kwamba wao walikombolewa. Mnaona? Amina! Haleluya!

Wakati mwingine ninatamani Mbinguni sana,  
Na utukufu nikakaouona kule;  
Itakuwa furaha jinsi gani wakati  
nitakapomwona Mwokozi wangu,  
Katika ule Mji mzuri wa dhahabu!  
Ninalekeea kwenye Mji huo mzuri  
Aliouandaa Bwana  
[Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>486</sup> Isaya alisema, katika Isaya 9:6, “Na amani Yake na maongeo Yake hayatakuwa na mwisho. Úweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake; Naye ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Na uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake; na maongeo Yake na amani Yake havina mwisho.” Hata wanyama wako kule. Loo, jamani!

Dubu atakuwa mpole, na mbwa mwitu  
atakuwa mtulivu;  
Na simba atalala pamoja na mwana-kondoo;  
Na mnyama pori, ataongozwa na mtoto  
mchanga;  
Lakini nitabadilishwa.

<sup>487</sup> Nitabadilishwa kutoka kiumbe hiki mimi niliye, Siku hiyo itakapokuja, kwa maana ninalekeea kwenye Mji ule. Ninalekeea kwenye Mji ule mzuri! Ninahisi zile Nguvu za ukombozi katika moyo wangu wote sasa.

<sup>488</sup> Kama hivi sivyo ilivyo, basi nimepoteza maisha yangu; nimewafundisha wengine mambo ya udanganyifu. Lakini ninapotazama chini na kuona ya kwamba ile ahadi aliyoiweka ya siku hii, na kuionna Hiyo ikidhihirishwa; na kuangalia kusanyiko hili la maili elfu moja na mia tano mraba limeketi hapa, wateule ambaa wameitwa kutoka katika madhehebu na jamii

na kanuni za imani na kadhalika, wamekusanyika pamoja; huku nikiona Neno likijidhihirisha Lenyewe, ninajua, bila shaka hata kidogo, vito yya taji yangu vitang'aa kuliko kitu cho chote kile ulimwenguni, katika Siku ile.

<sup>489</sup> Utafika wakati! Enyi watu, hatukusanyiki hapa bure. Tunaungojea tu wakati ule. Muda umeenda sana, sana, bali Yesu yungali karibu, karibu sana. Na, Utukufu Wake, ni mzuri sana. "Jina Lake ataitwa Mshauri." Ule Mji, mnaweza kuuona? Huko ndiko Bibi-arusi na Bwana Arusi watakakokaa, wala hawataninii tena . . .

<sup>490</sup> Sasa, kama unafikiri ni vizuri sana tunapoendesha maili mia kadha ili kuketi hapa na kulishwa Neno Lake, ambapo hiki ni kivuli tu, itakuwaje tutakapoishi kwenye ule Mji pamoja Naye! Nitakapokuwa jirani yako wa karibu, na tutakapokula hiyo miti, na tutakapotembea kwenye barabara hizo, tutakapotembea kwenye barabara hizo za dhahabu kwenye chemchemi, kunywa kutoka kwenye chemchemi, kutembea katika paradiso za Mungu, huku Malaika wanarukaruka kuizunguka dunia, wakiimba nyimbo za sifa, loo, itakuwa ni Siku ya namna gani! Inastahili kwa vyote. Njia inaonekana inaparuza, wakati mwingine inakuwa ngumu, lakini, loo! itakuwa kitu kidogo sana nitakapomwona Yeye, kidogo sana. Vipi yale majina mabaya na mambo ambayo wao wamesema, hayo yatakuwa nini nitakapomwona Yeye katika Mji ule mzuri, mzuri sana wa Mungu?

<sup>491</sup> Na tuinamishe vichwa vyetu.

Ninaelekea kwenye Mji mzuri  
Bwana wangu ameuandalia walio Wake;  
Wakati wote Waliokombolewa wa nyakati zote  
Wataimba "Utukufu!" wakikizunguka Kiti  
Cheupe cha Enzi.

Wakati mwingine ninatamani Mbinguni sana,  
Na utukufu wake nitakaouona kule:  
Itakuwa ni furaha jinsi gani nitakapomwona  
Mwokozi wangu,  
Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

<sup>492</sup> Kwenye kisiwa cha Patimo, Yohana aliuona! [Ndugu Branham analia kwa furaha—Mh.]

<sup>493</sup> Yesu mpenzi, tumaini hili, tumaini langu halijajengwa juu ya kitu kingine, Bwana. Huo ndio mama wa moyo wangu; Mji huo, yule Mfalme mkuu. Mungu, usimwache mmoja hapa aangamie, tafadhalii. Jalia tuyachunguze maisha yetu tena, leo, Bwana, tukikungojea kule Kuja kwa Bwana. Ambapo, wote Waliokombolewa, huko nje kwenye ule uwanja mkubwa wa michezo huko Roma, ambapo hao Wakristo waliliwa na simba, mavumbi yatapasuka siku moja!

<sup>494</sup> Hakutakuwako na makaburi kwenye mimba ya kile kilima cha Utukufu. Hakuna vitasa vyta mlango vitakavyoshikilia shada la maua ya mazishi. Hakuna chozi litakaloanguka mle. La, la. Hakuna kichuguu cha udongo kitakacholundikwa mle. Hakuna tufani itakayoupiga. Yote itakuwa ni utukufu kule.

<sup>495</sup> Tusaidie, Bwana. Kama kuna mmoja hapa...ambaye amekwisha itwa kwenye Karamu hii ya Arusi ya Mwana-Kondoo, miaka hii elfu moja ya Utawala wa Miaka Elfu, kisha kuingia kwenye ule Mji baada ya Fungate kwisha. Ule Utawala wa Miaka Elfu ni Fungate tu. Halafu Yeye, Bibi-arusi, atachukua nanii Wake...Bwana Arusi atampeleka Bibi-arusi Wake Nyumbani. Ni Wake. Bwana Arusi Wake; Bibi-arusi Wake. Loo! Yeye ameenda kuandaa Nyumba, tangu alipomposa.

<sup>496</sup> Jalia tuwe waaminifu Kwake Yeye Ambaye ni Neno, kwa kuwa Yeye ni Neno. Haidhuru wengine wanajaribu kututusi namna gani, kutuweka mbali na Huo; Bwana, nisogeze karibu.

Kwa kuwa wakati mwingine ninatamani  
Mbinguni sana,  
Na utukufu wake nitakaouona kule:  
Itakuwa ni furaha jinsi gani nitakapomwona  
Mwokozi wangu,  
Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

<sup>497</sup> Makao ya Baadaye ya Bwana Arusi na Bibi-arusi! Yeye anarudi...[Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...kwenye Karamu Ya Arusi; itakuwa siku tatu na nusu. Kisha turudi tena, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwenye fungate yetu. Na halafu Yeye—Yeye ataunyesha wazi ule Mji. Kama bwana arusi anavyomshusha bibi-arusi, jinsi maskini bibi-arusi huyo anavyosimama akiangalia makao yake ya baadaye kwa mshagao mkubwa! Na kwa imani, leo, Bwana, tunauona kule ng'ambo. Utakuwa papa hapa duniani. Wewe uliahidi jambo hilo.

<sup>498</sup> Kanisa Lako litakombolewa kabisa, moja ya siku hizi. Halafu ulimwengu Wako utakombolewa, vitu vingine vyote. Lakini kwanza umewakomboa watu Wako, miili yao iliyofanyizwa kutokana na ulimwengu.

<sup>499</sup> Tusaidie, Mungu. Kama kuna mmoja hapa ambaye hana hakika kabisa ya jambo hilo, Bwana, naomba walipokee sasa hivi.

<sup>500</sup> Ninajua nimechukua muda mrefu na kumekuwa na joto, lakini, enyi watu, hatutakuwa daima tumesimama hapa. Mimi sitakuwa daima mchungaji wenu. Hebu tulihakikishe.

“Hivi kuna njia, Ndugu Branham?”

<sup>501</sup> Naam, wewe kuwa sehemu ya Neno, sehemu ya Neno la siku hizi. Huwezi kuwa sehemu ya Neno la siku ya Musa; sehemu hiyo imekamilika tayari, hiyo ilikuwa ni miguu. Tuko kwenye kichwa sasa. Hiki ni Kristo. Si ule wakati wa mikono, kule nyuma katika

Luther, la. Huu ni wakati wa Kichwa. Kristo, Jiwe la Kifuniko, anakuja kwenye ule Mwili.

<sup>502</sup> Kama hujisikii sawa kabisa juu ya jambo hilo, po pote uwezapo, tafadhali inua mkono wako ili niweze kuona. Hebu kila mtu mwingine ainamishe kichwa chake. Mungu awabariki.

<sup>503</sup> Sema, “Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham. Ninataka sana kuwepo huko! Si—sitaki kupakosa mahali pale, Ndugu Branham. Ni—ninachunguza, ninafanya kila niwezalo, lakini niombee sasa, tafadhali?” Mungu awabariki.

<sup>504</sup> Huku ukiwazia juu ya jambo hilo sasa, omba tu, useme, Mungu . . .” Liko moyoni mwako. Angalia, kama unasikia kitu fulani kikivuta, kikiuwasha moyo wako, hicho ndicho. Ni sifa ile ikijaribu kujitangaza.

Ninaelekea kwenye Mji ule mzuri  
Bwana wangu ameuandaa kwa walio Wake;  
Wakati wote Waliokombolewa wa nyakati zote  
Wataimba “Utukufu!” wakikizunguka Kiti  
Cheupe cha Enzi.

Wakati mwingine ninatamani Mbinguni sana,  
Na utukufu nitakaouona kule:  
Itakuwa ni furaha jinsi gani nitakapomwona  
Mwokozi wangu,  
Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

<sup>505</sup> Baba wa Mbinguni, tuchukue sasa, Bwana. Jalia yule Mchungaji Mkuu, yule Mchungaji Mkuu Anayekomboa, yule Mchungaji Mkuu Ambaye aliacha Utukufu, akijua ya kwamba baadhi ya zile sifa zilikuwa zimepotea katika yale mambonde makubwa ya dhambi, ambako mbwa mwitu na wale—wale wanyama karibu wangemla maskini kondoo yule; bali Yeye aliacha zile kumbi za dhahabu, akashuka akaja duniani na akawa mmoja wetu, kusudi apate kuutangaza upendo wa Mugu kwetu. Pale akawakuta, baadhi yao wakiwa kwenye madhehebu, baadhi yao katika nyumba za malaya, baadhi yao mitaani, vifofu, baadhi yao kwenye vifungo na kwenye njia kuu, bali Yeye alimkomboea kila mmoja ambaye Baba alikuwa amemchagua Yeye amkomboe.

<sup>506</sup> Naye alituagiza, ya kwamba tungeishi sehemu hii ya Neno kwa nyakati zetu. Nasi tunaona yale matengenezo makuu ya Luther, katika wakati ule; na ya Wesley; na ya Pentekoste. Sasa tunalitazamia lile Jiwe la Kifuniko cha ule Mji. Ee Mungu, tunajua wakati na ahadi ambayo tumepewa kwa ajili ya siku hii, jinsi ambavyo Hili litarudishwa tena. “Nuru ya Jioni itaivisha tunda lake. Na itakuwa ya kwamba kutakuwa na siku ambayo haiwezi kuwa ni mchana wala usiku, inayoweza kuitwa hivyo, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.”

<sup>507</sup> Mwana yule yule wa Mungu aliyetukuka, akijidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu hapa duniani,

akiifanya ile ahadi iishi yenewe kabisa, aliyapofusha macho ya Mafarisayo na Masadukayo na Maherodi, na kadhalika.

<sup>508</sup> Na leo hii jambo hilo linajirudia tena, Neno likidhihirishwa kama tu liliyokuwa. Neno, kujua siri za moyo, kama tu vile ilivyokuwa hasa, kama Maandiko yalivyosema, ambayo hayawezi kutanguka. Tusaidie, Mungu, kutambua jambo hilo.

<sup>509</sup> Wasaidie hawa sasa walioinua mikono yao. Jalia wakaze mshipi zaidi kidogo; wavae Injili ya Amani; wavae silaha zote za Mungu; washushe chapeo chini; wachukue ngao ya imani; waende mbele, tangu leo na kuendelea. Tujalie, Bwana.

<sup>510</sup> Muda kidogo tu, tutaitwa, kisha Kunyakuliwa kutakuja. Kundi dogo sana tu, kama Henoko, litanyakuliwa.

<sup>511</sup> Halafu, “wazao waliosalaia wa yule mwanamke, wazishikao amri za Mungu,” Wayahudi, “wenye ushuhuda wa Yesu Kristo,” Mataifa, watasakwa kama mbwa, “nao watatoa maisha yao kwa ajili ya ushuhuda wao.”

<sup>512</sup> Halafu, asubuhi moja kubwa, kupambazuka kwa ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa ajili ya ile—ile Fungate kutaanza.

<sup>513</sup> “Ndipo hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.” Ndipo, baada ya ile miaka elfu, kulikuwako na Hukumu, ikionyesha ya kwamba Hamu alikuwa kwenye safina. Naye Hamu yungali pale katika wale waliosalia. Wale waliolisikia na kulikataa itawabidi kuhukumiwa.

<sup>514</sup> Sasa, tujalie, Bwana, ili kwamba tusihesabiwe mionganoni mwao, bali tutaitwa kwenye ile Karamu ya Arusi. Kwa kuwa, tunamtambua Yesu mionganoni mwetu leo. Tunaingia pamoja Naye; kutoka ulimwenguni, tuingie ndani Yake. Hebu tutembee katika Mji huo, tutoke pamoja Naye.

<sup>515</sup> Ninazeeka, Bwana. Sina mahubiri mengi zaidi ya kuhubiri. Bali bila shaka nakutumaini Wewe. Mimi ninautazamia Mji ule, kama alivyofanya baba yangu Ibrahimu. Kuna Kitu ndani yangu kinachoniambia unakuja. Ninajaribu kila mahali, Bwana, kueneza Nuru na kuwaita. Jalia hata mmoja wa hawa, Bwana . . .

<sup>516</sup> Jinsi ulivyonifunulia jambo hilo vizuri sana, muda mfupi uliopita. Kutoka mzingo wa kama maili elfu moja na mia tano, mmoja tu *hapa* na *mwinge pale*, wameketi pamoja leo, waliokusanyika katika mahali pamoja padogo, wakiungojea Mji ule utokee. Tunakiri ya kwamba sisi ni wasfiri na wageni. Sisi ni waliotupwa. Makafiri, ulimwengu, hucheka na kufanya mizaha; madhehebu ya kidini hucheka; bali sisi hatutikiswi na mambo kama hayo. Tufanye sehemu ya Neno, Bwana, wasiotikiswa. “Itakuwa katika siku za mwisho.” Na iwe ni sisi, Bwana, jalia tuhesabiwe mionganoni mwao. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>517</sup> [Ndugu Branham anatalia kidogo—Mh.] Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Na tuinamishe vichwa vyetu namna *hii*.

Ninaelekea kwenye Mji ule  
 Bwana wangu ameuandaa kwa walio Wake;  
 Wakati wote Waliokombolewa wa nyakati zote  
 Wataimba “Utukufu!” wakikizunguka Kiti  
 Cheupe cha Enzi.

Wakati mwingine ninatamani Mbinguni sana,  
 Na utukufu wake nitakaouona kule;  
 Loo! itakuwa furaha jinsi gani  
 nitakapomwona Mwokozi wangu,  
 Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

<sup>518</sup> Sasa, kama itatubidi kuishi katika Mji huo pamoja, peana tu mkono na mtu fulani, useme, “Mungu akubariki, msafiri. Umetoka wapi? Louisiana, Georgia, Mississippi? Mimi ni msafiri, pia. Ninautazamia Mji ule.”

<sup>519</sup> Ninautazamia Mji ule, Ndugu Neville. Ninaenda kule . . . ? . . . Amina. Ndugu Capps, mimi ninautazamia Mji ule, bado, usiku wa leo. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Hakuna Uchungu*—Mh.]

Na utukufu wake nitakaouona kule:  
 Itakuwa ni furaha ya namna gani  
 nitakapomwona Mwokozi wangu,  
 Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

Loo, dubu atakuwa mpole, na mbwa mwitu  
 atakuwa mtulivu;  
 Na simba atalala pamoja na mwana-kondoo,  
 loo, naam;  
 Na mnyama pori kutoka . . . , wataongozwa na  
 mtoto;  
 Nami nitabadilishwa kutoka kiumbe mimi  
 niliye, loo! naam.

Loo! kutakuwa na amani kule bondeni kwa  
 ajili yangu siku moja;  
 Loo! kutakuwa na amani kule bondeni kwa  
 ajili yangu. (Kweli! Naam!)  
 Hakutakuwa na huzuni tena, hakuna majonzi  
 tena, sitaona shida tena;  
 Na kutakuwa na amani huko bondeni kwa ajili  
 yangu.

<sup>520</sup> Mfalme wetu asiyeonekana, asubuhi ya leo, atadhihirishwa. Nami sitamwangalia Bill Dauch kwenye umri wa miaka tisini. Hutaniangalia mimi kwenye umri wa miaka hamsini. Lakini nitabadilishwa, Siku hiyo.

Na wakati mnyama wa msituni, ataongozwa na mtoto;  
 Lakini nitabadilishwa, kubadilishwa kutoka kiumbe hiki nilicho mimi.

<sup>521</sup> Je! wewe hutafurahi? Nywele zenyе mvi zitakwisha; mabega yaliyoinama. Lakini uzuri, usiopatikana na mauti, tutasimama katika mfano Wake, tuking'aa kuliko juu. Loo, inapendeza sana!

. . . kwa ajili yangu, Ee, Bwana, naomba;  
 Hakutakuwa na huzuni, hakuna majonzi tena,  
 sitaona shida;  
 Na kutakuwa na amani huko bondeni kwa ajili  
 yangu.

<sup>522</sup> Hilo ndilo lilitoluteletu hapa. Ni wangapi wenu wanaohitaji nguvu kwa ajili ya safari? Mungu na atujalie jambo hilo! Ni wangapi wenu walio wagonjwa mwilini mwenu, askari waliojeruhiwa? Dazani, ama zaidi. Mnaamini Yeye yuko hapa, yule Mfalme asiyeonekana? Vitu vionekanavyo; visivyoonekana hudhihirishwa na vinavyoonekana. Ni yeze yule jana, leo, na hata milele, ila tu mwili wa nyama. Sasa, kama huyu ni Roho Wake mbaye amehubiri hili kuitia kwangu, Yeye atafanya kazi alizozifanya alipokuwa hapa. Loo! ni jambo zuri namna gani!

Ninaelekeea katika nchi ya ahadi,  
 Ninaelekeea katika nchi ya ahadi;  
 Loo! ni nani atakayekuja aende pamoja nami?  
 Ninaelekeea kwenye nchi ya ahadi.

Kote kwenye nyanda hizo pana  
 Inang'aa Siku moja ya Milele;  
 Huko Mungu Mwana anatawala milele,  
 Na kuutawanya usiku.

Loo! ninaelekeea kwenye nchi ya ahadi,  
 Ninaelekeea kwenye nchi ya ahadi;  
 Loo! ni nani atakayekuja aende pamoja nami?  
 Ninaelekeea kwenye nchi ya ahadi.

<sup>523</sup> Watu mia tano wakienda mtoni kule, siku ya kwanza ambapo yule Malaika wa Bwana alipoonekana kwa macho, kuthibitisha, kama alivyofanya kwenye Mlima Sinai, ya kwamba nilikuwa nimekutana Naye. Nilitembea kuingia mtoni, na mamia wakiimba wimbo uo huo kwa ajili ya ubatizo. Huyu hapa anakuja, akishuka, Nguzo ile ile ya Moto mnayoona kwenye picha pale; ikishuka chini, papa hapa mtoni, na kusema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza, Ujumbe huu utakutangulia Kuja kwa pili." Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo, mnaona.

Loo, ni nani atakayekuja aende pamoja nami?  
 Ninaelekeea kwenye nchi ya ahadi.

<sup>524</sup> Nguzo ile ile ya Moto iko hapa pamoja nasi. Mnatambua hilo? Yeye amewafanya wengine wetu kwa ajili ya kitu kimoja, na wengine kingine. Kama mkiweza, bila tashwishi moja, kuamini ya kwamba Yeye yuko katikati ya hili jengo, ninaamini atajithibitisha Mwenyewe kwenu. Itawaridhisha? Kama sitamfikia kila mmoja... Inaelekea sasa nane, lakini kama... Kidogo imepita saa saba, hasa. Kama mtaamini, hebu Yeye na ashuke juu yetu! Imani yetu iko wapi? Mnaona, hamna budi kuamini jambo hilo. Kama hutalitilia shaka, hata kidogo, litatenda kazi.

<sup>525</sup> Mimi—mimi ninatambua Uwepo wa Mungu wa Utu wa Kristo, Ambaye ni Neno. Nayo Biblia ilisema, “Neno ni... lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, nalo linakata viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, na hutambua mawaza yaliyo—yaliyo moyoni, likifunua siri ya moyo.”

<sup>526</sup> Angalia. Mbona, mimi sikujua mambo haya, miaka kadha iliyopita. Na wakati niliposema jambo hilo, bila kulijua, angalieni jambo alilofanya. Yeye alisema, “Sasa utawashika watu mkono, na, usiwazie lo lote, nena tu sifa utakayoambiwa. Useme ni kivimbe, cho chote kile.” Kisha akasema, “Itakuja kutokea ya kwamba haitakubidi kufanya jambo hilo.” Mnaona? Mnaona? “Itatambua kitu kile hasa kilicho ndani yao.” Tuna kila aina ya miigo, tunajua jambo hilo, karibu iwapoteze walio Wateule kama yamkini. Angalia jinsi jambo hilo lingine linavyoambatana na Neno, ndipo utajua kama ni kweli ama si kweli. Lakini, hata hivyo, Yesu anadumu yeye yule jana, leo, na hata milele.

<sup>527</sup> Ni wangapi walio hapa ambao ni wagonjwa, nanyi mnajua siwajui? Inua mkono wako, useme, “Na—najua hunijui mimi.” Loo, ni tu, ninakisua, kila mahali. Jambo tu likupasalo kufanya ni kuamini tu.

Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu;  
Amini tu, amini tu,  
Yote yatendeka, amini tu.

<sup>528</sup> Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa juu ya nchi katika siku ya mwisho. Wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa, ama, atakapo jifunua Mwenyewe katika siku ya mwisho.” Sasa, si katika siku za zamani, siku za katikati; siku ya mwisho, mnaona, Yeye angefunua. Na sasa tuko katika siku za mwisho. Sodoma inakaa vile kabisa, kila kitu, wale wajumbe, vile kabisa.

<sup>529</sup> Ilikuwaje kwa—kwa wale wachache waliosalia walioitwa watoke pamoja na kundi la Ibrahim? Kuna Mmoja aliye kujua kati yao, katika mwili wa kibinadamu; aliywakilishwa katika mwili wa kibinadamu, akila pamoja nao, akinywa pamoja

nao, chakula kile kile walichokula, kila kitu. Yeye alisimama mionganoni mwao, akawaambia Ujumbe. Kisha akasema, "Nitafanya kitu hiki kikuu."

<sup>530</sup> Naye Ibrahimu akaendelea kuchunguza, "Huyu ndiye? Nimekuwa nikiutazamia Mji. Huyu ndiye Mfalme wake?"

<sup>531</sup> Naye akasema, "Kwa nini Sara akatilia jambo hili shaka?" Hemani, nyuma Yake.

<sup>532</sup> Ibrahimu akasema, "Bwana Mungu, Elohim!" Maana, Yeye alitambua mawazo ya Sara.

<sup>533</sup> Yesu alisema ingerudia tena wakati Yeye angefunuliwa katika siku ya mwisho, lile Jiwe la Kifuniko likija kwenye ule Mwili. Kuwakomboa ninii... Hao ni wale Waliokombolewa, akija kuwachukua Walio Wake. Yeye yuko hapa pamoja nasi.

<sup>534</sup> Sasa, kuna kama dazani ya mikono tu, ama zaidi, iliyoinuliwa. Ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kumponya kila mmoja wenu. Kweli. Ninaamini ndivyo mlivyo. Siamini ya kwamba mtu kweli angeweza kuketi mahali kama hapa bila... katika wakati wa namna hii, na hali ya namna hii, bila ya kujua, kutambua kitu fulani.

<sup>535</sup> Ninawataka mwombe. Ninataka mjue shida yenu, katika—katika—moyo wenu, unaona, kisha uanzze kuomba, useme, "Bwana Yesu, nifunulie jambo hili. Nina—ninakuzungumzia Wewe shida yangu. Na sasa mtume Roho Wako Mtakatifu kwa Ndugu Branham, apate kutimiza kile alicho sema kuwa ni Kweli, katika Ujumbe huu ambao amenena habari zake leo kuhusu Wewe, ninajua ya kwamba itakuwa ni Kweli. Sasa, nifunulie jambo hilo, Bwana. Sema nami."

<sup>536</sup> Sasa limetawanywa, kwa namna fulani hapa na kila mahali. Kwa hiyo ombeni tu, na aminini tu kwa moyo wenu wote, ya kwamba Mungu atalijalia jambo hilo. [Ndugu Branham anatalilia kidogo—Mh.]

<sup>537</sup> Sasa nawatakeni mniangalie, na kuomba. Kama tu vile Petro na Yohana walivyosema, "Tutazame sisi." Yeye alitaka kitu fulani, naye yuko tu karibu kukipata. Nawe unataka kitu fulani, nami ninaamini uko karibu tu kukipata. Yeye alisema, "Tutazame sisi."

<sup>538</sup> Akasema, "Mimi sina dhahabu, wala fedha sina; lakini nilicho nacho, ndicho nikupacho."

<sup>539</sup> Sasa, kuponya, sina ko kote. Huko kote kuko katika Kristo. Lakini nilicho nacho, karama ya Mungu, ndicho niwapacho, imani ya kumwamini Yeye. Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wenu na aponywe. Aminini jambo hilo. Mnaona? "Kama mnawenza kuamini!"

<sup>540</sup> Maskini mwanamke anayeketi pale, akiniangalia. Yeye alikuwa analia, dakika chache zilizopita, akiomba. Yeye anaumwa kikoromeo ambacho kinamsumbia. Sikui mimi.

Wewe ni mgeni kwangu. Hilo ni kweli, sivyo. [Yule anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Wewe hutoki hapa. Umetoka Chicago. Bibi Alexander. Kama jambo hilo ni kweli, punga mkono wako. Sasa rudi Chicago uwe mzima.

<sup>541</sup> Yeye aligusa nini? Kitu kile kile mwanamke yule aliyekuwa na kutokwa na damu alichogusa, upindo wa nguo Yake, si yangu.

<sup>542</sup> Hapa yupo maskini bibi anayeketi papa hapa chini mionganoni mwa umati, kama ninaweza kumfanya anielewe mimi. Wewe uliyeinua kichwa chako upande. Sikuju. Wewe ni mgeni kwangu, bali una ugonjwa wa tumbo. Mumeo anaketi karibu nawe. Yeye ana kasoro kwenye sikio lake. Jina Lako ni Czap. Siwajui. Hamtoki hapa. Mmetokea Michigan. Kama hiyo ni kweli, pungeni mikono yenu. Rudini Michigan, wazima. Imani yenu inawaponya. "Ukiweza kuamini, yote yawezekana."

<sup>543</sup> Maskini bibi huyo pale mwenye ugonjwa wa koo, anayeketi papa hapa nyuma kule mwisho, kutoka Georgia, amevaa nguo nyeupe. Rudi, kule Georgia, ukiwa mzima. Yesu Kristo anakuponya. Unaamini jambo hilo?

<sup>544</sup> Bibi anayeketi pale, anayenitazama, mwisho kabisa wa kile kit. Yeye ana ugonjwa wa vimelea puan. Ataamini hayo, Mungu atamponya. Bibi Brown, amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakufanya... Sikuju, bali Yeye anakujua. A-ha. Unaamini jambo hilo? Inua mkono wako. Hiyo ni kweli.

<sup>545</sup> Anayeketi hapa kwenye machela haya. Mwambie aangalie huku. Amekuwa anaugua, akiendelea. Kama ningaliweza kumponya, ningefanya hivyo, bwana. Siwezi kuponya. Yeye si wa hapa; anatoka mbali sana. Umetoka Missouri. Ugonjwa wako uko ndani. Bali kama utaamini kwa moyo wako wote, wala usitilie shaka, Yesu Kristo anaweza kukuponya nawe unaweza kurudi Missouri, mzima, na kutoa ushuhuda wako. Unaamini jambo hilo? Basi likubali, kisha uchukue kitanda chako uende nyumbani. Yesu Kristo anakuponya.

<sup>546</sup> Unaamini? Huo ni utambulisho wa Uwepo wa Mfalme wa Milele. Mnaamini jambo hilo sasa, kwa moyo wenu wote? Sasa, bila shaka Yeye amefanya duara, kulizunguka jengo hili kabisa. Mnaamini jambo hilo kwa moyo wenu wote? Mnaamini mko katika Uwepo Wake?

<sup>547</sup> Sasa, unaamini na kukubali ya kwamba wewe ni mmoja wa raia wa Ufalme huu? Inua mkono wako. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sisi ni sisi kwa sisi; wewe ni sehemu yangu, mimi ni sehemu yako; sisi sote ni sehemu ya Kriso. Sasa, pamoa, na tuwekeane mikono sisi kwa sisi.

<sup>548</sup> Papa hapa, mwanamke aliyekuwa kwenye kitanda ameamka, anatembeatembea, anarudi nyumbani akawe na afya. Amina.

<sup>549</sup> Ninyi, kila mmoja, ameponywa, kama mtaamini. Sasa Wekeaneni mikono, nanyi ni sehemu hii ya Kristo. Sasa ombea mtu uliyemwekea mikono, jisi tu unavyotaka.

<sup>550</sup> Bwana Yesu, tunakutambua Wewe hapa. Wewe ni Mfalme wetu; Wewe unajitambulisha Mwenyewe kati Yetu. Tunakushukuru kwa ajili ya Uwepo huu. Na, Bwana, Wewe ulisema, "Mkiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' usilililie shaka jambo hilo; uamini ulilosema litatimia, linaweza kuwa lako, ulilosema linaweza kuwa lako."

<sup>551</sup> Kwa hiyo, katika kutii amri hii, katika kulitii Neno la Mungu ambalo haliwezi kushindwa, sisi kama raia Wako kutoka maili elfu moja na mia tano mraba, kama ule Mji, tunawambia Shetani, ibilisi aliyeshindwa, "Mwisho wako ni kuchomwa moto. Sisi ni wajumbe wa ule Mji wa mraba, ule Mji ambamo Mwana-Kondoo ndiye Nuru. Sisi ni sifa za Mwenyezi Mungu zilizotamkwa, ambao Yesu Kristo amewakomboa kwa neema Yake."

<sup>552</sup> Shetani, toka, na umwache kila mgonjwa aliye hapa ndani, katika Jina la Yesu Kristo. Mikono mitakatifu iliyokombolewa, kwa sababu wao wanaliamini Neno nao ni sifa za wazo la Mungu, sasa mikono hiyo imewekewa mmoja juu ya mwingine. Huwezi kuwashikilia tena. Toka, katika Jina la Yesu Kristo!

<sup>553</sup> Sasa, katika Jina la Bwana Yesu, sasa, Yeye yuko hapa. Neno Lake linasema yuko hapa. Uwepo wako na imani yako vinanena, kwamba, wewe ni mmoja wa wajumbe. Hata kila kipimo cha kijiografia tunachoweza kuonyesha, ndivyo ilivyo. Hivi mnaweza kutambua ya kwamba ninyi ni wana na binti za Mungu waliokombolewa? Mnatambua *huku* ndiko Nyumbani kwenu? *Huku* ndiko mnakoelekea.

<sup>554</sup> Hiyo ndiyo sababu mlikuja hapa, hiyo ndiyo sababu mlimjia Kristo, mnajilisha kwenye Neno Lake. Na kama mnaweza kuwa na wakati kama huu, hapa, kwa sifa Zake tu zilizotamkwa, itakuwaje tutakapoingia katika Uwepo Wake? Loo! litafurahisha sana! Kila mmoja wenu ana haki ya kuwaponya wagonjwa, kuwekea wagonjwa mikono. Kila mmoja wenu ana haki ya kubatiza.

<sup>555</sup> Kama kuna mtu hapa ambaye hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kidimbwi ni wazi.

<sup>556</sup> Hivyo ndivyo tu utakavyofaulu, a-ha, hiyo ni kweli, ni kutii kila Neno. Kumbukeni, sehemu moja ndogo ya Neno, hapo mwanzo, ilisababisha kila dhambi duniani. Yesu alisema, "Kila atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hiki, ama kuongeza neno moja Kwake, hataingia." Jina Lake litaondolewa kwenye Kitabu, mara atakapofanya jambo hilo.

<sup>557</sup> Na hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa, Kanisani, vinginevyo ila katika Jina la Yesu Kristo. Kama hujabatizwa namna hiyo, afadhali ufanye hivyo.

<sup>558</sup> "Loo!" unasema, "haileti tofauti yo yote." Ililetä kwa Hawa.

<sup>559</sup> Shetani alisema, "Loo! hakika, Mungu, unajua Mungu . . ." Lakini, alifanya hivyo. Yeye alisema hivyo.

<sup>560</sup> Yeye alimpa Petro funguo za Ufalme, na kile kilichofungwa hapo Pentekoste kimefungwa milele. Hiyo ndiyo sababu Bibi-arusi alitokea apate kuonekana kabla tena, mara ya pili; hakuna budi kuwe na Kanisa lililoitwa litoke katika siku ya mwisho, kama ilivyokuwa katika siku ya kwanza, kama hilo kabisa. Mti umechipua kutoka kwenye mizizi yake, kufikia kwenye Mti wa Bibi-arusi, kama ulivyofanya wakati ule; kipeo cha Mungu tena, kama nilivyosema Jumapili mbili zilizopita, kupelekwa kwenye Mji ule.

Mungu awabariki. "Sasa naamini."

<sup>561</sup> Shetani ameshindwa. Yeye anajua. Yeye yuko duniani, anatembea kama simba angurumaye. Haitachukua muda mrefu kufikia atakapokwisha kabisa, amekwisha. Yeye anajua wakati wake. Anatembea kama simba angurumaye.

<sup>562</sup> Lakini, kumbukeni, yule Mfalme wa Amani anasimama karibu; yule Mtu Mmoja wa Mungu aliye Mkuu. Mjenzi Hodari wa utu wangu, Mjenzi Hodari aliyenijenga nilivyo mimi, aliyekujenga ulivyo wewe, yuko hapa. Kama Mjenzi hodari, Ambaye anajua jinsi ya kujenga nyumba yote nzima, mahali pake panapofaa, ni nani anayejua vizuri zaidi kuliko Mjenzi Hodari? Naye yuko hapa kujithibitisha, Mwenyewe, yuko hapa.

<sup>563</sup> Sasa limewekwa misingi juu ya imani yako. Amini, amini tu!

Ninaelekea kwenye Mji ule mzuri  
 Bwana wangu ameuandalia walio Wake;  
 Ambako wote Waliokombolewa wa nyakati  
 zote  
 Wataimba "Utukufu!" wakikizunguka Kiti  
 Cheupe cha Enzi  
 Wakati mwingine ninatamani Mbinguni sana,  
 (Wakati haya yote yatakapokwisha)  
 Na utukufu ule nitakaouona kule:  
 Itakuwa ni furaha jinsi gani nitakapomwona  
 Mwokozi wangu,  
 Katika Mji ule mzuri wa dhahabu!

<sup>564</sup> Kumbukeni, kanisani, usiku wa leo, watakuwa wakifanya ushirika. Kama uko hapa mjini, bado, ungetaka kuja, tungetaka kuwa pamoa nawe. Ni kumbukumbu la kile tutakachokula, moja ya siku hizi, pamoa Naye.

<sup>565</sup> Ninawapenda ninyi. Sijui jinsi ya kuonyesha jambo hilo. Ninasikiri ninyi ni chumvi ya dunia. Nami ninasikia mwenendo wenu mzuri kati ya walimwengu, hivyo hilo linanipa matumaini zaidi kwenu.

<sup>566</sup> Lakini, wazieni, kundi hili dogo, zuri kama tulivyo, litavunjika-vunjika mojawapo ya siku hizi. Tatalitamani moyoni jambo hili. Lakini kama ikitokea kwamba mmoja wetu aage dunia kabla hatujakutana tena, tataninii... .

Nitakulaki asubuhi, upande mwangavu wa mto

Wakati huzuni zote zimeondolewa;

Nitakuwa nimesimama karibu na lile lango, milango itakapofunguliwa wazi,

Mwishoni mwa siku ndefu na yenye kuchosha ya maisha.

Nitakutana nawe asubuhi, karibu na mto mwangavu,

Mimi mara nyngi...?...kule chini karibu na mto, na, kwa furaha tutafanya upya urafiki wetu, (nitawaona wakati huo, nitawajua)

Utanijua kwenye ile asubuhi, kwa tabasamu langu,

Nitakutana nawe asubuhi, kwenye ule Mji, Mji uliojengwa mraba.

<sup>567</sup> Je! mnaupenda? “Hata twonane!” Sasa hebu tusimame. *Peleka Jina La Yesu*, tupe sauti yake.

<sup>568</sup> Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye si ni wa ajabu? [“Amina.”] Mnaamini hii ni Kweli? [“Amina.”] Unaelekea huko, kwa neema ya Mungu? [“Amina.”] Mpaka tutakapofika kule:

Wewe peleka Jina la Yesu  
Liwe silaha yako;  
Utakapojaribiwa,  
Lilia Jina hilo.

Hilo tu ndilo la kufanya, mpaka tutakapowaona tena. Vema.

Peleka Jina la Yesu,  
Ko kote uendako;  
Litafurahisha moyo,  
Peleka uendako.

Thamani, na tamu!  
Ni Jina Lake Yesu;  
Thamani, na tamu!  
Ni Jina Lake Yesu.

<sup>569</sup> Sasa, ilinibidi kuruka Ujumbe wangu. Siku moja, Bwana akipenda, nitarudi na kuchukua hii “milango,” na kuichukua, mnaona, ambapo tunaweza kuwa na wakati zaidi. Mmekuwa mkipiga makelele juu ya kutokaa muda mrefu vyatukosha. Tumekaa, leo. Ni joto. Lakini, sasa, Mungu awabariki. Ninapenda huko kuimba.

<sup>570</sup> Jirani fulani hapa, alisema, hivi majuzi walipozima kipaza sauti, kasema, "Nilifurahia huo Ujumbe sana, lakini kwa nini mlikatiza huko kuimba kuzuri, mnaona, huko nje?" Kwa hiyo, ewe jirani, kama unasikiliza asubuhi ya leo, ninafikiri tuna majirani wazuri kuliko wote walioko Jeffersonville. Tunaegesha magari yetu mbele ya nyumba zao na kila kitu; hawasemi neno juu yake; tunaendelea tu. Kwa hiyo, tunawashukuru sasa.

<sup>571</sup> Loo, jinsi Yeye alivyo wa ajabu! Mungu awe pamoja nanyi sasa.

...Jina, na tamu!

Ni Jina Lake Yesu.

Hata twonane...

<sup>572</sup> Na tuinamishe vichwa vyetu. Mchungaji ataturuhusu tuondoke, katika muda kidogo. Mungu awe pamoja nanyi!

...twonane Kwake kwema, (kwenye ule Mji  
mkuu, kwenye kile Kiti kikuu cha Enzi)

Hata twonane huko juu!

Mungu awe nanyi daima.



*MAKAO YA BAADAYE YA BWANA ARUSI WA  
MBINGUNI NA BIBI-ARUSI WA DUNIANI SWA64-0802*

(The Future Home Of The Heavenly Bridegroom And The Earthly Bride)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 2 Agosti, 1964, katika Maskani ya Branham, huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)